# MTINDO KATIKA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI

**SHULE YA FANI NA SAYANSI ZA JAMII**

**NA**

**MINING JUDITH CHEMUTAI**

**C50/CE/23089/2011**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**MEI, 2016**

**IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine.

Sahihi…………………………………………………..Tarehe……………………………….

Mining Judith Chemutai.

**WASIMAMIZI**:

Tasnifu hii imetolewa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi.

Sahihi…………………………………………………...Tarehe…………………………………….

Dkt. Edwin Masinde.

Sahihi…………………………………………………Tarehe……………………………………

Dkt. Joseph Maitaria.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu Davies Odwenya Epale na watoto wangu Moses Okware Epale, Felix Imodoi Epale na Sharlyne Ajuma Epale.

**SHUKRANI**

Shukrani zangu za mwanzo ni kwa Maulana aliyenijalia uhai, afya njema na nguvu za kuifanya kazi hii iliyokuwa na vizingiti vingi vilivyonisibu lakini kwa rehema zake Mola, niliweza kufua dafu.

Shukrani zangu za pekee ni kwa wasimamizi wangu Dkt. Edwin Masinde na Dkt. Joseph N. Maitaria kwa maelekezo yao, maoni, fikra , maarifa, mapendekezo, ushauri na mwongozo wa kila anuai walionipa uliopelekea kazi hii kufaulu.

Vile vile, nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili na lugha nyingine kwa mafunzo yao ya kozi mbalimbali zilizoniwezesha kuteua mada hii ili kuitafitia. Shukrani zangu za pekee ni kwa Dkt. Wafula aliyetoa mwanga kuhusu miongozo ya nadharia iliyofanya kazi hii kupata mwelekeo.

Aidha, nawashukuru wanagenzi wenzangu tuliosoma pamoja nao kozi hii kwa ushauri wao na maarifa waliyonipa. Shukrani zangu za pekee zimwendee Wafula Cathrine, Barasa na Charity kwa maarifa mengi niliyopata kutoka kwao na ushauri ulionitia moyo kutekeleza kazi hii.

Namshukuru pia mwalimu wangu mkuu Bw. Parklea Kibet aliyeniruhusu kila mara kwenda kuishughulikia kazi hii nilipohitajika chuoni.

Shukrani zangu za dhati ni kwa mume wangu mpendwa Davies O. Epale kwa kujitolea kwake kwa udi na uvumba hasa kifedha, kimawazo na mawaidha yaliyochangia pakubwa kufanikisha kazi hii.

Istoshe, nawashukuru wazazi wangu Vincent Chebus Mining na Mary Nafula Mining bila kuwasahau wazazi wangu wakwe Joseph Epale na Leonarah Epale kwa mawaidha yao yaliyonitia moyo na matumaini ya kukamilisha kazi hii.

Nikitamatisha, shukrani za kipekee pia ziwaendee ndugu zangu Salome , Sammy,Joy,Mercy,Caro, Harriet, Lilian,Moses na Philip kwa kunitia moyo kutekeleza kazi hii bila kuchoka. Pia, nawashukuru wifi zangu Everlyne, Dorry,Lydia , Clare na shemeji Edmond kwa mawaidha yao yaliyonichochea kutia bidii za mchwa katika kazi hii.

**IKISIRI**

Utafiti huu ulishughulikia Mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.Tumetumia diwani mbili za hadithi fupi .Diwani hizi ni *Pendo la Heba*(1996)na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine(2004)*. Pia tulibainisha na kujadili mitindo husika inayotumiwa katika hadithi fupi za Kiswahili.Mitindo hii ni ;taswira,tashbihi,tashihisi na majazi.Vile vile,tulionyesha matarajio ya athari zinazotokana na matumizi hayo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kimtindo.Ili kupata data faafu,tulitumia mbinu kusudio. Data ya kimsingi ilipatikana maktabani kutokana na kazi teule. Aidha, mtafiti alisoma makala, vitabu na tasnifu ili kupata ujumbe unaohusiana na mada hii.Pia,alizingatia mtandao ili kufahamu masuala ibuka yanayohusiana na hadithi fupi.Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia iliyoteuliwa na matokeo yaliyowasilishwa kwa njia ya maelezo. Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi imeshughulikia maswala ya kikaida kama vile suala la utafiti,malengo ya utafiti,maswali ya utafiti,sababu ya kuchagua mada,misingi ya nadharia,yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Katika sura ya pili ,fasili, historia na maendeleo ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili hadi sasa yameangaziwa.Pia,sifa na vijenzi vya utanzu wa hadithi fupi ya kisasa ya kiswahili vimeelezwa kwa upana. Sura ya tatu imeeleza matumizi ya taswira na matarajio ya athari zinazotokana na matumizi hayo katika diwani teule za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Sura ya nne nayo imeshugulikia matumizi ya tashbihi,tashihisi na majazi katika diwani teule za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili .Vile vile,matarajio ya athari zinazotokana na matumizi ya mitindo hii husika yameelezwa. Sura ya tano ambayo ni ya mwisho ni hitimisho na matokeo ya utafiti kwa jumla.Pia, sura hii imetoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye.Utafiti wetu ulifua dafu na kwa uhakika umetoa mchango wake katika upanuaji wa uelewa wa utanzu huu wa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ambao umechipuka tu baada ya tanzu nyingine za fasihi andishi na bado unaendelea kukua.

**ABSTRACT**

The main objective of this research was to study the styles in swahili short story. We used two short story books which are; *Pendo la Heba(1996)* and Mayai *Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004)*. In our research, we also outlined and discussed different kinds of styles. This are; similes, personification, imagery and symbolism. We also showed the expected effects of the use of these different kinds of styles in choosen short story books. We were guided by stylistic theory in our research. To get the expected data, we used purposive sampling in a way that it rhymed with the choosen literature set books. The data was mainly obtained in the library from selected text. The researcher also read books, thesis and other materials related to the topic of study. The researcher also used the internet to familiarize herself with current issues related to the study. Analysis of data was guided by the tenents of the theory mentioned. The findings were presented by descriptive method. Chapter one dealt with the statement of the problem, objective of the study, research questions, importance of the study, the tenents of the theory, literature review and research technique methods. In chapter two, we also discussed the origin, history and the development of modern swahili short stories up to then. The characteristics of the modern swahili short stories was also explained at large. However, the tenents which build up the short story were discussed especially how it is relevant to short stories. Chapter three explained the use of imagery and its expected effects as used in the selected modern swahili short stories. Chapter four, analysed the use of similes, personification and symbolism in the selected short stories. Its expected effects was also discussed. Chapter five is the conclusion and summary of the research results. This chapter has also suggested research topics to be researched on in future.

## MAELEZO YA ISTILAHI

| | | |
|---|---|---|
| Mtindo | : | Ni dhana inayotumiwa Katika uchambuzi wa fasihi kuelezea jinsi mwandishi anavyoiunda kazi yake. |
| Hadithi fupi | : | Ni masimulizi yanayojifunga katika idadi ndogo ya wahusika na tukio fulani maalum. |
| Hadithi fupi ya kisasa | : | Ni masimulizi yaliyoandikwa kwa kinathari juu ya tajriba fulani ya maisha. |
| Nadharia ya kimtindo | : | Ni nadharia inayoeleza kwamba kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Kwavyo, jinsi mtunzi atumiavyo lugha, husaidia kutoa ujumbe wake kwa wasomaji. |
| Diwani | : | Ni mikusanyiko yoyote ya kazi za kifasihi. |
| Njia ya kimakusudi | : | Ni mbinu ya uteuzi wa sampuli inayodhamiria tu idadi fulani ya watu waliohusika au vitu vilivyohusika . |

**YALIYOMO**

IKIRARI ..................................................................................................... ii
TABARUKU ..................................................................................................... iii
SHUKRANI ..................................................................................................... iv
IKISIRI ..................................................................................................... v
ABSTRACT ..................................................................................................... vi
MAELEZO YA ISTILAHI ..................................................................................................... vii
YALIYOMO ..................................................................................................... viii
**SURA YA KWANZA ..................................................................................................... 1**
1.0 Utangulizi ..................................................................................................... 1
1.1 Suala La Utafiti ..................................................................................................... 4
1.2 Maswali Ya Utafiti ..................................................................................................... 5
1.3 Malengo Ya Utafiti ..................................................................................................... 5
1.4 Sababu Ya Kuchagua Mada ..................................................................................................... 5
1.5 Upeo na Mipaka ..................................................................................................... 6
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..................................................................................................... 7
1.7 Misingi ya Nadharia ..................................................................................................... 14
1.8 Mbinu za Utafiti ..................................................................................................... 19
1.8.1 Muundo wa Utafiti ..................................................................................................... 19
1.8.2 Mahali pa Utafiti ..................................................................................................... 19
1.8.4 Ukusanyaji wa Data ..................................................................................................... 21
1.8.5Uchanganuzi wa Data ..................................................................................................... 21
**SURA YA PILI ..................................................................................................... 23**
**FASILI, HISTORIA NA MAENDELEO YA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI ..................................................................................................... 23**
2.0 Utangulizi ..................................................................................................... 23
2.1. Fasili mbalimbali za hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ..................................................................................................... 23
2.1.1Mgogoro unaohusu hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ..................................................................................................... 25

2.2 Historia na maendeleo ya hadihi fupi ya kisasa ya Kiswahili hadi sasa..........................27
2.3 Sifa za Hadithi Fupi ya Kisasa ya Kiswahili..................................................................37
2.3.1Sifa ya ufupi katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili..............................................37
2.3.2Sifa ya uasili katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ..............................................38
2.3.3 Sifa ya umoja katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ...........................................38
2.3.4 Ubanifu na mbano katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ................................ 39
2.3.5 Ubora wa mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.................................. 39
2.3.6. Tendo dhahiri katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ....................................... 40
2.3.7Maudhui katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ............................................... 40
2.3.8 Umbo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili .................................................... 41
2.3.9 Wakati katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili................................................... 41
2.3.10 Mandhari katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ............................................. 42
2.3.11 Usimulizi katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili............................................. 42
2.4. Vijenzi vya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ....................................................... 42
2.4.1. Dhamira ................................................................................................................. 43
2.4.2 Maudhui ................................................................................................................. 44
2.4.3 Mandhari ................................................................................................................ 44
2.4.4 Mtindo .................................................................................................................... 45
2.4.5 Wahusika ................................................................................................................ 45
2.4.6 Muundo wa hadithi fupi........................................................................................... 46
2.5 Hitimisho ................................................................................................................. 51
**SURA YA TATU ......................................................................................................... 53**
**MATUMIZI YA TASWIRA NA ATHARI ZINAZOTOKANA NA MATUMIZI HAYO KATIKA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI. ................................................ 53**
3.0 UTANGULIZI ......................................................................................................... 53
3.1 Taswira ..................................................................................................................... 53
3.2 Matumizi ya Taswira ................................................................................................ 54
3.2.1 Pendo la Heba .......................................................................................................... 54
*3.2.2 Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* .................................................... 67
3.3 HITIMISHO.............................................................................................................. 82
**SURA YA NNE ............................................................................................................ 83**

**MATUMIZI YA TASHBIHI,TASHIHISI,MAJAZI NA ATHARI** ........ **83**
**ZINAZOTOKANA NA MATUMIZI HAYO KATIKA HADITHI FUPI YA** ........ **83**
KISASA YA KISWAHILI ........ 83
4.0 UTANGULIZI ........ 83
4.1 Matumizi ya Tashbihi ........ 83
4.1.1 Pendo la Heba ........ 83
4.1.2 Mayai Waziri wa Maradhi ........ 88
4.2 Matumizi ya Tashihisi ........ 94
4.2.1 Pendo la Heba ........ 94
4.2.2 Mayai Waziri wa Maradhi. ........ 97
4.3. Matumizi ya Majazi ........ 101
*4.3.1 Pendo la Heba* ........ 101
4.3.2 Mayai Waziri wa Maradhi ........ 106
4.4 Hitimisho ........ 108
**SURA YA TANO** ........ 109
**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO** ........ 109
5.0 Utangulizi ........ 109
5.1 Muhtasari ........ 109
5.2 Matokeo ya Utafiti ........ 110
5.3 Mapendekezo ........ 111
**MAREJELEO** ........ 113

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Hadithi fupi ni moja wapo ya tanzu za fasihi andishi kama vile tamthilia, riwaya na ushairi. Wamitila (2000:54) anaeleza kuwa hadithi fupi ni ile ambayo inashughulikia suala fulani kwa muhtasari na huwa aghalabu na mhusika mmoja anayejitokeza wazi ingawa hakuzwi kama ilivyo katika novela au riwaya. Anaendelea kusema kwamba hadithi fupi haina upana wa kimaudhui wala uchangamano wa kimuundo unaotokana katika tanzu nyingine za kinathari. Hata hivyo, hadithi fupi hutofautiana kwa urefu na wakati mwingine kigezo cha urefu huwa hakiwezi kutegemewa katika kuainisha utanzu huu.

Kulingana na Poe (1938) ameeleza sifa za hadithi fupi kama vile utanzu ulio mfupi ambao unahitaji kusomwa kwa kikao kimoja tu. Anasisitiza lengo la hadithi fupi ambalo ni kuzua athari moja iliyo ya kipekee. Upekee huu unaufanya utanzu huu kujitegemea na kutofautishwa na riwaya.

Mohochi (9197) anasema kuwa utanzu wa hadithi fupi umepuuzwa.Hata hivyo,ni utanzu muhimu sana katika jamii ya leo kama tanzu nyingine za fasihi andishi.

> Nayo hadithi fupi ya kisasa katika Kiswahili ni sehemu ya maendeleo ya jamii.Licha ya uchanga wake,huu ni utanzu ambao unaendelea kukua kwa haraka sana.Katika nchi za Ulaya na Marekani, hadithi fupi ya kisasa inayo historia ya takribani miaka mia moja hamsini. Katika ukanda wa Afrika Mashariki, utanzu wa hadithi fupi za kisasa umeweza kutumiwa kwa miaka mingi.

MCOnyango anazipa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili miaka ya kati ya karne ya ishirini. Anasema kuwa zilianza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili karne hii. Anaendelea kusema kwamba tafiti za awali kuhusu hadithi fupi katika lugha ya Kiswahili zilifanywa na watu kama vile Albert Gerard. Gerard anasema kuwa tangu miaka ya elfu moja na mia tisa hamsini tafsiri za Kiswahili za hadithi fupi za Kichina na Kirusi zilianza kutokeza.

Naye Ntiba ameongeza kwa kusema kuwa kuwepo kwa ngano za kikwetu zinazokaribiana na hizi tafsiri, kulifanya kuzipokea kuwa rahisi. Baada ya kupokea tafsiri hizi, waswahili walianza kutunga na kuandika hadithi zao fupi.

Istoshe, hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili imeanza hivi juzi na inapaswa kushughulikiwa kitaaluma.Vile vile, Mohochi (1997:4) anasema kwamba, ilipofika karne ya kumi na nane na kumi na tisa, hadithi fupi za kisasa zilianza kuchapishwa kwenye magazeti na katika majarida.

Naye Mohochi (1997) anadai kwamba, hadithi fupi ni utanzu mgeni bali historia yake imejengeka katika ngano. Hadithi fupi hizi zimekuwa sehemu za utamaduni wa jamii. Hivi sasa hadithi fupi zinajitokeza sio katika hali ya ngano lakini katika miundo na mtindo tofauti. Mohochi anatilia maanani kuwa ngano za hapo awali zilitumia mtindo tofauti na hizi za hadithi fupi za kisasa.  Maandishi  yalipoibuka yalizua njia nyingi za kuwasilisha kazi za sanaa. Hadithi fupi kama kazi ya sanaa iliathiriwa katika uwasilishaji wake, ndipo pana haja kutafitia mtindo katika utanzu huu ili ueleweke zaidi.

Aidha, mwandishi wa hadithi fupi huwa na lengo anapoiandika hadithi yake. Mbali na lengo, mtunzi vile vile hulazimika kuteua msamiati wa maneno yatakayotumiwa kuibua ujumbe wake kwa njia inayowavutia wasomaji. Kwa hivyo, huteua mtindo mwafaka ambao huutumia kuwasilisha maudhui ya kazi yake kwa jamii. Swala hili linasisitizwa na wanamtindo kwamba lugha ndicho chombo tekelezi kinachosaidia katika kuelewa ujumbe uliokusudiwa kama vile tashihisi, tashbihi, majazi miongoni mwa fani nyinginezo zinazoweza kuathiri hadithi fupi ya Kiswahili. Kila mtunzi huwa na namna yake ya kuandika kazi yake.

Jambo hili kuhusu mtindo pia limeangaziwa na Mbatiah (2000:xiii) anayesema kwamba watunzi wa kimagharibi na hasa Marekani wanatukuza mtindo katika kazi za kifasihi. Nao watunzi wa Afrika kama vile Ngugi wa Thiong'o na wengine wanatilia mkazo mtunzi kutumia mtindo au fani kama chombo cha kumwezesha kuwasilisha hisia zake kwa wasomaji au wasikilizaji. Kwa hivyo, mtindo anaoutumia mtunzi kutoa ujumbe wake au dhamira yake ni vipengele vinavyotegemeana.

Kwa ajili hii, utafiti huu utakusudia kuchunguza mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili, kama njia anayoitumia mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Hivi ni jinsi vile Leech na Short(1981) wanavyosisitiza mawazo ya Lorge kuwa,lugha inayotumika hutekeleza mujukumu tofauti na kupitisha ujumbe kwa urahisi.

Hata hivyo,Mohochi (1997) anasema kwamba, japo hadithi fupi ni utanzu wa kale zaidi katika jamii baada ya ushairi, umuhimu wake ndio umepata kubainika na kuthaminiwa. Utunzi wake vile vile, ndio umeweza kushika kasi. Aidha, uhakiki wake umeanza kutiliwa maanani. Ni katika muktadha huu ambapo utafiti huu ulilenga

kuhakiki mchango wa mtindo katika kuwasilisha maudhui ya mwandishi wa hadithi fupi teule za kisasa za Kiswahili.(*Pendo la Heba na Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.)*

## 1.1 SUALA LA UTAFITI

Utafiti huu umejishughulisha na uchunguzi wa mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Suala la mtindo ni muhimu katika usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi, hasa hadithi fupi za Kiswahili. Hii ni kwa sababu maudhui yanayosawiriwa hufungamana na mtindo anaoutumia mwandishi. Hivyo, kazi yoyote ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Kwa hivyo, mwandishi anavyotumia lugha husaidia kutoa ujumbe wake kwa wasomaji au wasikilizaji.

Aidha, jambo hili linashadidiwa na Coombes anayesema kuwa wahakiki wengi husisitiza maudhui na kusifu kazi kutokana na maudhui yaliyojadiliwa huku wakisahau lugha au mtindo uliotumiwa katika kueleza maudhui hayo. Kwa hivyo, mwandishi lazima aonyeshe umaarufu kwa matumizi ya lugha wala si maudhui tu.Kwa ajili hii,matumizi ya mtindo huwasaidia watunzi kujenga dhamira na mafunzo.

Kwa sababu hii, uchunguzi huu ulidhamiria kubainisha jinsi mtindo hutumiwa katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili kuwasilisha ujumbe. Pia, hadithi fupi ya kisasa ni miongoni mwa kazi za hivi karibuni katika maendeleo ya utunzi wa fasihi ya Kiswahili.Hivyo,kulikuwa na haja ya kubainisha namna hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili inavyoshughulikiwa ili utanzu huu ueleweke vyema zaidi hasa tukitambua kwamba bado unakua.

## 1.2 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu ulingozwa na mwaswali yafuatayo:

1. Ni mitindo ipi inayotumiwa katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili?
2. Mitindo hiyo hutumiwa vipi katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili?
3. Je, matarajio ya athari zinazotokana na mitindo hiyo ni yapi?

## 1.3 Malengo Ya Utafiti

Utafiti wetu umetimiza malengo yafuatayo:

1. Kubainisha mitindo inayotumiwa katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.
2. Kuonyesha namna mitindo hiyo inavyotumiwa katika kusawiri hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.
3. Kuonyesha matarajio ya athari zinazotokana na matumizi hayo.

## 1.4 Sababu Ya Kuchagua Mada

Wamitila (2002) anasema kwamba hadithi fupi ni utanzu ambao umezuka baada ya tanzu nyingine za fasihi andishi na haujashughulikiwa na wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili.Tafiti nyingine ambazo zimefanywa zimechunguza vipengele kama vile,dhamira,maudhui na wahusika katika tanzu nyingine za fasihi hasa riwaya,tamthilia na ushairi huku utanzu wa hadithi fupi ukipuuzwa. Haya maoni ya Wamitila japo yameegemezwa zaidi katika hadithi fupi kwa jumla, yanaweza kutumiwa katika maendeleo ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

Ntiba (2011) miongoni mwa wengine aliangalia dhana ya mtindo katika hadithi fupi kwa ujumla.amezingatia vipengele vingine kama vile dhamira na maudhui, kipengele cha mtindo kikijadiliwa kwa ufupi tu. Hivyo, bado pana haja ya utanzu huu wa hadithi fupi kutafitiwa zaidi.

Mtunzi anapoitunga kazi yake, hulazimika kuchagua mtindo wake atakaoutumia vizuri. Hivyo basi, mtunzi anayechagua mtindo wake vizuri atawasilisha kazi yake ya utunzi vilivyo. Ataweza kufikia malengo ya kazi yake ipasavyo. Kutokana na kauli hii, ndipo tulitaka kuchunguza mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ili kuonyesha namna watunzi wanavyofanikisha kazi zao.

*Pendo la Heba na Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, kwa ambavyo diwani hizi ni za kisasa, kujua mtindo uliotumiwa katika diwani hizi itawafaa wahadhiri, wanagenzi wa vyuo vikuu na hata wanaounda mitaala kuhusu namna ya kuchambua hadithi vilivyo kwa kuelewa mtindo unotumika katika diwani ya hadithi fupi ya Kiswahili husika. Jambo hili litarahisisha uchambuzi kuhusu usawiri wa ujumbe.

## 1.5 Upeo na Mipaka

Kuna vipengele vingi vya mitindo,lakini utafiti huu ulishughulikia kipengele cha taswira, tashbihi, tashihisi na majazi katika diwani teule ya *Pendo la Heba*(1996) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.Haikuwa lengo la utafiti huu kulinganisha na kulinganua mitindo ya hadithi fupi za awali na za kisasa.Kiini cha utafiti huu ni kuonyesha mitindo inayotumiwa na waandishi wa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.*

Diwani ambazo tulishughulikia ni mbili za *Pendo la Heba na Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004)*. Hizi ni baadhi ya hadithi fupi zinazoingia katika kumbo la hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.Mitindo iliyotumiwa katika diwani hizi ni vielelezo vya sifa zinazoweza kutumiwa katika kuainisha utanzu wa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

Diwani hizi mbili zimeteuliwa kwa sababu zilikuwa na data iliyohitajika kutosheleza mahitaji ya utafiti huu.Ziliteuliwa kimakusudi.Hii haimanishi ya kwamba hakuna hadithi fupi za kisasa nyinginezo ambazo zingeteuliwa.

## 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Kuna kazi nyingi ambazo zimeandikwa na waandishi mbalimbali kuhusu mtindo wa hadithi fupi. Kazi hizi zinahusiana na mada hii teule na baadhi ya nyinginezo zilitupa pia mwelekeo ingawa zinatofautiana kwa upande mwingine.

Mwanzo kabisa kuna utafiti uliofanywa na Mukopi (2005), unaohusu sifa za usimulizi zinavyoingiliana na sifa za uandishi katika hadithi fupi za Kiswahili. Utafiti huu uliweza kutofautiana na wetu hasa zile sifa za usimulizi alizoeleza na zile za uandishi hazikufanana na zile tulizoshughulikia. Kwa sababu, katika utafiti wetu tulishughulikia kipengele cha taswira, tashbihi, tashihisi na majazi.Hata hivyo, uliweza kutupa mwelekeo mwafaka.

Naye Ntiba (2011), ametafiti kuhusu namna dhamira za waandishi wa hadithi fupi huathiri uteuzi wa mtindo wanaotumia kuwasilisha jambo. Mwishowe, ameangalia namna mazingira yanavyoathiri utunzi wa waandishi. Kipengele cha jinsi dhamira za

waandishi huathiri mtindo, kilifaa sana katika utafiti wetu. Mitindo aliyoshughulikia ilitoa mwangaza zaidi katika utafiti huu.

Aidha, utafiti wa Muusya (2012), ulikuwa wa manufaa makubwa sana katika utafiti wetu. Muusya, alitafiti kuhusu mandhari katika hadithi fupi.Amechunguza mitindo inayotumiwa na waandishi wa hadithi fupi kujenga mandhari mbalimbali. Amekitazama kipengele cha taswira, tashbihi na majazi, vipengele ambavyo utafiti wetu ulishughulikia pia.Vipengele hivi vilifaa pakubwa sana katika utafiti wetu.

Lodge (1972) amezungumzia mtindo kwa upana. Anasema kwamba mtindo ni jinsi ya kujieleza. Ni ule upekee wa mwandishi wa kueleza kwa kisanaa mambo ya kawaida. Anaendelea kusema kuwa, uteuzi wa tamathali za semi na msamiati hutegemea mtindo wa msanii binafsi. Kulingana na maelezo yake, mtindo wa msanii mmoja utakuwa tofauti na wa mwingine na hii ndio sababu tunaweza kufanya utafiti wa aina moja lakini kazi za waandishi mbalimbali. Maelezo yake Lodge yalifaa utafiti wetu.Hii ni kwa sababu utafiti huu unahusu matumizi ya tamathali za semi katika hadithi fupi. Tofauti iliyopo ni jinsi vile alizungumzia mtindo kwa jumla katika kazi ya fasihi kwani hajarejelea tanzu husika.

Mtafiti mwingine aliyefanya utafiti wa kusaidia ni Osore (1994), ambaye alitafiti mtindo katika riwaya. Alihakiki riwaya za *Suleiman Mohamm*ed kiisimu. Alichunguza jinsi maudhui ya riwaya ya Mohammed yanavyobainika kupitia viwango vya sintaksia, semantiki na isimu amali. Osore hakuegemea sana kwenye tamathali za semi kwa kuwa aligusia tu taswira na methali. Sehemu ya tamathali za semi hasa kipengele cha taswira katika utafiti wake Osore kilitufaa kwa kiasi. Tofauti

iliyopo baina ya utafiti wake na wetu ni kwamba yeye alijadili mtindo katika riwaya kwa misingi ya kiisimu ilhali sisi tulishughulikia mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili tukiegemea katika misingi ya kifasihi.

Istoshe, Senkoro (1988), amechambua mashairi kadha wa kadha kwa kuzingatia mtindo wa watunzi pamoja na dhamira zao. Alifanya hivyo kwa kutazama baadhi ya mashairi ya wanajadi na wanamabadiliko. Kazi yake ilikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu ilitupa mwelekeo. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na yetu kwa sababu sisi tulishughulikia mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili naye aliangalia mtindo katika ushairi.

Pia, Senkoro ameeleza mtindo katika fasihi kwa jumla. Anasema kwamba mtindo ni ile namna ambayo msanii hutunga kazi na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kaida zilizofuatwa za kimapokeo au za kipekee. Anasisitiza msanii kuzingatia mtindo kwa kuipa kazi yake sura ya kifani na maudhui kwa njia ambayo mtunzi mwingine asingeweza kuipa hivyo, hata kama jambo linalozungumziwa na watunzi wawili ni lile lile moja. Iwe tu kwamba, ni upande wa maudhui, msimamo na mtazamo wa kiulimwengu wa msanii ndio ubainishao mtunzi huyo na mwandishi mwingine.

Senkoro ameainisha sehemu kuu za mtindo, maudhui na fani.Pia nafsi ya mtunzi inayojitokeza katika muoano wa haya maudhui na fani. Ameelezea aina mbalimbali za mtindo kama vile mtindo wa kishairi hasa, mtindo wa kiuandishi wa habari, mtindo wa kihotuba na mtindo wa kidhahania. Kazi ya Senkoro ingawa

imezungumzia fasihi kwa ujumla na kueleza mitindo mingine ambayo sisi hatukushughulikia, ilitupa mwelekeo katika kazi yetu kwa kiasi fulani.

Naye Senkoro (1982:28), anasema kuwa mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hatimaye hutokeza au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo. Anaongezea kwa kusema kwamba ni ile namna ambayo mwanasanaa huipa kazi yake ya kifasihi sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwingine asingeweza kuipa hivyo, hata kama jambo linaloongelewa na wasani hawa wawili ni lile lile moja. Mtindo kimsingi humwezesha mtazamaji, msomaji au msikilizaji atambue msanii wa kazi ya fasihi inayohusika.

Diyanni (2000), asema kwamba mtindo katika hadithi fupi ni utambuzi wazi wa upekee wa mwandishi kama vile uso au sauti yake inavyoweza kutambuliwa kimakusudi ikiashiria upekee wao waandishi kwa kuutazama ulimwengu. Anasisitiza kwamba mtindo katika hadithi fupi ni uteuzi wa maneno unaofanywa na mwandishi, mpangilio wake katika sentensi na hali ya kuwepo na kutokuwepo kwa lugha ishara hasa za ulinganisho. Anaeleza dhana ya mtindo kama ubunifu na ishara za ulinganishi zinazotumiwa na waandishi wa hadithi fupi kuwasilisha upekee wa mtazamo wao kuhusu ulimwengu. Anatamatisha kwa kusema kuwa, mtindo ni utambulisho wa kila mwandishi kama mwongozo wa kuelewa kazi zao. Kazi hii ya Diyanni ilitufaa katika utafiti wetu kwa vile aligusia matumizi ya ishara za ulinganisho, vipengele ambavyo kazi yetu inashughulikia.

Naye Elizabeth (1998), ameeleza mtindo kama jinsi mwandishi anavyoteua na kuwasilisha ploti, msuko, wahusika, mtazamo na mandhari ya hadithi. Anasema kwamba lugha ndicho chombo ambacho hutumiwa na waandishi kuwasilisha sehemu hizi na kwa sababu hii, kuchanganua mtindo wa mwandishi katika hadithi fupi ni kutazama jinsi alivyotumia lugha. Elizabeth anaona kwamba, baadhi ya matini ya lugha yanayochangia mtindo ni uteuzi wa maneno na tamathali za usemi. Anatilia mkazo suala hili kwa kusema kwamba, unaposimulia utani kwa ujuzi wa lugha ya hali ya juu utafurahiwa na utaiacha hadhira ikicheka. Pia, mbinu za mwandishi na athari mbalimbali zilizopo zinaweza tambuliwa na zikusaidie kupata mwelekeo wa kuitafsiri hadithi fupi. Maelezo yake Elizabeth yanafaa utafiti huu kwa vile anaangazia suala la tamathali za semi ambalo utafiti wetu ulishughulikia.

Wamitila (2003), asema kwamba mtindo katika hadithi fupi ni dhana inayotumiwa katika uchambuzi wa fasihi kuelezea jinsi mwandishi anavyoiunda kazi yake. Anasema ni yale mazoea ya mwandishi fulani. Aeleza kuwa mtindo ni mazoea ya kuandika au kuzungumza. Anasisitiza kwamba mazoea haya yanahusu; usimulizi wa mwandishi, tamathali anazotumia, lugha yake, anavyomaliza hadithi zake, mpangilio wake wa matukio, taswira, usawiri wake wa wahusika, majina yao na kadhalika.Vile vile, anaeleza kwamba kuhusiana na matumizi ya lugha, msomaji anapaswa kuangalia tamathali za semi kama vile tashbihi, tashihisi, sitiara, chuku, tabaini, tanakuzi, tasfida na taswira.Vipengele hivi humwezesha mwandishi kulielezea jambo au tukio kwa njia inayoacha athari kubwa kwa wasomaji.

Hata hivyo, anasisitiza kuwa msomaji aweze, si kutambua tu tamathali hizo, bali aweze kuelezea umuhimu wake, kama zinafaa au hazifai. Wamitila pia alielezea

vipengele vingine vya matumizi ya lugha kama vile misemo, nahau, methali na msamiatia. Kazi hii ya Wamitila ilifaa utafiti wetu pakubwa hasa baadhi ya vipengele vya tamathali za semi.

Wamitila (2002), amezungumzia ubora wa mtindo katika hadithi fupi. Anasema kwamba hadithi fupi inatarajiwa kuwa na mtindo wa kuvutia msomaji na kumfanya anaswe na hadithi yenyewe. Aeleza kuwa mbinu zinazotumiwa na mwandishi zinastahili kumshawishi msomaji. Pia, ufupi wa utunzi utakifanya kipengele hiki cha mtindo kujitokeze waziwazi. Anasisitiza mwandishi kuzitumia mbinu za utunzi na lugha zitakazomwezesha alifikie lengo lake kwa njia inayokokoteza lisemwalo. Maelezo ya Wamitila (2002), yalifaa kazi yetu kwa vile alielezea kipengele cha lugha katika hadithi fupi. Kipengele ambacho tulikishughulikia katika utafiti wetu.

Wamitila (2002)katika kamusi yake ameelezea dhana ya mtindo kwa jumla katika fasihi. Asema, mtindo ni dhana inayorejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Ni jinsi vile mwandishi fulani anavyojieleza katika kazi yake. Asema kuwa uchunguzi wa mtindo ulihusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za semi, balagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya zake na uakifishi wake. Aliongezea kuwa kila mwandishi ana mtindo wake wa pekee. Amewataja waandishi kama vile Mohamed S. Mohamed, M.S. Mohamed na Shafi Adam ambao kazi zao zinatofautiana kwa vile ambavyo wametumia mitindo tofauti katika utunzi wao wa riwaya na ushairi. Maelezo haya ingawa yamezungumzia mtindo kwa jumla katika fasihi andishi, kuna vipengele au baadhi ya sifa zilizofaa utafiti wetu hasa tamathali za semi ambazo tumezishughulikia katika hadithi fupi.

Njogu (2007), ameeleza mtindo katika kazi ya fasihi kwa jumla. Anazumgumzia kuhusu uhakiki wa kazi ya fasihi. Asema kuwa kuna kipengele cha mtindo ambacho huzingatia jinsi mbalimbali au mbinu ambazo mtunzi anazitumia kusema au kusimulia hadithi yake. Asema kwamba kuna matumizi ya nyimbo, barua, Ishara, taswira, hadithi ndani ya hadithi, mchezo ndani ya hadithi, mashairi na mitindo ya kutumia picha. Aendelea kusema kwamba katika fasihi tumezoea kuchambua kazi kifani na kimaudhui. Kifani humaanisha kuchunguza ule ufundi wa kisanaa unaotumiwa kuiwasilisha ile kazi kwetu. Anasema kuwa hapa huchunguza matumizi ya lugha kwa kuangazia usanii wa lugha, matumizi ya tamathali za semi, sentensi ndefu na fupi, msamiati na matumizi ya kuchanganya ndimi. Kazi hii ya Njogu ingawa haijikiti katika utanzu wa hadithi fupi sana, ilifaa utafiti wetu.

Kwa mujibu wa Msokile (1992), mtindo ni namna ambavyo mwandishi huipa kazi yake sura ambayo kifani na kimaudhui itakuwa tofauti na nyingine iliyoandikwa na mtu mwengine.

Katika mtandao, unaeleza mtindo kama kipengele cha hadithi fupi. Unasema kwamba mtindo unahusu jinsi mwandishi anateu usemi wake, muundo wa sentensi, ufundi wa kifasihi na muwala. Mtandao umetoa mfano wa mwandishi kwa jina Hemingway ambaye ameandika kwa kutumia sentensi fupi na matumizi ya maneno yaliyo rahisi, naye mtunzi George Orwel kwa upande mwingine alitumia sentensi zilizo ndefu nyingine zikirudiwarudiwa.

Vile vile, mtandao unaelezea kwamba katika uandishi wa hadithi fupi, mtindo wa mwandishi huwasilishwa kwa uteuzi wa mbinu za kifasihi zinazotumika kuifanya

hadithi fupi iwe na taswira, ishara, mafumbo, tashihisi, kinaya, nahau na mbinu nyingine za kifasihi.

Mwandishi wa hadithi fupi ana mtindo wa kipekee unaotokana na uteuzi wake wa usemi, muundo wa sentensi, mawazo yake, dayalojia, mbinu za kifasihi na muwala. Mtindo hutokana na usemi, uteuzi wa maneno na matumizi ya lugha rahisi. Kwa mfano, kama anatumia sentensi ndefu, zisizokamilika, sahili au changamano au zinazojirudiarudia kama vile mwandishi Cormac McCarthy katika kitabu chake cha 'The Road' alitumia sentensi nyingi zisizokamilika kuelezea hadithi yake.

Njia nyingine ya mwandishi kubainisha mtindo wake wote tukirejelea mtandao ni kwa kiasi cha mawazo anayowasilisha kwa msomaji kama anaelezea kwa kina au anatumia ufupisho wa masimulizi au matumizi ya nathari hapa na pale.

Kwa hivyo, mtandao unaeleza kuwa mtindo katika hadithi fupi huonyesha matini yaliyomo ya dayalojia ama mawazo anayotumia mtunzi yanayomwelezea zaidi mhusika katika hadithi hasa asili yake, elimu, motisha yake na kile ambacho kila mhusika anaamini kuhusu ulimwengu. Mengi ambayo mtunzi husema yanatokana na tajriba na upendeleo wa mtunzi. Kazi hii ya mtandao ilifaa kazi yetu hasa vipengele vya taswira na tashihisi ambavyo vimeelezewa katika mtandao.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Nadharia ya uhakiki wa kimtindo inaeleza kwamba kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Kwa hivyo, mwandishi anavyotumia lugha husaidia kutoa ujumbe wake kwa

wasomaji au wasikilizaji. Lugha ndicho chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii zote za wanadamu. Wanamtindo wanasisitiza umuhimu wa lugha kama chombo tekelezi kinachosaidia katika kuelewa ujumbe au maudhui yaliyokusudiwa.kwa ajili hii, nadharia hii itatuwezesha kubainish mitindo inayotumiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili kusawiri ujumbe katika diwani teule.

Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ya uhakiki wa kimtindo ni Leech na Short (1981). Kulingana nao, mhakiki lazima azingatie matumizi ya lugha katika muktadha fulani.Wanasisitiza ufafanuzi wa De Saussure aliyetofautisha 'Langue' na 'Parole' ambapo "Langue" ni sheria wanazozijua wazungumzaji ilhali "Parole" ni matumizi ya lugha au sheria hizi husika. Wanasisitiza dhana ya" parole" kuliko "Langue". Wanadai kwamba mtindo ambao ni matumizi ya lugha humtambulisha mtunzi.

Hata hivyo, lugha katika kazi za fasihi huazimia kuleta uhusiano na majukumu ya kazi ya sanaa.Wanaeleza kuwa lugha huwezesha mwandishi kuwasilisha mawazo yake kimaandishi kwa hadhira na hivyo, mtindo ni kigezo mojawapo cha kupimia kufaulu kwa kazi za usanii.

Leech na Short wanaendelea kueleza  kwamba katika mawasiliano, kuna njia fulani maalum za matumizi ya lugha ambazo hupata mantiki kwa kurejelea muktadha wa matumizi yake. Pasipo kuuelewa muktadha unaorejelewa katika matumizi, mawasiliano hayo huenda yakachukuliwa kuwa yasiyo na maana na mantiki. Leech na Short wanaeleza kuwa, mnenaji huzingatia kwamba kuna ushirikiano fulani kati yake na mnenewa hivi kwamba, anachokisema huongozwa na kile ambacho msemewa anakifahamu awali.

Vile vile, muktadha na mazingira yanayofahamika na msemewa huwa na mchango mkubwa kuhusu namna ambavyo msemewa atateua maneno atakayotumia kuwasilisha ujumbe wake. Nadharia ya kimtindo pia imeendelezwa na wataalamu mbalimbali kama vile: Crystal na Davy (1969), Lodge (1988), Chapman (1982) miongoni mwa wataalamu wengine. Hivyo, Leech na Short (1981) wanatamatisha kwa kusema kwamba, mpangilio au uteuzi wa mawazo ya mwandishi ni muhimu. Kwa hivyo, mtindo ni sehemu ya ujumbe.

Kulingana na Crystal na Davy (1969), wanaeleza mtindo kama tabia ya mtu kuhusu namna ambavyo anatumia lugha ili kuwasilisha ujumbe wake. Hii inatokana na sababu kwamba kila mtu ana njia ya kipekee ya kufanya mambo na hakuna watu wawili ambao wana tabia ile ile.Vivyo hivyo, kila mtu ana upekee wake wa kutumia lugha.

Aidha, wanaeleza kuwa mtindo hudhihirisha matumizi ya kipekee ya lugha ya mtunzi. Hivyo basi, kubainisha mtunzi mmoja na mwingine.Vile vile, wanaeleza mtindo kwa mtazamo wa kifasihi ambapo lugha inaweza kutumiwa kwa njia inayoonekana kuwa ya uwazi lakini ikawa na maana ya kitamathali au maana ya kifasihi. Maana ya kifasihi inahitaji ufundi au uelewa wa muktadha na mazingira yanayorejelewa ili kueleweka na walengwa.

Naye Lodge (1988), anasema mtindo ni jinsi ya kujieleza. Ni ule upekee wa mwandishi kueleza kisanaa mambo ya kawaida. Uteuzi wa tamathali za usemi na msamiati hutegemea mtindo wa msanii binafsi. Hulingana na mawazo yake. Ni wazi kwamba mtindo wa msanii mmoja utakuwa tofauti na mwingine, ndio tunaweza

kufanya utafiti wa aina moja lakini kazi za waandishi tofauti. Lodge anasisitiza kwamba chochote mwandishi anachokifanya ni kwa kutumia lugha.

Ntiba (2011), anaeleza mtindo kama njia ya mwandishi ya kuwa na tajriba yake, kuupanga na kuuwasilisha uelewa na fikra zake. Anaongezea kwa kunena kwamba mtindo unahusisha mambo kama vile uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, ishara za uashiriaji, mpangilio wa sentensi na aya pamoja. Hivyo basi, kila mwandishi huwa na mtindo wake wa uandishi.

Kwa mujibu wa Halliday (1971), mwandishi wa hadithi fupi hujaribu kuzingatia sura ya mtindo bora utakaoleta mvuto kwa wasomaji. Mtindo mara nyingi hutegemea ubunifu wa fikra za mwandishi. Uteuzi wowote wa lugha ni mtindo. Ni bora kuelewa lugha iliyotumika katika kazi husika na uelewa wa jumla kuhusu ulimwengu.

Naye Ngara (1982), ameorodhesha mbinu mbalimbali ambazo huchukuliwa kama mihimili ya nadharia hii hasa katika mtazamo wa kifasihi. Mbinu hii, ni kiwango cha msamiati ambapo mtafiti hujishughulisha na uteuzi wa mbinu kama vile jazanda, tashbihi na istiari.

Naye Chapman (1982), akinukuliwa na Kairu (2005), anashikilia kuwa hakuna mtu anayeweza kujadili fasihi bila kuzingatia lugha.Wahakiki wanaojishughulisha na mambo kama maudhui, wahusika na tajriba ya mwandishi huongozwa na lugha.Baada ya kurejelea fafanuzi tofauti tofauti zilizotolewa na waandishi mbalimbali kuhusu nadharia ya mtindo ni muhimu kusema kwamba, tuliweza kutumia nadharia hii katika utafiti wetu kwa sababu ilituwezesha kubaini matumizi ya mitindo iliyotumiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili teule hasa katika

kusawiri ujumbe wa waandishi wa diwani hizi teule. Vile vile nadharia hii ilitusaidia kuweza kumtambua na kumtofautisha mwandishi mmoja na mwingine. Isitoshe tuliitumia kama kigezo cha kupimia kufaulu kwa kazi ya waandishi wa diwani teule tulizochanganua.Tulitumia nadharia hii katika kazi yetu na si nadharia nyingine yeyote ile kwa sababu nadharia zile zingine hazishughuliki na swala la mtindo

Kwa jumla, kutokana na nadharia hii, tuliweza kupata mihimili ifuatayo iliyotuongoza katika utafiti huu.

1. Wanamtindo husisitiza umuhimu wa lugha kama chombo tekelezi kinachosaidia kueleza ujumbe uliokusudiwa.

2. Kiwango cha msamiati ambapo mtafiti hujishughulisha na uteuzi wa mbinu kama vile jazanda, tashbihi na Istiari.

3. Mwandishi wa fasihi lazima aonyeshe umaarufu katika kutumia matumizi ya lugha ya kuvutia.

Mihimili ambayo tumeorodhesha hapo juu ilitusadia kujibu maswali ya utafiti wetu.

Mihimili ya kwanza miwili ilitusaidia kubainisha na kuonyesha matumizi ya mitindo inayotumika katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili za *Pendo la Heba* (1996) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Mhimili wa tatu ndio ulifanikisha kubainisha matarajio ya athari zinazotokana na matumizi hayo ya mitindo katika hadithi fupi husika.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo.Ulieleza namna watunzi walivyotumia tamathali kama vile taswira, tashbihi, tashihisi na majazi katika kusawiri na kutoa ujumbe.

### 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani. Tulisoma maandishi na machapisho kuhusu uhakiki wa mtindo katika hadithi fupi, maandishi yaliyohusu nadharia ya kimtindo yalisomwa na machapisho yote muhimu kuhusu utafiti huu ili kuimarisha lugha, suala la utafiti na mbinu za utafiti. Utafiti huu ulifanywa katika maktaba ya chuo kikuu cha Kenyatta, chuo kikuu cha Nairobi na chuo kikuu cha Moi.Ni katika vyuo hivi ambapo kulikua na urahisi wa kupata habari kuhusu nadharia, makala kuhusu mbinu za utafiti kwa jumla.pia kulikuwa na habari kuhusu tahakiki na yaliyoandikwa kuhusu mada.

Habari hizo zilitosheleza mahitaji ya utafiti husika.hivyo,mtafiti hangezuru kila chuo kikuu humu nchini Kenya na kwingineko.

### 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli lengwa ilikuwa diwani teule za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Diwani hizi ni *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine (1996) na Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004)*. Katika diwani hizi mna jumla ya hadithi ishirini na sita. Hapa utafiti ulitumia hadithi kumi na tatu. Katika kuteua hadithi hizi pia tulitumia

mbinu kusudio. Hii ni kwa sababu mbinu kusudio hulenga sampuli maalumu kwa sababu ya data yake. Hivyo mbinu hii huongozwa na sifa ya kipekee katika sampuli husika. Sampuli hii ilitosheleza data tuliyohitaji katika utafiti huu. Hizi diwani mbili zilikua na data iliyotosheleza mahitaji ya utafit wetu. Kutoka katika kila diwani hadithi mahsusi ziliteuliwa kama ifuatavyo:

*Pendo la Heba na Hadithi Nyingine:*

| | |
|---|---|
| Pendo la Heba | Ukurasa 1-10 |
| Mtembo | Ukurasa 27-31 |
| Jitu la kisasa | Ukurasa wa 39-43 |
| Jahanamu | Ukurasa 44-50 |
| Genge | Ukurasa wa 51-59 |
| Kisasi | Ukurasa 66-71 |

*Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*

| | |
|---|---|
| Siku ya Mganga | Ukurusa wa 20-37 |
| Kachukua Hatua Nyingine | Ukurasa wa 38-49 |
| Mayai Waziri wa Maradhi | Ukurasa wa 63-77 |
| Msamaria Mwema | Ukurasa wa 78-89 |
| Fumbo la Mwana | Ukurasa wa 90-97 |

| | |
|---|---|
| Ngome ya Nafsi | Ukurasa wa 98-114 |
| Mkimbizi | Ukurasa wa 115-124 |
| Ndimi za Mauti | Ukurasa wa 125-135 |

### 1.8.4 Ukusanyaji wa Data

Mbinu iliyotumika katika ukusanyaji wa data katika utafiti huu ni usomaji wa kina na kisha kwa kunukuu sehemu ambazo zina matumizi ya taswira, tashbihi, tashihisi na majazi.Matumizi ya vipengele hivi katika hadithi fupi ya kisasa yanasaidia kubainisha mitindo ya waandishi wa hadithi fupi teule.Kwa mfano kutokana na aina za taswira na tamathali za lugha,unapata kuelewa ni mitindo gani ambayo imetumiwa na waandishi wa hadithi fupi teule.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa kwanza iliainishwa na kupangwa kulingana na matumizi ya taswira, tashbihi, tashihisi na majazi. Kisha mtafiti alichanganua mitindo iliyotumiwa kwa kuzingatia matumizi ya tamathali kama vile taswira, tashbihi, tashihisi na majazi. Aidha, alizingatia maswali ya utafiti, matarajio ya athari zinazotokana na taswira zilizotumiwa, tashbihi, tashihisi na majazi.Vile vile, uchanganuzi uliongozwa na mihimili ya nadharia.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Data

Matokeo yaliyokusanywa yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Katika kufanya haya yote, mtafiti alitumia mifano yenye kurejelea namna mtindo ulivyotumiwa katika utunzi wa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

# SURA YA PILI

# FASILI, HISTORIA NA MAENDELEO YA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, lengo letu kuu ni kushughulikia fasili, historia na maendeleo ya hadithi fupi ya Kiswahili hadi sasa. Pia, sifa maalum za utanzu huu zimejadiliwa kwa mapana. Hatimaye, vijenzi vya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili, vimeangaziwa ili kuonyesha uwiano uliopo kati ya vijenzi hivi na matumizi ya mtindo katika hadithi fupi.

## 2.1. Fasili mbalimbali za hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Kumekuwa na utata kuhusu fasili ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahli.Wataalamu wengi hawajakubaliana ni nini maana hasa ya hadithi fupi ya Kiswahili. Hata hivyo, ingawa imeshinda juhudi zote kutoa fasili mwafaka au moja itakayofaa, kuna waandishi tofauti tofauti ambao wameibuka na fasili ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

Mbatiah (2000) anaeleza kwamba hadithi fupi ni masimulizi yaliyoandikwa kinatharia juu ya tajriba fulani ya maisha, aghalabu mwandishi huiwasilisha tajriba hiyo kwa kujikita katika tukio moja.Uti wa mgongo wa utanzu huu ni hadithi.

Wamitila (2002) asema kuwa hadithi fupi ni utungo mfupi wa kinathari unaojishugulisha na suala fulani kuu. Ni utungo wenye wahusika ambao hawakuzwi

kwa kina na unaotumia mbinu za kimaelezo za kibunifu zenye uelekezi wa kiwango cha juu. Utungo huu hautumii mandhari kwa upana na una athari kuu moja. Istoshe, unaweza kusomwa kwa kikao kimoja kifupi tu.

Naye Wamitila (2002) anaeleza hadithi fupi kama hadithi inayojifunga kwa idadi ndogo ya wahusika na tukio fulani maalumu. Anaongezea kwa kusema kuwa hadithi fupi huwa haionyeshi mabadiliko ya sehemu na wakati wa matukio kwa upana.Aidha, haijiingizi kwenye undani wa wahusika. Hadithi fupi husomeka kwa kipindi kifupi sana.

Vile vile, Wamitila (2002) amefafanua hadithi fupi kama bustani ya kuchipuza vipaji vya waandishi wa tanzu nyinginezo kama vile riwaya, tamthilia na hata ushairi. Pia, anasema kuwa ni utanzu unaowakilisha kwa kiasi fulani sawia ya kimpito kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

Istoshe Poe (1938) ameeleza hadithi fupi kama utungo mfupi wa kinathari unaojishughulisha na suala fulani kuu. Kwayo wahusika ambao hawakuzwi kwa kina na unaotumia mbinu za kimaelezo na kiubunifu zenye uelekezi wa hali ya juu. Poe asema kwamba utungo huu, hautumii mandhari kwa upana na una athari kuu moja na unaweza kusomwa kwa kikao kimoja.

Kwa maoni yetu binafsi, hadithi fupi ni utanzu ambao hueleza matukio kwa ufupi. Hata hivyo, hadithi inayosimuliwa huwa ni fupi. Mwaandishi hutumia wahusika wachache kusawiri ujumbe husika. Bila shaka, mandhari hayawasilishwi kwa mapana sana kama ilivyo kwenye riwaya au tamthlia.Kwa hivyo, huwa ni hadithi ya kinathari inayosimuliwa kwa kifupi na huzungukia mhusika mmoja mkuu.Kwa hivyo,pana haja

ya kuweza kueleza mitindo inayotumiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili ili kubainisha tofauti ya utanzu huu na tanzu nyinginezo za fasihi andishi kama vile riwaya na tamthilia.

### 2.1.1Mgogoro unaohusu hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Aidha, tunapoelezea hadithi fupi ni nini, kumezuka mgogoro kati ya wataalamu wa fasihi kuhusu maana ya hadithi fupi. Mbatiah (2000:viii) aeleza kuwa wataalamu wengi wamekiri kwamba ni vigumu kuutolea fasili utanzu huu. Kwamba, fasili ambazo zimetolewa na baadhi ya waandishi na wahakiki zimechipuza mijadala mikubwa. Wengi wamekiri kwamba, ni vigumu kuutolea fasili utanzu huu. Mbatiah asema kwamba, fasili ambazo zimetolewa zimezua mijadala mikubwa na kwa wengine hazikubaliki kabisa .Istoshe, ameelezea mambo yanayosababisha utanzu huu kukosa fasili moja.

a) Hadithi fupi ni utanzu unaokaribiana na riwaya na kwa hivyo, tanzu hizi zote zinatumia stadi za utunzi zinazofanana.

b) Hadithi fupi ni utanzu mnyumbufu na mbadilifu sana kutoka taifa na mwandishi mmoja hadi mwingine.

c) Mtindo wa kuandika hadithi fupi hutofautiana sana kwamba matokeo yake ni ya aina nyingi sana.

d) Waandishi wengine wa hadithi fupi wametumia utanzu huu kama ngazi ya kupandia kwenye uandishi wa riwaya. Kwa ajili hii, utanzu huu aghalabu hunyimwa uhuru na huangaliwa kama ni mazoezi ya utunzi wa riwaya.

Naye Mohamed (1995) aeleza kuwa neno “fupi”ndilo linaloleta utata. Hivyo, asema kuwa ikiwa kuna hadithi fupi, riwaya nayo ni hadithi ndefu, kwa hivyo, ni kazi gani ya nathari ya urefu wa kiasi kipi inaweza kuitwa riwaya na kazi yenye ufupi gani inaweza kuitwa hadithi fupi. Hivyo, swala la urefu na ufupi limezusha matatizo mengi. Hapo mwanzo, suala la urefu lilitegemea kuwepo kwa viwango vya idadi ya maneno.Kama vile vipimo vya riwaya ya Ann Karenina (1875-76) au War and Peae za Toistoy (1865-72). Siku hizi, suala la urefu na ufupi halitiliwi maanani.

Mawazo haya yamechipuza kauli ya Edger Allan Poe asemaye kwamba hadithi fupi au riwaya hutambuliwa kwa uchangamano wake. Ndiposa Hathaniel Hawthoren (1938) asema kwamba:”Hadithi fupi si sura katika riwaya au tukio wala kituko ambacho kimechopolewa katika hadithi fupi au kisa kirefu, bali ni hadithi inayomtia na kumteka msomaji na kumfanya aamini kuwa ingeweza kuchambuliwa ikiwa itakuzwa na kuwa ndefu au kama itafanywa sehemu ya kazi kubwa.”

Kwa hivyo, hata kama kumekuwepo na kutoelewana kuhusu fasili ya hadithi fupi, bado utanzu huu unaweza kutambuliwa kwa kujikita katika sifa zake halisi. Ni katika muktadha huu wa wataalamu mbalimbali wanapojadiliana kuhusu utanzu huu, ndipo unapoendelea kupata mwangaza zaidi.Bila mawazo ya waandishi hawa, hadithi fupi isingeweza kukua na kufikia kiwango hiki.Pia, tusingeweza kuwa na waandishi wengi ambao wameandika vitabu vingi vya hadithi fupi. Hii imechangia pakubwa katika kueleweka kwa utanzu huu.

Hata hivyo, mwandishi mwenye athari kubwa katika hadithi fupi Poe,mbali na kuandika hadithi fupi, aliweza kutoa mapendekezo kuhusu mambo muhimu

yanayopaswa kuzingatiwa katika uandishi wa hadithi fupi.Mapendekezo haya yametumiwa na waandishi wengi kama mwongozo wa kuandika na kuelewa utanzu huu kwa mapana. IribeMwangi(2007:vii) ameyaeleza mapendekezo haya kama yanavyofuata:

a) Iwe na urefu wa kuweza kusomeka katika mkao mmoja.
b) Iweze kusababisha hisia au athari ya aina moja.\
c) Itumie maneno yatakayoitoa athari aliyonuia mwandishi.
d) Iwe na matumizi mazuri ya maneno ili kusababisha mgao wa kihisia kuliko wa kiakili.
e) Iwe fupi kiasi cha kutoathiri msuko wake kisanaa.

Mapendeikezo haya vile vile, yametilia mwanga fasihi ya hadithi fupi. Istoshe, mbali na ugumu wa kuutolea fasili na mwangaza utanzu huu, hali hii haichukuliwi kama kuwa ni udhaifu, bali huangaliwa kama kitovu cha nguvu zake. Pia, utanzu huu umeendelea kukua na kuimarika hasa waandishi wengi wakiutumia kama ngazi ya kupanda kwenye uandishi wa riwaya.

Istoshe tunapoelezea mitindo husika inayotumiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili tunauweka wazi utanzu huu kueleweka na kuendelea kukua.

**2.2 Historia  na maendeleo ya hadihi fupi ya kisasa ya Kiswahili hadi sasa**

Hadithi fupi ni utanzu ambao historia yake si ndefu sana kama tanzu nyinginezo za fasihi. Ni utanzu ambao umezuka baada ya tanzu nyingine kama vile, riwaya, tamthilia na ushairi. Utanzu huu unatekeleza majukumu muhimu katika jamii sawa na tanzu zile nyingine.

Kulingana na Mohocho (1997) anautazama utanzu wa hadithi fupi kama utanzu ambao historia yake imejengeka katika ngano ambazo ni za kale sana katika Jamii. Anasema kwamba, hadithi fupi hizo zimekuwa sehemu *ya utamaduni wa jamii, zilizosimuliwa miongoni mwa wavuvi, wawindaji, wanawake nyumbani, vyumba vya watoto na hata sasa madarasani. Jambo hili limesisitizwa na Mconyango* (2006) asemaye kuwa:

> "Utanzu wa hadithi fupi kama tujuavyo ni utanzu mchanga sana ukilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili. Utanzu mkongwe wenye ukuruba na utanzu huu mpya wa hadithi, ni ule wa hadithi za Waswahili za kupokezwa kizazi hadi kizazi yaani ngano."

Jamii zote ulimwenguni zinaona ngano kama utanzu wenye historia ndefu zaidi ya hadithi fupi. Ngano huwa na historia inayoanzia kwenye fasihi simulizi katika jamii zote. Ni vyema kuelewa hadithi fupi katika mwanda mzima wa tungo liitwalo hadithi, ziwe ni hadithi za kitamaduni (ngano) au za kisasa.

Naye Mwanzi (1987) anashikilia kuwa mzizi wa hadithi fupi ni masimulizi ya hapo awali ambayo yamekuwa na kuendelezwa hadi sasa.

Mohochi anatambua kuwa, muda huu wote, binadamu wamesimuliana hadithi fupi kwa ajili ya kuonya kuhusu tabia fulani katika jamii na kuwaburudisha wanajamii katika sherehe. Mohochi asema kwamba, hivi sasa hadithi fupi zinajitokeza sio katika hali ya ngano lakini katika miundo na mitindo tofauti. Anasisitiza kuwa ngano za hapo awali zilitumia mtindo tofatuti na hizi za hadithi fupi za kisasa. Hii ni kwa sababu ya kuzipokea kwa maandishi kazi za sanaa. Hadithi fupi kama kazi ya sanaa

iliathiriwa katika uwasilishaji wake.Istoshe, Mohochi(1997:63) katika makala yake yanayohusu "Hadithi fupi:Utanzu uliodharauliwa." anasema hivi:

> "Jamii nyingi zimekuwa na hadithi fupi katika masimulizi. Ngano ni aina ya fasihi ambayo ina historia ndefu sana katika jamii."

Kulingana na maoni yetu, utanzu huu wa hadithi fupi una historia fupi kwa sababu umechipuka tu baada ya tanzu nyingine za fasihi.Kwa ajili hii, hatuwezi tukaulinganisha na ngano ambazo zimekuwepo katika jamii tangu zamani. Ngano nyingi hazikuandikwa jinsi vile hadithi fupi zimeandikwa.Hata hivyo, hadithi fupi nyingi na zilianza kuandikwa vitabuni baada ya waandishi kutambua umuhimu wa utanzu huu katika jamii.Muundo wake ukiwa changamano, tofauti na ule wa ngano

Walipotunga hadithi hizi waliweza kutumia mitindo mbalimbali ya utunzi. Hivyo kuna haja ya kubainisha na kueleza mitindo hii ili kuweka wazi ujumbe husika katika tanzu za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

Aidha, kwenye utangulizi wa *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine (2000)* Mbatiah anaelezea akimnukuu Foster (1927:42) akisema kuwa hadithi fupi ni masimulizi juu ya matukio yalivyopangwa kama yalivyotukia. Hivyo basi, masimulizi ni msingi wa utanzu wa hadithi fupi. Hali hii inategemea jinsi msanii anavyopanga matukio yake kiwakati. Hata hivyo, hadithi fupi ni utanzu ambao ni wa kisasa, hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.

Nao Mohochi na Mbatiah wanatazama hadithi fupi kama kwamba msingi wake unatokana na ngano.Hivyo basi, katika fasihi ya Kiswahili, ngano za mwanzo

hazikuhusiana kamwe na utamaduni wa kigeni. Hadithi za mwanzo kabisa zilikuja na wageni na baadaye kutafsiriwa katika Kiswahili.

Hata hivyo, katika eneo la Pwani utamaduni wa wageni unajitokeza. Uislamu unajitokeza katika hadithi zilizotafsiriwa na baadaye kutungwa na Waafrika. Baadhi ya hadithi hizi ni kama vile *Hekaya za Abunuasi (1935)* zilizosimuliwa na Waswahili kama *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar (1989)*. Hadithi nyingine za hapo awali zilizotafsiriwa kutoka lugha ya kigeni hadi Kiswahili, zilikuwa za *Alfu lela Ulela (1928)* na *Kisiwa chenye Hasina (1929).*

Hadithi nyingi za mwanzo zilitukuza Uarabu, Uzungu na kuponda Uafrika. Zilimkejeli Mwafrika kwa kumwita mjinga. Hadithi hizi hatimaye zilishindwa kufanya kazi zilizofanywa na ngano za hapo zamani. Baadaye ilimbidi mwafrika atumie zile hadithi zilizomsawiri mwafrika, utamaduni wake na ujumla wa maisha yake katika jamii.

Kwa sababu hii, ilimbidi atunge hadithi ambazo zingetoa hali halisi ya mwafrika, itikadi zake, mila, hali ya kisiasa, hali ya kiuchumi na yote yaliyomzingira mwafrika ili kurejesha na kuiumba upya hali ya mwafrika iliyodharauliwa na wageni.

Kwa maoni yetu,ni kutokana na hali hii ya hadithi za mwanzo kuandikwa zikiwa na lengo la kuwakejeli Waafrika,ndiposa iliweza kuchochea waafika kujitosa katika bahari hii ya kuandika hadithi fupi hasa zile zilizokashifu wageni na kudumisha mila na desturi za wenyeji ambao ni Waafrika.Hali hii kwa upana, ilichangia kukua kwa hadithi fupi hatua kwa hatua.

Vile vile, kati ya jamii za Ulaya na Marekani, hadithi fupi ina historia ya takribani miaka mia moja hamsini.Msingi wa utanzu wa hadithi fupi, unahusishwa kwa kiasi kikubwa na mtunzi na mhakiki wa Kimarekani aliyefahamika kama Edgar Allan Poe. Anayejulikana kama mwasisi wa utanzu huu pamoja na mhakiki aliyefahamika kama Brander Mathews ambaye ndiye aliyetaja neno la Kingereza la "short story" (hadithi fupi) kwa mara ya kwanza.

Poe alitoa maelezo yake kuhusu hadithi fupi katika karne ya kumi na tisa. Kwa mujibu wa Wamitila (2002) fikra zake ambazo hunyemelewa sana, ni za mwaka wa 1842. Wamitila (2002) asema kuwa, utanzu huu umekuwa sana hasa kiuchapishaji katika fasihi za lugha nyingine za Ulaya ikilinganishwa na Kiswahili.Lakini hilo si suala la kushangaza ikikumbukwa kuwa, fasihi ya Kiswahili bado inakua. Hata hivyo, historia ya ukuaji wa utanzu huu katika fasihi nyingi inafanana.

Kulingana na maoni yetu ni kwamba, ingawa imesisitizwa kuwa hadithi fupi ina historia ndefu hasa katika nchi za Ulaya na Marekani, vile vile barani Afrika kuna hadithi fupi zilizoandikwa hapo awali. Hasa zile za *Hekaya za Abunuasi* mwaka wa elfu moja mia tisa thelathini na tano ambazo zilielimisha na kutoa mafunzo kwa jamii. Kwa sababu hii,ni thibithisho tosha kuwa hadithi fupi pia katika bara la Afrika zimeanza miaka mingi iliyopita.Kwa ajili hii ni muhimu kueleza mbinu ya mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

Karne ya 18 na 19, ilishuhudia hadithi fupi nyingi kuanza kuchapishwa kwenye magazeti na majarida mengi, yaliyowavutia watu wengi kuyasoma.Maelezo haya yamesisistizwa na Wamitila (2002) anayesema kuwa:

> "Utanzu huu umekuwa na kuchapisha magazetini katika fasihi za lugha nyingine, ikilinganishwa na Kiswahili. Ukuaji na maendeleo ya utanzu huu, unafafanuliwa katika fasihi ya mataifa mengi.Waandishi walianza kuandika hadithi hizi zikachapishwa magazetini na kusomwa na wengi.

Naye Mohochi anatoa mfano wa Poe kwa kutaja hadithi ya *'' The two Drivers"* ya Walter Scoff, iliyochapishwa katika *"Chronicles of Conagate"* mwaka wa 1927, kuwa hadithi ya kwanza ya kisasa katika lugha ya kiingereza. Hadithi fupi kama utanzu unaoweza kujisimamia ulianza kuchapishwa kwenye vitabu na kuwafikia wasomaji wengi katika jamii. Mohochi anataja hadithi za *Hekaya za Abunuasi* zilizochapishwa mwaka wa (1935) kama hadithi fupi za kwanza kuchapishwa Uswahilini.

Istoshe, katika eneo la Afrika Mashariki hadithi fupi za kisasa zilifikia miaka mingi baadaye. Kwa mujibu wa Mconyango (2006), Albert Gerard akiwa mtafiti aliyetambuliwa anazipata hadithi fupi za kisasa miaka ya kati ya karne hiyo ya ishirini.

Aidha, tangu miaka ya elfu moja mia tisa hamsini, hadithi fupi za Kichina na Kirusi, zilitafsiriwa na zikaanza kutokea na kuwepo. Kwa vile kulikuwepo na ngano za kikwetu zilizokaribiana na hizi tafsiri, ilifanya zikakubaliwa kwa urahisi.Baadaye, walianza kutunga zao. Kufikia miaka ya elfu moja mia tisa sitini, hadithi fupi za Kiswahili zilianza kutokeza katika magazeti hasa nchini Tanzania. Hadithi nyingine zikishiriki katika mashindano ya uandishi wa hadithi fupi zilisomwa katika idhaa ya BBC, jambo ambalo Wamitila (2002:67) anasema kwamba:

> "Hadithi nyingine zilizoshiriki katika mashindano ya uandishi wa hadithi fupi, zilichapishwa katika mifululizo ya *Mapenzi ni Kikohozi*,*Kinywa Jumba la Maneno* na *Pavumapo Papalilie."*

Anasisitiza kuwa diwani hizi za hadithi fupi ziliweka msingi wa kuandika na kuchapishwa kwa Hadithi fupi. Wamitila anatoa orodha ya diwani nyingine katika miaka ya sabini kama vile *Paarapanda Na Hadithi Nyingine (1974),* Uwike *Usiwike Kutakucha (1978)* za Ruhumbika, *Pepeta* na S. Yahya, *Zaka la Damu na Hadithi Nyingine* ya (BAMITA). Katika miaka ya themanini kulichapishwa diwani nyingine kama vile:

a) *Si Wazimu si Shetani (1978)* chake (S.A. Mohamed).
b) *Dhuluma na Hadithi Nyingine (1980)* cha Barshed.
c) *Twenzetu Macha*, inayotumia lugha ya mitaani na iliyojaa vicheksho.
d) *Tamaa Mbele na Hadithi Nyingine* na *Nipe Nikupe na Hadithi Nyigine* vya (A, Banzi).
e) *Nitakuja kwa Siri* cha M. Msokile.
f) *Hapa na Pale* cha Takiluki
g) *Jamila Mpenzi na Hadithi Nyinginezo* cha F.E.M.K. Senikoro) na
h) *Papa la Mji* cha J. Rutayisingwa.

Diwani zilizoshuhudiwa hivi karibuni miaka ya tisini hadi sasa ni kama vile:

(a) *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine (1997)* kilichohaririwa na Wafula na King’ei.
a) *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine (2000)* kilichohaririwa na Mbatiah.
b) *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004)* kimehaririwa na Wamitila.
c) *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine (2007)* kilichohaririwa na Walibora.

Hivi leo, utanzu wa Hadithi fupi umekita mizizi. Mohochi (2000) anaeleza kuwa baada ya hadithi fupi kuthibitishwa kama utanzu mojawapo wa fasihi andishi katika karne ya kumi na tisa, umeendelea kukua. Waandishi wengi wameshiriki kuandika hadithi fupi nyingi zinazoangazia maswala ya kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na hata ya kijamii.Kwa hivyo, tangu awali hadithi fupi ziliendelea na baadaye kupelekea kuchapishwa kwenye vitabu.

Grandasaigne (1985) anaeleza pia jinsi utanzu huu wa hadithi fupi ulivyoendelea kukua kila uchao.Anatambua kuwa, fanani wa fasihi simulizi wa hapo awali aliingiliana na hadhira yake ana kwa ana kuliko kama ilivyo sasa. Hivyo basi, hadithi fupi iliendela huku ikibadilika.Katika karne ya kumi na tisa. Hadithi fupi ilijisimamia na kujitenga kama utanzu wa kipekee ulio na sifa zake tofauti na tanzu nyingine.Kwa sababu hii ni vyema kubainisha mtindo unaotumiwa katika utanzu huu wahadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

Naye Mc Clare (1980) kuhusu utanzu huu wa hadithi fupi anasema kuwa katika maswala ya kiakademia, ushairi, tamthilia na riwaya zimesisitizwa zaidi. Hadithi fupi imejitokeza kama utanzu mahsusi wa fasihi andishi katika Karne ya kumi na tisa tu. Maoni yake yanakaribiana na ya Reid (1977) ambaye anasema kuwa, ni katika Karne ya kumi na tisa ambapo hadithi fupi imejitokeza kama utanzu maalumu wa fasihi andishi.

Reid anapinga vikali wale wanaodunisha utanzu huu kwa sababu ya ufupi wa hadithi zenyewe.Anasema kwamba, wingi wa kurasa si muhimu kuliko yale yanayojadiliwa. Reid na Mc Clare wanasema kwamba, utanzu huu wa hadithi fupi umeanza tu, karne

ya kumi na tisa.Hii ni kwa sababu hapo awali ulikuwa umepuuzwa na waandishi wengi.

Nayo maudhui yanayozongumziwa na waandishi, si kama ya hapo awali, kwani mabadiliko yametokea. Hadithi fupi hizi zimebadilika kulenga hali ya sasa hasa, maendenelo ya jamii katika siasa, teknolojia, hali ya kiuchumi na jinsi inavyoathiri binadamu wa hivi sasa.Kujadili mtindo katika hadithi fupi hizi ambazo zimekuwa na mabadiliko ni jambo muhimu kwa wanafasihi na jamii nzima.

Nao wahusika waliotumiwa katika hadithi hapo awali, wanatumiwa hata sasa. Waandishi hawa hawakupuuza yale ya zamani, bali waliyatumia na kuyaweka katika muktadha wa hali halisi ya maisha ya sasa hivi ili kuyasawiri maisha ya sasa ya binadamu. Hadithi fupi za kisasa zimeumbwa kutokana na uchumi na urembo wa umbuji wa uchache wa maneno ambayo mtunzi hutumia ili kueleza wazo au tukio moja katika hadithi.Kauli hii imesisitizwa na Parker (1966:88) anayesema kuwa:

> “ Hadithi fupi nzuri ni ile inayomwelekeza msomaji katika kuyaelewa maisha ya sasa na hata ya baadaye.”

Leo hii, tunapozungumzia suala la utanzu wa hadithi fupi baada ya hadithi fupi kuchapishwa kwenye vitabu, tafiti kadha wa kadha zimeweza kufanywa ili kukuza utanzu huu ambao bado unaendelea kukua. Baadhi ya tafiti hizi ni:

a) Fani katika hadithi fupi, (Mohochi, 2000).

b) Mtindo na maudhui katika hadithi fupi za Kiswahili (Mbutia, 2003).

c) Umahaluti katika hadithi fupi za Kiswahili (Mukopi, 2005).

d) Taathira ya Dhamira kwa mtindo katika haditha fupi (Ntiba, 2011).

e) Wahusika katika hadithi fupi (Mulewa, 2008).

f) Athari ya Mbinu rejeshi katika hadithi fupi (Musili, 2013 bado inatafitiwa).

Licha ya utanzu huu kuchipuka baada ya tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile, riwaya na tamthilia, unaendelea kukua kwa kasi.Kwa mujibu wa Mbatiah (2000) mbali na utanzu huu, kushughulikia maswala mengi ya kijamii, ni utanzu ambao umetambuliwa katika asasi za kielemu.Anasema ya kwamba, umuhimu wa utanzu huu utambuliwe kwa kufundishia hadithi fupi katika asasi za elimu

Kulingana na maelezo haya ya Mbatiah, ni maoni yetu kuwa baada ya hadithi fupi kutambuliwa katika asasi za elimu na kutahiniwa katika vyuo vikuu na shule za sekondari, ilichipuza waandishi wengi wa hadithi fupi.Vitabu vingi viliweza kuandikwa hali iliyopelekea utanzu huu kuendela kukua.Diwani ya kwanza kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa ikiwa ni ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004).* Kwa sasa inayotahiniwa ni *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine (2007)* yake Walibora.

Kwa upande mwingine, vyombo vya habari vikiwemo redio na magazeti vimeendelea kukuza utanzu huu wa hadithi fupi hasa kwa kuangazia maswala mbalimbali ya hadithi fupi yanayochapishwa na kuchambuliwa katika magazeti na redioni.Hii pia, imesaidia kukuza utanzu wa hadithi fupi.Mtindo unaotumiwa katika hadithi fupi hizi za kisasa unapobainishwa, unaweka wazi maudhui ya mwandishi na hii inawapa wanagenzi kuwa na uelewa mpana kuhusu kazi za fasihi zinazotahiniwa shuleni.

## 2.3 Sifa za Hadithi Fupi ya Kisasa ya Kiswahili

Kulingana naye Wamitila (2002a), hadithi fupi ni utanzu unaojitegemea na wenye wasifu wa kujitosheleza.Kwa mchango wetu, sifa hizi za utanzu huu zimewezesha wasomi kuweza kutambua utanzu huu kwa urahisi. Hata hivyo, sifa hizi pia zimeweza kutumiwa ili kuutofautisha utanzu huu na tanzu nyingine za fasihi andishi.Sifa hizi ni kama ifuatavyo:

### 2.3.1Sifa ya ufupi katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Sifa ya ufupi ni muhimu sana katika utanzu wa hadithi fupi. Kwa mujibu wa Wamitila (2002) ,kigezo cha kwanza cha kupima hadithi fupi kimo kwenye jina lenyewe. Ufupi,ni sifa inayoeleweka na wahakiki wa utanzu huu na katika fasihi za ulimweng.Kazi inayoainishwa kama hadhithi fupi, haina urefu wa riwaya.Hata hivyo, kuna baadhi ya hadithi fupi za Kiingereza ambazo ni ndefu sana.Kwa mfano zile za Edger Poe za *"The Murder of Usher"* ni ndefu kuliko riwaya.Kwa hivyo, lazima pawepo vipengele vingine vya kutumia ili kuainisha utanzu huu.

Henry anaeleza kuwa, hadithi inayochukuliwa kama fupi zaidi iwe na maneno kati ya 250 na 1500. Naye mwaasisi wa nadharia hii ya hadithi fupi, E.A Poe alipendekeza kuwa, hadithi fupi iweze kusomeka katika kikao kimoja kifupi cha nusu saa.Naye Grandsaigne anasema kwamba si lazima hadithi fupi izingatie ufupi au umbo, kwani kuna uhuru.

Kwa maoni yetu, hadithi fupi yoyote ile lazima iweze kutumia idadi ndogo ya maneno yanayobeba ujumbe unaokusudiwa na mwandishi. Kwa hivyo, sifa ya ufupi katika hadithi fupi ndicho kigezo kinachotumiwa kubainisha utanzu huu.

### 2.3.2Sifa ya uasili katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Hii ni sifa ambayo inaweza kutumiwa kwa kazi nyingi za kifasihi zinazopaswa kuwa kazi asilia za waandishi wanaohusika.Baadhi ya wahakiki wanaamini kuwa, kazi za kifasihi huathiriwa na kuathiriana kwa kiasi kwamba hatuwezi kuongea kuhusu uasili. Wahakiki kama Bakhtini na wengineo wanaamini kuwa mwandishi anapoandika huwa anajihusisha na matamko au mjadala wa usemaji wa waandishi waliomtangulia. Baadhi ya wahakiki wa umuundoleo pia wanaamini kuwa kazi za kifasihi haziwezi kukwepa kuathiriwa na kazi zilizotangulia.

### 2.3.3 Sifa ya umoja katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Suala la umoja ni muhimu sana katika utanzu huu. Poe anasema kwamba, hadithi fupi inapaswa kuzua athari ya umoja. Umoja huu hutokana na hadithi fupi kujihusisha na suala fulani kuu. Habari yoyote ambayo haifai kuendelezwa na ambayo haichangii athari hii haifai kuwekwa katika hadithi.Masimulizi huzungukia mhusika mmoja mkuu ingawa wahusika wengine huwepo. Lakini hubaki kuwa wachache sana. Pia, mwandishi wa hadithi fupi huwa hana uhuru wa kumjenga mhusika yeyote kwa kirefu au undani. Ni sehemu ndogo tu ya maisha ya mhusika hushughulikiwa. Kuwepo kwa wahusika wengi huhitaji muda wa kuwakuza na kuwaendeleza.

Hadithi fupi pia huwa na tukio moja kuu na hisia moja au mbalimbali zinazosababishwa na hali moja. Msomaji huhisi kwamba amepata wazo. Kwa vyovyote vile, hisia ya kutokana na hadithi huwa si zenye kubadilikabadilika. Tukirejelea tukio moja, kuna uwezekano wa kuwepo kwa vitukio vingine ambavyo huwa vya kulijenga tukio kuu.Kwa hivyo, tukio na hisia hubaki ile ile moja tu katika hadithi.Kulingana na sifa hii tunaweza kusema kuwa yale yote yanayoshughulikiwa kwenye hadithi yawe machache.

### 2.3.4 Ubanifu na mbano katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Katika hadithi fupi mtunzi hastahili kutoka nje ya mada.Mwandishi wa hadithi fupi huhitajika kuwakuza wahusika wake waonekane kama wahusika waliokuzwa kikamilifu. Kwa hivyo, hata ingawa tunawaona kwa kipindi kifupi tunahisi kuwa wamekamilika kabisa. Hata hivyo, katika utanzu wa hadithi fupi, sifa kama hii haina matokeo mazuri kwa sababu inaathiri ule umoja wa kazi inayohusika. Mtunzi anajitahidi kujifunga kwenye mada kuu bila ya kuyashughulikia maswala ambayo hayana mchango kwenye mada kuu. Vivyo hivyo, hadithi fupi haitarajiwi kutumia mbinu rejeshi kwa upana kama ilivyo katika utanzu wa riwaya au tamthilia ambapo urejeshi hutawala au hutumika kwa wingi.

### 2.3.5 Ubora wa mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Hadithi fupi inatarajiwa kuwa na mtindo wa kuwavutia wasomaji na kumfanya msomaji anaswe na hadithi yenyewe. Matarajio ya msomaji ni kuwa, mbinu zinazotumiwa na mwandishi zitamshawishi. Ufupi wa utanzu huu unakifanya

kipengele hiki cha lugha na mtindo kujitokeza waziwazi. Kwa kuwa mwandishi hana nafasi kubwa, anapaswa kuzingatia mbinu za utunzi na lugha zinazomfanya alifikie lengo lake. Hata hivyo, zipo hadithi fupi nyingi ambazo ni chapwa.Kulingana nasi, ni bora pia mtunzi kujikita katika mtindo ambao mbali na kumvutia msomaji, utamsaidia pia kusawiri ujumbe wake kwa hadhira lengwa.Hivyo,suala la mtindo hutegemea uwezo alio nao mwandishi.

### 2.3.6. Tendo dhahiri katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Hadithi fupi inaposomwa tunatarajia kuliona tendo linalotokea.Katika hadithi fupi, mgogoro lazima ujitokeze mapema ili hadithi fupi iweze kumnasa msomaji kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hali hii inasisitizwa na kauli ya Edger Poe aliposema kwamba, hadithi fupi haitakuwa hadithi fupi ikiwa hapana tukio kuu linaloendelezwa. Hii ni kwa sababu katika mgogoro huwa na mhusika anayetaka kitu fulani kisha anayepinga. Kati yao kuna mvutano.Mvutano huu ni msingi wa mgogoro unaotia hamu ya kusoma ili tujue ni nani atakayefanikiwa.

### 2.3.7Maudhui katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Mwandishi wa hadithi fupi lazima anuie kutoa ujumbe, funzo au rai kulingana na maisha ya jamii.Lengo kuu la kutunga hadithi fupi huwa ni kuwasilisha ujumbe kwa hadhira.Mwandishi hutia bidii kutumia umbo zuri, mtindo bora na fani nzuri ili kuboresha hadithi yake. Afanyapo hivi, huweza kuwasilisha ujumbe wake kwa njia inayovutia na kuacha athari fulani katika akili, fahamu, kumbukumbu na moyoni mwa msomaji.Ule ujumbe ndio mada au kiini cha hadithi.

Maudhui ni yale mambo muhimu anayozungumzia mwandishi katika hadithi yake. Maudhui yaweza kuwa juu ya swala lolote linalohusu jamii anamoishi mwandishi au amewahi kuwa na tajriba nayo.Yaweza kuwa maudhui ya siasa, utamaduni, dini, elimu, uchumi, maadili, teknolojia au matamanio ya jamii.Maudhui yanaweza kuwa ya kujaribu kuzindua jamii au kutahadharisha au kutambulishia jamii na mawezekano mapya. Hata hivyo, Kibera anasema kwamba mwandishi wa hadithi fupi hana uwezo na wakati wa kuzikuza dhamira zake na maudhui.

### 2.3.8 Umbo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Muundo wa hadithi fupi lazima uwe na mfuatano wa kimantiki na wenye ukamilifu.Wasomaji na wahakiki hutarajia hadithi nzima iwe na mshikamano unaofuma pamoja na kufanya kazi nzima kuwa kitu kimoja kilicho na upatanifu kuanzia mwanzo hadi mwisho.Wataalamu wengi wanaeleza kuwa,ili hadithi fupi ifikie ubora wake lazima vipengele vyake kama vile masimulizi, tukio,wahusika,mandhari na mawanda yake yaainishwe vilivyo.Vipengele hivi vinapaswa kuelezwa kwa kuvikutanisha bila kupoteza muda au nafasi ndogo aliyo nayo mwandishi.Upanuzi wa kipengele chochote unaweza kutatiza mshikamano na umbo la hadithi nzima.Kwa maoni yetu, umbo la hadithi fupi linastahili kuwa sahili.Kuwe na mwanzo, kati na mwisho.

### 2.3.9 Wakati katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Mwandishi wa hadithi fupi hana wakati wa kuelezea mambo, matukio, wahusika na migogoro kwa undani kama ilivyo katika riwaya.Kwa maoni yetu, mtunzi wa hadithi

fupi anastahili kutunga hadithi ambayo itasowma kwa muda mfupi hasa nusu saa.Hadithi ionyeshe hali ya mwandishi kuwasilisha wazo lake kwa muda mfupi kwa wasomaji.

### 2.3.10 Mandhari katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Aghalabu matukio ya hadithi fupi hutokea mahali pamoja tu, yaani hayahusishi sehemu nyingi kwa sababu msisitizo mkubwa uko kwenye tendo sio mahali.

### 2.3.11 Usimulizi katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Katika riwaya, mwandishi anaweza kutumia usimulizi changamano unaohusisha wahusika kadhaa. Katika hadidhi fupi, usimulizi huwa sahili kwa kuwepo kwa msimulizi mmoja au mhusika ambaye anatumiwa na mwandishi kama jicho la kuangalia na kupimia yanayotendeka.

Kwa ujumla sifa za utanzu wa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zinapoelezwa ni vizuri kubainisha mitindo inayotumiwa kuelezea sifa hizi husika.

## 2.4. Vijenzi vya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili

Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili huwa zimejengwa kwa vijenzi vyake maalumu.Vijenzi hivi kwa pamoja huleta mshikamano wa hadithi nzima.Vijenzi hivi muhimu ni:dhamira, maudhui, mandhari na wahusika.Sehemu hii itaonyesha jinsi vijenzi hivi vinavyouiana na mtindo katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.Vijenzi hivi huwiana sana na mtindo.Kwa hivyo,ni vigumu kuvitenga na dhana ya mtindo

jinsi vile anavyosema Mohamed(1995:94) kwamba vijenzi vya hadithi fupi huwa na mkondo mmjoa usiokuwa na matawi au vitawi. Hakuna ndani yake simulizi ambayo haihusiani moja kwa moja na mwelekeo wa mkondo mkuu wa hadithi ambayo kwa kawaida inamhusu mhusika mmjoa au wachache.

### 2.4.1. Dhamira

Dhamira ni wazo linalotawala kazi ya kifasihi. Dhamira ndilo wazo kuu ambalo huipa kazi inayohusika mshikamano. Elementi nyingine za kazi ya kifasihi huelezeka kwa kuonyesha uhusiano wake na dhamira. Tabia za wahusika huhusiana na hata hutegemea wazo ambalo mwandishi analijenga katika hadithi. Ukweli au uzito wa dhamira ya kifasihi hutegemea kiwango cha ukamilifu wa uhalisia kilichofikiwa na kazi inayohusika katika taswira yake ya kipengele cha maisha inachokimulika.

Dhamira inaweza kujitokeza waziwazi katika kazi ya kifasihi. Katika hadithi fupi, huweza ikatajwa mahali fulani katika masimulizi au katika hadithi nyingine. Dhamira huwa imefichana.Kwa hivyo, itampasa msomaji kuvuta fikra na kusoma hadithi mara kadha ili kupata fasihi fulani ya maisha.

Hata hivyo, kuna uhusiano mkubwa kati ya dhamira na dhana ya mtindo.Hii ni kwa sababu dhamira ya mtunzi na mtindo anaotumia mtunzi katika kutoa ujumbe wake ni vipengele vinavyotegemeana katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, dhamira ya mwandishi haiwezi kumfikia msomaji bila kuwepo na mtindo. Hii kauli imetiliwa maanani na Wamitila (2002) anayesema kwamba dhamira

huingiliana na vijenzi vingine vya kazi ya fasihi ili kuunda kitu kimoja.Vijenzi hivi ni pamoja na: msuko, mandhari, mtindo, wahusika miongoni mwa vijenzi vingine.

### 2.4.2 Maudhui

Maudhui ni jumla ya masuala yanayoshughulikiwa.Maudhui huwa ni ujumbe wa mtunzi katika kazi yoyote ya fasihi. Kijenzi hiki cha maudhui kina uhusiano mkubwa na dhana ya mtindo. Hii ni kwa sababu mtunzi hawezi kuwasilisha ujumbe wake kwa msomaji bila kuwasilisha kwa njia fulani yenye mvuto ambayo ni mtindo. Hii inasisitizwa na kauli iliyotolewa na waandishi hawa: Ngugi wa Thiong'o, Ale la Guma, Ezekiel Mphalele na wengineo wanaosema kwamba shabaha kuu ya msanii sio kuumba fani bora tu, bali kutumia fani kama chombo cha kumwezesha kuwasilisha wazo au hisia fulani kwa hadhira yake. Kwa hivyo, mtindo ndio humwezesha mtunzi kuwasilisha maudhui au ujumbe kwa wasomaji.

### 2.4.3 Mandhari

Mandhari ni yale mazingira ambayo hadithi imeandikiwa. Umuhimu wa kuchunguza mazingira katika uchanganuzi wa fasihi hutokana na utambuzi kuwa kila jambo hufanyika mahali maalum. Kila jambo hutendeka mahali fulani.Mandhari ni elementi muhimu katika kazi ya fasihi.Elementi hii huweza kukamilishana na elementi nyingine katika hadithi fupi. Mandhari yana umuhimu katika kazi ya fasihi.Kwa hivyo, ni vema yaelezwe kwa urefu kidogo. Kwa upande mwingine, mtindo hutumiwa kusawiri mandhari. Hatuwezi kupuuza mtindo tunapoelezea mandhari. Hii

ni kwa sababu mandhari huweza kuathiri jinsi mwandishi anavyoandika kwani huweza kuathiri hata uteuzi wa mtindo. Kwa sababu hii, mwandishi yeyote anapoyaeleza mandhari katika hadithi lazima atumie lugha yenye mnato ambayo ni mtindo.

### 2.4.4 Mtindo

Mwandishi anapoanza kuandika huwa na maswala anayowasilililisha kwa wasomaji. Maswala hayo hayawezi kuwafikia wasomaji au kuwa na athari alizonuia mwandshi pasipo kuwepo na njia ya kuyawasilisha. Mtindo unaakisi jinsi mwandishi anayehusika huyatazama maswala fulani. Ni njia ya kuwasilisha na kufumbata tajriba yake. Kuupanga na kuuwasilisha uelewa wake. Uchunguzi wa mtindo huhusisha mambo kama vile uteuzi wa msamitai, tamathali za usemi, ishara za uashiriaji pamoja na hata jinsi anavyoziakifisha sentesi zake.Ni kupitia mtindo ndipo mtunzi huweza kueleza dhamira yake,maudhui,wahusika na hata mandhari.Kwa hivyo, ni kijenzi muhimu sana katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

### 2.4.5 Wahusika

Wahusika ni viumbe vinavyotumiwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe wake.Wahusika hutumiwa katika fasihi ili kuwasilisha pia dhamira ya mwandishi.Maelezo yanayotolewa na wahusika husukwa na mtunzi kwa kutumia lugha yenye mvuto.Huu ni mtindo wa mwandishi.

Sifa muhimu inayotofautisha riwaya na hadithi fupi ni usawiri wa wahusika. Kwa upande mmoja, mwandishi wa riwaya huwakuza wahusika wake hatua kwa hatua na kuwapa kina cha saikolojia na falsafa. Kwa upande mwingine, mwandishi wa hadithi fupi huweza kuwapa wahusika wake mapana na marefu kama hayo. Hana nafasi wala muda wa kuwajenga wahusika kama wa riwaya. Anawaumba wahusika wake kwa maelezo mafupi lakini kwa ishara maalumu zinazowatambulisha na kwa vidokezo vyenye kuangaza upekee wao.

Mwandishi wa hadithi fupi huwatumia wahusika kuwasilisha ujumbe wake au dhamira,Kwa sababu hii, maelezo yanayotolewa na wahusika hukuzwa na mtunzi kwa kutumia lugha yenye mvuto.Huu huwa ni mtindo wa mwandishi ambao huwezesha wahusika kupitisha ujumbe wa mtunzi kwa njia yenye mnato. Hali hii huweza kuwavutia wasomaji kusoma hadithi kwa kasi.

Mbatiah (2002:xviii) aeleza kwamba mhusika wa hadithi fupi anastahili kuwa thabiti kitabia na asibadilike.Pia, matendo yake yawe wazi na ya kuaminika.Istoshe, lugha wanayoitumia ishahibiane na ya jamii husika.Bila shaka jukumu la kila mhusika liweze kubainika na wahusika wawe wa kusadikika katika tabia na matendo yao.

### 2.4.6 Muundo wa hadithi fupi

Kwa mujibu wa Walibora na Mohammed (2007) Muundo ni ile namna ambayo sehemu mbalimbali za hadithi fupi hupangika ili kuileta sura au picha ambayo tunaipata kutokana na usomaji wa hadithi ile. Katika hadithi fupi, elementi kuu ya muundo ni ploti au msuko ambao ni mpangilio wa matukio pamoja na ubainishaji wa

vyanzo vyao. Hivi ni kusema kwamba, egemeo la ploti ni matendo ya wahusika. Wataalamu wa hadithi fupi wanakubaliana kwamba hadithi fupi hujitokeza kama tungo lenye ploti au msuko wenye mwanzo, kati na mwisho.

Wamitila (2002:69) asema kuwa, mianzo ya hadithi fupi huwa na jukumu kubwa katika muundo wa hadithi nzima. Ni katika sehemu hii ambapo mwelekeo wa hadithi unatokea. Mgogoro uliopo katika hadithi unaanza kujitokeza kwenye sehemu hii.Mwandishi huingiza msomaji katika mgogoro unaomhusu mhusika nguli wa hadithi katika sehemu hii ya mwanzo, pia mandhari ya hadithi, mada na dhamira huelezwa. Wahusika wa hadithi fupi wanatangulizwa kwenye sehemu hii pia. Hii ndiyo sehemu ambayo hudokeza ujumbe wa mwandishi. Kwa ufupi, msomaji huweza kuelewa kile mtunzi anakiizungumzia katika hadithi.Kwa hivyo, hii ndiyo sehemu ambayo huweka msingi wa hadithi nzima.

Sehemu ya kwanza ya hadithi inapaswa kuwa mbegu ya hadithi nzima. Sehemu hii inapaswa kumvutia na kumteka msomaji. Huu ndio msingi wa kauli inayotolewa na wahakiki kuwa mwandishi wa hadithi fupi anapaswa kuwa mjuzi wa mbinu ya muziki inayoitwa ‘shambulio.’ Hii ni kwa sababu muziki unavyoanza huathiri wasikilizaji kwa kiasi kikubwa. Katika uchunguzi wake wa hadithi fupi za kiingereza, Bonheim anatambua aina mbalimbali za mianzo. Kuna mianzo ya maoni ya maelezo ya taarifa na maongezi au mazungmzo. Sifa hizi, zipo pia katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Ni katika muktadha huu ambao mwandishi wa hadithi fupi huhitaji kutumia mtindo unaovutia wasomaji ili mara ya kwanza tu wasomapo hadithi fupi waweze kubebwa kuanzia mwanzo hadi mwishoni mwa hadithi.

Shemu ya kati ndipo utata hujitokeza kama mgogoro au mvutano kati ya fikira au msimamo tofauti kati ya wahusika au au hata sehemu kuu. Ndipo Mohamed (1995:36) akasema kuwa:

> “kazi muhimu ya mhakiki katika hadithi ni ile ya kutambua migogoro.Migogoro katika kazi ya fasihi ni jambo lisiloepukika. Hii hujenga mvutano baina ya wahusika na hatimaye kujenga maudhui kutokana na matakwa ya mwandishi.”

Mohamed ameeleza aina tatu ya migogoro ambayo ni: kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Mgorogo wa nne anasema ni wa kinafsi. Huu ni mgogoro tanzu wa migogoro mitatu ya awali.

Kwa hivyo, katika sehemu hii ya kati, hapa ndipo dhamira ya hadithi inapopaswa kuendelezwa kwa upana ili hadithi iweze kuwa wazi na kufahamika. Isibanwe sana kiwango cha kugeuza maana ya hapo awali na iwe kazi kamilifu yenye kumvutia msomaji. Inapaswa kuzingatia suala la umoja na umoja dhabiti. Mwanishi hana wakati kuangazia maelezo yasiyo na mchango katika athari ya umoja wa hadithi yake agandamize maana ya hadithi katika kila sentensi inayotumiwa.

Wasomaji wasome si tu katikatika ya mistari, bali katikakati ya maneno yenyewe. Kwa vile mwandishi wa hadithi fupi ana nafasi ndogo, anapaswa kutumia mbinu ya uelekezi kwa ufundi mkubwa. Aseme mengi kwa maneno machache ili aweza kukuza mgogoro kwa njia inayomvutia msomaji.Mwandishi wa hadithi fupi katika sehemu hii anapaswa kuteua maneno yanayovutia ili kuuelezea mgogoro huu unaotokea katika sehemu hii ya kati. Njia hii anayoitumia kuwasilisha mawazo yake kuhusu mgogoro, yatawavutia wasomaji.Hii itaweka dhamira na maudhui ya mwandishi wazi kabisa na yataeleweka kwa urahisi.

Sehemu ya mwisho hufikiwa ule mgogoro unapopata suluhisho. Mwandishi hudhihirisha waziwazi funzo lake katika hadithi hiyo. Katika sehemu hii, mwandishi aisuke na kuiandika hadithi yake kwa jinsi inayomfanya msomaji atake kufikiria mwisho wake. Hadithi isukwe kwa namna ambayo inapofikia mwisho, msomaji aachwe na athari kubwa. Jambo hili limeungwa mkono na Mohamed anayesema kuwa hapa ndipo hadhira hupata jibu muhimu la kazi ya fasihi ambalo huwa limecheleweshwa kutokana na mbinu rejeshi au taharuki. Pia, anasema kuwa sehemu hii husisismua sana. Waandishi huweka kilele mwishoni mwa hadithi. Wakati nwingine si lazima pawe na kilele kimoja kwani kunaweza kuwa na vilele vingi au kusiwe na kilele katika kazi ya fasihi hiyo.

Anaendelea kusema kwamba katika kazi ya Fasihi hasa sehemu ya mwisho, suluhisho hupatikana pale ambapo suluhisho hutokea. Kilele cha juu nacho kilele cha chini anasema ni pale ambapo matazamio ya hadhira hukidhiri. Kile cha chini anasema kwamba huwa ni udhaifu wa kazi za sanaa lakini katika kazi nyingine, kilele cha chini hukusudiwa na msanii. Hali hii anasema, hutokea katika hadithi fupi.


Hata hivyo, mwandishi mzuri wa hadithi fupi anapaswa kuujua mwisho wa hadithi yake tokea mwanzo kabisa.Kwa hivyo, kuanza kutayarisha hatua kwa hatua tokea mwanzo bila ya kumpa fununu jinsi itakavyokuwa. Sehemu hii ya mwisho ndipo panapopatikana ufundi mkubwa.

Istoshe, Wamitila (2002:67) asema kuwa sehemu hii ya mwisho ya hadithi fupi huweza ikahusisha utatuzi wa tatizo au kumalizia hadithi kwa njia ya kawaida. Pia, hadithi inaweza kutamatishwa kwa kuifanya kupingana na mawazo ya mwanzo au

mwandishi anaweza kudhihirisha funzo katika sehemu hii. Anaweza vile vile kuonyesha muhtasari wa mada ama atumie mbinu za kijanja kama ilivyotumika na mwandishi wa Kimarekani wa hadithi fupi anayejulikana kama O. Henry. Hata hivyo, waandishi wengi wa hadithi fupi huimalizia sehemu hii kwa kutatua au kutoa suluhisho la mgogoro uliojengwa hapo awali.

MCOnyango (2007) akieleza muundo wa hadithi fupi asema kuwa sehemu ya mwanzo wa msuko wa hadithi hujihusisha zaidi na kuelezea mkondo wa mgororo. Sehemu hii ya masimulizi hunawirisha kazi na kupandisha kiwango cha matarajio ya msomaji mpaka kwenye upeo wa hadithi.Katika sehemu ya upeo, vitendo hupungua pale ambapo mwandishi huelezea suluhisho la mgogoro, kisha hadithi hufikia kikomo. Msuko wa hadithi fupi hujitokeza kama msuko sahili ambapo mtiririko wa vituko hufululizwa moja kwa moja toka mwanzo hadi mwisho. Hivyo ni muhimu kubainisha mtindo ambao mtunzi ameutumia katika kujenga kazi yake yote ya fasihi.

Mohamed (1997:34) anasema kwamba muundo huu ni wa moja kwa moja na hujumuisha maelezo rahisi kwa kukua hadi mwisho. Kimsingi, anauita muundo huu, muundo wa kiutelezi na wengine huuita muundo wa msago jinsi vile umeonyeshwa pale chini kwenye mchoro husika.



Wakati mwingine, hadithi inaweza kufuata muundo usio wa kawaida. Matukio yanayosimuliwa huenda mbele na nyuma. Muundo huu, huitwa wa kioo. Hutokea pia muundo wa hadithi nyingine kuanza kwa maelezo yanayomalizia hadithi. Muundo huu hauna istilahi maalumu, lakini tunapoeleza tunasema ni muundo mwisho – mwanzo. Msuko unapokuwa tata au wa kioo mtiririko wa vituko huwa si wa moja kwa moja.

Hata hivyo, muundo wa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili huwa ni muundo sahili.Yaani,mwanzo,kati na mwisho.Mwandishi wa hadithii fupi hueleza mawazo yake moja kwa moja. Matukio hayatupwi hapa na pale. Hii ni kwa sababu hadithi fupi ni masimulizi ambayo ni mafupi,kwa hivyo mwandishi hana wakati mrefu kurusha vitukio hapa na pale. Anastahili kuyaeleza moja kwa moja.

## 2.5 Hitimisho

Katika sura hii, tumeonyesha fasili, historia na maendeleo ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili hadi sasa. Vile vile, tumeweza kueleza sifa kuu za hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili na vijenzi muhimu vya hadithi fupi. Katika maelezo tuliyoyatoa, imedhihirika kuwa ingawa utanzu wa hadithi fupi hauna historia ndefu, uchapishaji wa hadithi fupi hizi umechipuza kuwepo kwa waandishi wengi wa hadithi fupi ambao wameweza kuangazia maswala aidha ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na hata kiteknolojia. Hali hii imepelekea utanzu huu kuendelea kukua kwa kasi sana.

Aidha, imedhihirika wazi kwamba ijapokuwa kuna utata miongoni mwa waandishi wa hadithi fupi kutoa fasili mwafaka kuhusu utanzu huu, tumeweza kubainisha fasili

za utanzu huu za waandishi mbalimbali ambazo zitaweza kusaidia kueleweka kwa utanzu huu. Pia, kwa kuelezea sifa za utanzu huu na vijenzi vyake hasa jinsi vile vinavyouwiana na dhana ya mtindo, itasaidia utanzu huu kufahamika zaidi.

# SURA YA TATU

# MATUMIZI YA TASWIRA NA ATHARI ZINAZOTOKANA NA MATUMIZI HAYO KATIKA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI.

## 3.0 UTANGULIZI

Sura hii ilishughulikia matumizi ya taswira na matarajio ya athari zinazotokana na matumizi hayo katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Matumizi haya ya taswira yametumiwa kusawiri ujumbe wa mwandishi katika machapisho ya *Pendo la Heba (1996)* na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine [2004]*. Mihimili iliyotuongoza katika sura hii ni ule unaosisitiza umuhimu wa lugha kama chombo tekelezi kinachosaidia kueleza ujumbe uliokusudiwa. Muhimili huu ulitusaidia kuangalia namna watunzi walivyotumia taswira katika utunzi wao.

Aidha muhimili wa pili uonatilia maanani kiwango cha msamiati, ambapo mtafiti hujishughulisha na uteuzi wa mbinu kama vile jazanda, tashbihi, na istiari ulitumiwa pia. Muhimili huu ulituwezesha kutathmini matarajio ya athari zinazotokana na matumizi ya taswira katika utunzi.Nao muhimili wa tatu unaomhitaji mtunzi wa fasihi kuonyesha umaarufu katika matumizi ya lugha ya kuvutia, ulituauni kukadiria athari za kutumia tamathali teule.

### 3.1 Taswira

Taswira humsaidia mtunzi kufafanua matukio kwa kiwango kikubwa.Hata hivyo, katika fasihi dhima kuu ya taswira ni kutoa maelezo na muhala ya picha zinazotukia

akilini mwa wasomaji.Pia, humsaidia msomaji kukumbuka sifa na matukio katika kazi za fasihi. Vile vile, huifanya kazi ya fasihi kuvutia inaposomwa.

Kwa mujibu wa Msokile (1993:45) taswira ni jumla ya mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya msanii katika kazi ya fasihi. Taswira hizi zaweza kuundwa na kirai au neno. Kwa maoni yetu, taswira ni yale maelezo ya mwandishi yanayojenga picha akilini mwa msomaji anaposoma kazi yoyote ile ya fasihi. Picha hizi mara nyingi hupitisha ujumbe wa mwandishi kwa hadhira yake.

## 3.2 Matumizi ya Taswira

### 3.2.1 Pendo la Heba

Katika diwani hii mwandishi ameweza kutumia taswira katika hadithi fupi mbalimbali. Kwa mfano, katika hadithi fupi ya *"Pendo la Heba"*kuna maelezo yanayomhusu Musa na sebule ya nyumba yake ambayo yanazua picha ya akilini.Tunaarifiwa kwamba Musa alikuwa ameketi kwenye kochi la sifongo sebuleni.(u.k 1). Musa alivalia shati la mkunguru, suruali nyeusi na viatu ni makubadhi. Mkononi alifunga saa ambayo ukanda wake ulisaki katika mkono ulionona. Sebuleni mlikuwa na runinga ya rangi, meza ndefu kwa ndogo na saa nne zilizotundikwa katika kila kiambaza. Pia kulikuwepo makombe ya mashindano, picha za watoto wao na picha ya harusi ya Lea na Bw. Musa.

Bila shaka, maelezo haya yanayochora picha ya chumbani mwa Musa yanadhihirisha wazi kuwepo kwa matabaka katika jamii. Picha hii inawasilisha

ujumbe kwamba familia ya bwana Musa ni ya watu ambao wamo katika tabaka la kati kiuchumi.Familia hii ilikuwa na uwezo wa kukimu mahitaji yake ya kila siku.Iliweza kujikimu kichakula,kiafya,kimavazi, kimakazi na hata kielimu.

Musa kuwa na saa mkononi na nyingine nne chumbani mwake inathibitisha maudhui ya utaratibu maalum wa kufanya mambo na ratiba zilizofuatwa ipasavyo.Wakati haukutumiwa ovyo,kazi zilifanywa kulingana na wakati wake.Saa yenye umbo la bara la Afrika inawasilisha maudhui ya uzalendo. Inabainisha kuwa familia hii iliienzi nchi yake na kuionea fahari na kuthamini uafrika wao.

Familia hii ilithamini sana elimu. Jambo hili limeonyeshwa na yale makombe ya mashindano yaliyokuwepo katika nyumba hii.Walishiriki katika mashindano mbalimbali yaliyowaletea ushindi na mafanikio makubwa. Bwana Musa alisoma na kuwa daktari mwenye umahiri mkubwa.Naye mkewe Lea alikuwa msaidizi wa waziri. Hali hii inaashiria suala la bidii maishani.Bidii hii ndiyo iliyowawezesha kuishi maisha mazuri waliyokuwa nayo kwani hawakuwa fukara.

Mwaandishi anapochora picha hii, anatarajia msomaji kutambua umuhimu wa bidii maishani.Bidii huwezesha waja kuwa katika kiwango fulani cha maisha kinachoiwezesha familia kujikimu vilivyo.Vile vile, anabainisha hali ya kuwa na mwongozo katika utendaji kazi. Anatarajia kuonyesha umuhimu wa kuutumia muda kwa uangalifu.Aidha, inamhitaji msomaji kuelewa umuhimu wa kuthamini nchi yake na uraia halisi.

Pia, kuna picha ya jiji la Tokyo.Picha hii inaonyesha barabara za mji huu zilivyojengwa kiustadi, mji huu ulikuwa na nyumba za ghorofa nyingi ajabu,

madaraja ya kupendeza na magari makubwa. Taswira hii inaonyesha nchi ya Japan ambayo imeendelea sana hasa inapolinganishwa na nchi za Afrika ambazo hazijaaendelea kiuchumi na kiteknolojia.Lea na waziri wake wanapozuru nchi hii wanatambua mazingira yake ya kupendeza hasa walipolinganisha nchi ya Kenya walikotoka ambayo ilikuwa nyuma kimaendeleo.

Taswira hii imechorwa na mwandishi kuonyesha maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Inadhihirisha kuwa jamii ya watu wa Tokyo ilikuwa imeendelea sana, ikilinganishwa na watu wa jamii ya akina Lea. Lea alipokuwa katika mji huu aliona barabara zilizotengenezwa vizuri,magari makubwa na marefu. Hoteli walizozuru kujivinjari usiku na waziri wake zilivutia sana. Hali hii inathibitisha wazi kuwa nchi hizi za ng'ambo zilikuwa zimeendelea sana zikilinganishwa na zile za kiafrika.

Vile vile, picha hii ya mji wa Tokyo inadhihirisha maudhui ya usaliti. Maudhui haya yameonyeshwa kupitia mhusika Lea mkewe Musa. Anapopata fursa ya kutembelea jiji la Tokyo na mkubwa wake waziri, anashiriki mapenzi na mkubwa wake.kwa hivyo, anamsaliti mumewe Musa japo familia yao ilikuwa thabit,i yenye upendo na ushirikiano.

Mwandishi ametuchorea picha hii akitaka kubainisha suala la uwajibikaji wa nchi za ng'ambo ambao umewasaidia kupiga hatua maishani.Istoshe, analenga kuonyesha hali halisi ya maisha katika ndoa.Anadhihirisha vizingiti vinavyokumba ndoa nyingi na vinavyoweza kusababisha talaka au utengano katika ndoa.

Aidha, katika hadithi fupi ya *"Jitu la Kisasa"* kuna picha akilini inayojichora kuhusu mtoto wa Lomo alivyoaga dunia.Madaktari waliojaribu kuokoa maisha ya mtoto huyo

hawakufua dafu.Mwishowe, mtoto huyo alikata kamba akiwa hospitalini alikokuwa amelazwa kwa matibabu.Muda mfupi baadaye, waombolezaji walianza kujumuika nyumbani mwa Mzee Lomo ili kuandaa mazishi.Taswira hii inaeleza na kuwasilisha ujumbe wa huzuni.Kifo kinapotokea husababisha pengo kubwa katika jamii hasa familia iliyofiwa.Wakati mwingine, waja hukata tamaa maishani hasa aliyeaga anapokuwa uti wa mgongo katika familia hiyo.

Pia, kuna picha ya waombolezaji waliokuwa nyumbani mwa Mzee Lomo kwa maombolezi huko shambani katika kijiji cha Lambeka. Wazee kwa wavulana walikaa mahali pao ambapo walikuwa wamewasha moto mkubwa wa kuota pale uani.Akina mama pia walipewa nyumba moja kubwa ya kuwapa usalama na hifadhi. (u.k 41). Katika nyumba hii ya wanawake, ndipo mke mmoja aliyekuwa amefunga tu pingu za maisha hivi karibuni alinyemelewa na kubakwa na mwanamume mmoja.Taswira hii inawasilisha maudhui kadhaa.Inasisitiza suala la ushirikiano kunapotokea msiba kama huu wa matanga.Wanakijiji hujumuika pamoja kuisaidia familia iliyofiwa kwa hali na mali ili kutayarisha mazishi.Kwa hivyo, tunapata kufahamu kuwa kulikuwa na utangamano mzuri wa wanajamii wakawa wanasaidiana wakati wa majanga kama vile mauti.

Picha hii pia, inaonyesha maovu yaliyosakini katika jamii yetu ya leo. Uovu unaosisitizwa hapa ni ubakaji. Wabakaji hawa walikuwa waovu kama majitu ya zamani. Ubakaji unapotekelezwa mara nyingi wahusika hukisia kuambukizwa na magonjwa kama vile ya zinaa au ukimwi jinsi vile ilivyodhamiriwa kwa mke huyu aliyebakwa. Anapelekwa hospitalini kupimwa ili kufanyiwa uchunguzi zaidi kama ameambukizwa magonjwa mabaya.

Picha hii pia imetumiwa kuonyesha maudhui ya taasubi ya kiume katika jamii hii husika.Tunafahamishwa kuwa wakati wa msiba kama huu wa matanga, wavulana walijumuika pamoja na wazee wakati wa usiku kuota moto. Hawa usalama wao haukutiliwa maanani sana jinsi vile wa wanawake ulivyothibitiwa.Wanawake nao walitengewa sehemu yao ya kujisetiri usiku wakati huo wa matanga ili kupumzika.Hata hivyo, pale kulipokuwa na upungufu iliwalazimu kulala nje. Vyumba hivi vililinda usalama wao. Hivyo walionwa kama viumbe hafifu vilivyohitaji kupewa ulinzi mkali.Hali hii inadhihirika pale ambapo mwanamume wa mke aliyebakwa anapothibitisha kitendo hiki kimetibuka na kutekelezwa ambapo anamvamia mbakaji na kumpiga vibaya sana.Hii inaonyesha kwamba jinsia ya kike ililindwa dhidi ya uhasama wowote ule.Hata sasa wanawake bado wanachukuliwa kama viumbe dhaifu na wanaotegemea wanaume.

Picha ya wanawake kutengewa nyumba ya kulala na wanaume kuwasha moto nje uani wa kuota usiku wanapokesha ni dhihirisho tosha kwamba kulikuwa na uhaba wa vyumba vya kulala ambavyo vingewatosha watu wote. Hii inaonyesha kwamba watu wa kijiji hiki walikuwa wa tabaka la chini. Walikuwa maskini na wasingeweza kumudu kuwa na vyumba vinavyotosha umati mkubwa wa waombolezaji.

Mwaandishi ametumia taswira hizi akimtaka msomaji kutambua ukosefu wa maadili na baadhi ya wahusika katika jamii inavyoweza kusababisha maafa na hata fujo miongoni mwa jamii husika.Istoshe, anamtarajia msomaji kutambua umuhimu wa umoja na ushirika katika jamii panapotokea msiba.Vile vile, anamtarajia msomaji kung'amua usawa wa kijinsia katika jamii.Wanawake wasichukuliwe kama viumbe dhaifu visivyo na uwezo kama wanaume.Hata hivyo, mwandishi anamtarajia

msomaji kutambua umuhimu wa kuwa na ujira unaotosha ili kuweza kukimu mahitaji ya kimsingi.

Pia, mwandishi wa hadithi fupi ya *“Jahanamu”* yake Mwenda Mbatiah, kuna taswira ya jiji la Nairobi Mtaa wa Mathare alikoishi Mganga pamoja na aila yake.Mwandishi ameanza kwa kuelezea taswira ya jua lililomulika dunia kama jikarabai siku hiyo ya jumapili.Tunaelezwa kwamba uvuguvugu wa mmuliko huu ulistarehesha miili ya wapenda kuota jua la asubuhi.(u.k 44).Taswira hii inawasilisha maudhui ya wakati.Wakati huu wa asubuhi ndio uliotumiwa na wakristo kujitayarisha kwenda maabadini kusali na kumwabudu Mola.

Vile vile, mtunzi anatuchorea picha ya nyumbani kwa akina Mganga.Mganga na aila yake waliishi katika kibanda kilichotengenezwa kwa vipande vya mabati, makaratasi magumu na udongo. Kibanda hiki kilivuja hasa majira ya mvua kama kwamba kilikuwa kimeezekwa kwa chungi.(u.k 46 ). Pia, kuna picha ya eneo zima la Mathare ambalo tunaelezwa lilikuwa limejaa vibanda vibovu vilivyojaa mavi ya watoto, mbwa na mbuzi, mkojo wa walevi, uozo wa makombo ya mboga viazi na ndizi na maji ambamo mbuzi waliogea hata bata.Uchafu huu wa kila aina ulitoa uvundo uliohujumu pua kama dharuba kali ya mishale elfu inayochoma kwa pamoja. Taswira hii imeendelezwa na pale moto ulipozuka na kuteketeza vibanda vyote isipokuwa kile cha kina Mganga pekee na wakazi wakashindwa kuuzima (uk47).

Mwandishi anatuchorea picha hizi kuashiria maudhui ya umaskini.Kina Mganga waliishi maisha ya kimaskini.Eneo zima kuwa na vibanda vibovu inaonyesha jinsi ambavyo watu walivyoishi katika mazingira magumu wakawa hawana uwezo

kutokana na unyonge waliokuwa nao wa kiuchumi.Wakazi hawa walioishi katika mtaa huu wa Mathare katika mabanda walikuwa na pato la chini katika jamii. Hapa ndipo familia ya Mganga iliishi maisha duni ya ulitima uliokithiri. Eneo zima lilijaa uchafu wa kila anuai:mavi ya watoto,mbwa na mbwa, mkojo wa watu, uozo wa makombo ya mboga,viazi na ndizi, maji meusi walimoogea bata. Uchafu huu ulitoa uvundo uliohujumu pua za watu.Umaskini huu usingewawezesha wakazi hawa kujenga nyumba nzuri na kuishi katika mazingira nadhifu.

Katika hadithi hii, pia kuna taswira tunayochorewa ya mtaa wa Eastleigh. Mahali hapa kulikuwa na jengo kubwa la kanisa la dhehebu la Katoliki. Familia ya akina Mganga walikwenda kumwabudu maulana kila siku ya jumapili kanisani humu.Picha hii inawasilisha maudhui ya dini.Mamake Mganga, Mganga na Siti walikuwa wakristu kwelikweli. Hata hivyo, Mganga hakuwa na imani hii, alilazimika kushiriki katika ibada ilimradi asimuudhi mamake.

Picha nyingine inayojichora akilini katika hadithi hii, inatokea pale Mganga anafukuzwa na mwendawazimu aliyeshika jiti kubwa. Mganga aliamua kukimbia akiogopa mwendawazimu asimpige kwa lile jiti. Nao askari kanzu walimshuku kuwa mhalifu. Papo hapo, akamiminiwa risasi mbili zilizopasua kichwa chake na kuumwaga ubongo wake mweupe kwenye lami nyeusi .Tukio hili lilitokea katikati mwa jiji la Nairobi kulikokuwa na makundi mengi ya watu kama vile: askari kanzu, wendawazimu, washukiwa wa ujambazi na hata barabara nyeusi za lami.Mwishowe,askari wanapofika muda mfupi baadaye na kuchunguza kitambulisho chake Mganga kikatambulisha kuwa si jambazi bali ni mwanagenzi wa chuo kikuu cha Nairobi (uk 50).

Taswira hii inadhihirisha maudhui ya ukosefu wa usalama katika jiji la Nairobi.Inakisiwa kuwepo kwa majambazi katika mji huu wanaotekeleza uhalifu na kuibia watu. Hii ndio sababu askari wanapomwona Mganga anakimbia wanamshuku kama mwizi na kumpiga risasi iliyomwua. Hata hivyo, askari hawa si waangalifu.Wanafyatua risasi ovyo bila hata kujua kama mhusika ni mhalifu au la. Hii inatokana na serikali iliyokuwa imeelekeza maafisa wa usalama kumpiga risasi na kumwua yeyote anayeshukiwa kuwa mhalifu.Kauli hii nayo inatudokezea kuhusu uongozi mbaya pamoja na sheria potovu za serikali zisizowalinda raia. Hii ni kwa sababu baadaye askari wanakuja kubaini kuwa aliyeuawa hakuwa jambazi bali ni mwanafunzi wa chuo kikuu cha Nairobi.

Katika hadithi hii, pia mna picha inayojichora akilini mwetu ya taasisi za kielimu. Mwandishi ametuchorea chuo kikuu cha Nairobi alikokuwa akisoma Mganga (u k 48). Picha hii ya chuo kikuu na shule alikosoma Siti dadake Mganga, inatudokezea kuhusu maudhui ya elimu. picha hii ni dhihirisho tosha kwamba watoto wa jinsia zote walielimishwa bila kubagua jinsia yoyote katika jamii hii inayosawiriwa na mwandishi.Wazazi wa akina Mganga ingawa walikuwa na uwezo duni wa kifedha, walijimudu kuwaelimisha wana wao hadi chuo kikuu.Kwa hivyo, jamii hii ilithamini sana elimu.

Mganga anatia bidii masomoni ili aje baadaye aisaidie aila yake iliyokuwa katika lindi la mateso.Hii ndiyo sababu anapotoka hospitalini kumtazama mamake aliyekuwa katika hali mahututi, anawaza kuwa huenda mamake akakata kamba na tayari dadake Siti alikuwa ameangamizwa na ugonjwa wa kipindupindu. Hivyo anawaza atakapohitimu atafaa nani baadaye ilhali hawapo. Hii inaonyesha kwamba

jamii hii ilielimisha wana wao wakiwa na matumaini ya wao kuajiriwa ili kuwafaa baadaye.

Ipo taswira ya hospitali alikolazwa mamake Mganga. Hii ni hospitali ya Kenyatta (uk 49). Picha hii ya hospitali imetumiwa kuwasilisha maudhui ya mkurupuko wa maradhi katika mitaa ya Mathare hasa mabandani kwa ajili ya uchafu uliokuwa umeenea na kutapakaa kila mahali. Inaashiria pia huduma za kimatibabu. Sekta hizi ziliwashughulikia wagonjwa kwa kuwatibu wagonjwa wenye maradhi tofauti tofauti.

Mwandishi wa hadithi hii ya *Jahanamu* anatuchorea picha hizi akitarajia msomaji kutambua umuhimu wa kuwa na mapato ya kuweza kukimu mahitaji yetu ya kimsingi. Ukosefu wa mapato husababisha waja kuishi katika makazi mabovu na hata mazingira machafu. Uchafu huu, wa kimazingira husababisha maradhi yanayoenea kwa kasi sana na kuua idadi kubwa ya watu.vile vile, anamtarajia msomaji kuelewa umuhimu wa kwenda kanisani ili kujifariji hasa unapokumbwa na matatizo chungu nzima. Isitoshe, mtunzi anatarajia kuonyesha hofu inayoweza kukithiri miongoni mwa watu hasa hali ya usalama inapodorora nchini.Wananchi na walindausalama huishi maisha ya hofu na kutoaminiana.

Katika hadithi fupi ya *"Mtembo"* mtunzi Rayya Timammy, anatuchorea picha ya Fadhila alipomsukuma mamake kisimani. Fadhila alihusudi vyungu vilivyokuwa vinatengenezwa na MwanaMize Matongo, kiasi cha kuweza kukubali kumsukuma mamake kisimani afe ili MwanaMize Matongo akiolewa na babake aweze kumtengenezea vyungu. Anapomsukuma mamake, anamezwa na ng'ombe aliyekuwa na nyumba mle ndani.Babake anamwoa MwanaMize kumfurahisha Fadhila.Baadaye,

Fadhila anateswa na kutopata kile alichotarajia (uk 27). Taswira hii, mwandishi anawasilisha maudhui ya wivu, malezi na migogoro katika jamii. Malezi haya mabaya yanasababisha mgogoro katika familia hii. Fadhila aliteswa na mama wa kambo. Hapo ndipo akawa anakwenda kisimani kuimba, ng'ombe anafungua kinywa, Fadhila anatumbukia mle ndani. Anakutana na mamake anayemwonyesha mapenzi ya dhati.Anamlisha chakula kizuri na kumvisha mavazi mazuri.

Taswira nyingine ni ya kisimani. Hapa ndipo Fadhila alimsukuma mamake akatumbukia ndani na kufa.Pale kisimani ndipo palipokuwa na ng'ombe.Ng'ombe huyu ndiye aliyemeza mamake Fadhila. Mwandishi anaeleza kuwa ndani ya ng'ombe huyu mlikuwa na nyumba alimoishi mamake Fadhila.Humo ndimo Fadhila alikuwa akiingia na kukutana na mamake. Baadaye ng'ombe huyu aliuawa na mifupa yake ikatupwa hapo kisimani palipotokea mtembo (uk28). Kisima huwa na maji na maji ni uhai.Kwa hivyo mwandishi anapotuchorea taswira hii inawasilisha maudhui ya mafanikio. Fadhila alipitia mateso chungu nzima alipolelewa na mamake wa kambo MwanaMize matongo. Mwishowe, Fadhila aliweza kufanikiwa, hasa alipoolewa na mwana wa kifalme na maisha yake yakanawiri.

Kuna taswira ya makazi ya kifalme. Mwanawe mfalme alikuwa mwenye mali nyingi (uk30). Picha hii inaonyesha matabaka katika jamii.Mwana huyu wa mfalme alikuwa wa tabaka la juu. Kwa hivyo, hili ni dhihirisho tosha kuwa uongozi huandamana na watu wa tabaka la juu.

Mwandishi anapotuchorea picha ya Fadhila kumsukuma mamake kisimani ili MwanaMize amtengenezee vyungu na vile vile kuolewa na babake, anamtarajia

msomaji kubaini umuhimu wa kuthamini wazazi wetu waliotuzaa na kutupa malezi yaliyo bora.Vile vile, mwandishi anatarajia msomaji kutambua umuhimu wa kuwa na utu maishani.

Picha ya makazi ya kifalme na inayoambatana na uongozi inapochorwa, mtunzi anatarajia kuonyesha migawanyiko katika jamii inayotenga watu na kuwaweka katika viwango tofauti tofauti vya maisha kulingana na mapato yao.

Katika hadithi fupi ya *"Genge,"* kuna picha ya sehemu ya jangwani. Mwandishi anatuelezea ujia ambao Maria anapitia asubuhi na mapema. Mwandishi anasema alipitia katika kijia kilichokuwa na majani ya kila aina,miguu na viatu vyake vikalowa chepechepe. Huu ni wakati ambao alikuwa anaenda kumwona mbunge wake mheshimiwa Mlaji amsaidie kupata kazi(uk51). Taswira hii inaashiria unyonge aliokuwa nao Maria. Unyonge huu ulisababishwa na umaskini wa nyumbani kwao. Pia picha hii inaonyesha utengano uliokuwapo kati ya raia maskini na matajiri. Utengano huu ulisababishwa na kuwepo kwa tabaka la juu la matajiri na lile la chini la maskini.

Kuna taswira ya jumba kubwa la mheshimiwa Mlaji lililolindwa na majibwa makali.Mtunzi anasema kuwa ndani ya jumba hili mlikuwa na makochi makubwa yenye foronya ya kina kirefu. Ukutani, mlikuwa na mapambo ya kila anuai.pia kulikuwa na vyombo chungu nzima: matelevisheni, vinanda, video, tarakilishi, meza, viti, saa kubwa ya dhahabu, shehena ya vyombo vya kaure, fedha na shaba na zulia lenye rangi ya kila aina(uk 52).

Taswira hii inadhihirisha jinsi viongozi walivyojipatia mali nyingi kwa njia ya ufisadi. Utawala wao ulikuwa mbaya na uliwagawanya wanajamii katika matabaka makuu mawili. Tabaka la mabwenyenye na lile la walalahoi. Kina mheshimiwa Mlaji walitoka katika tabaka la juu na waliishi maeneo yaliyokuwa yameendelea. Ni dhahiri kuwa Maria alitoka katika tabaka la walalahoi.Aliishi katika eneo ambalo halikuwa na maendeleo hata kidogo.Barabara zilikuwa mbovu na hazikuwa na mwangaza.

Mwandishi pia anatuchorea taswira ya kilabu ya Peponi ilipopatikana hoteli walimokutana Maria na mheshimiwa Mlaji. Hoteli ya kilabu hiki ilikuwa inavutia na ilipatikana katika Mtaa wa Maisha. Kulikuwa na njia kuu ya kwenda katika mtaa huu iliyopita katika vitalu vya miembe na midimu.Mtaa huu ulikuwa na majumba makubwa ya kisasa ya mabwenyenye. Pia pale Peponi palikuwa na jengo la ghorofa.Chumba rasmi cha mwenye hoteli ambamo Maria alikuwa akutane na wafadhili wake. Chumba hiki kilikuwa katika ghorofa ya sita. Mlango wa chumba hiki ulikuwa unapendeza.Ulikuwa na kioo chenye mmeremeto wa rangi zilizotokana na mtambo wa tarakilishi.Pia, kulikuwa na simu kwenye mlango (uk55).

Taswira hii inaashiria utajiri. Kando na utajiri, mwandishi ametuchorea picha hii kuwakilisha maudhui ya usasa.Inaonyesha maisha mapya yenye usasa.Usasa huu umewezeshwa na maendeleo ya teknolojia ya kisasa. Hata hivyo, inabainika wazi kuwa teknolojia hii imewezeshwa na uwezo wa kiuchumi katika jamii. Ni bayana kuwa wanaotumia vifaa vya kisasa ni wale wenye uwezo mkubwa kiuchumi. Hawa ni kama vile Bwana Mkaange na Mheshimiwa Mlaji.

Taswira hizi zinazoashiria umaskini, matabaka na usasa katika jamiii, mtunzi anazitumia akitarajia kubainisha jinsi wanyonge hudhulumiwa na walivyo navyo.Mabwenyenye hutwaa mali inayowawezesha kuishi maisha mazuri huku wanyonge wakiangamia katika lindi la mashaka.

Nayo hadithi fupi ya *"Kisasi"* ina taswira kadha.katika hadithi hii, mna picha ya hospitali.Hapa ndipo anapopatikana Daktari Madevu.Hospitalini humu ndimo Njeri alimoenda kwa uchunguzi wa kimatibabu (uk 66). Picha hii inajenga maudhui ya huduma za kimatibabu zinazotoa tiba kwa watu wenye magonjwa na matatizo mbalimbali. Kabla ya matibabu daktari humwelezea mgonjwa magonjwa anayougua. Kuna magonjwa mengine kama ukimwi yaliyowatia hofu wanaougua na kuwatamausha.Wagonjwa wengi kama kina Njeri waliweza kuchanganyikiwa kiwango cha hata kutojitambua na hata kutotambua walikokuwa wakienda.

Pia katika hadithi hii, mna picha ya basi alilosafiria Njeri kutoka hospitalini (uk67). Picha hii inaonyesha matatizo yanayokumba sekta ya uchukuzi pamoja na wafanyakazi wake.Vile vile, inaashiria ukosefu wa maadili ya kikazi ya utingo wa basi.Anamwambia Njeri ampe nauli na aendelee kulia kama alikuja mahali hapo kulia

Kuna picha nyingine hadithini humu ya chuo kikuu walikosoma Njeri, Onyango na Nyaboke. Tunaelezwa kuhusu vyumba mbalimbali vya kulala vya wanafunzi hawa (uk68).Taswira hii inawakilisha maudhui ya elimu. Tunaweza pia kutambua zile changamoto zinazokumba sekta hii ya elimu. Baadhi ya changamoto hizi ni kama vile mapenzi ya kiholela shuleni yanayoweza kusababisha mimba za mapema shuleni hata maambukizi ya magonjwa mabaya kama vile ukimwi.

Fauka ya hayo, kuna picha nyingine ya kanisa. Hili ni kanisa ambalo Njeri alikuwa akishiriki ibada (uk71). Mwandishi anatuchorea picha hii kuwakilisha maudhui ya kidini.Inaashiria pia hali ya matumaini kwa wale waliotamauka. Njeri anapoelezwa na Daktari Madevu kuwa ameambukizwa ugonjwa wa ukimwi, anapoteza matumaini ya kuishi tena. Anaposhiriki ibada na kushauriwa na hata kupimwa, ikagunduliwa kuwa hana viini vya ugonjwa huu, anakuwa na matumaini ya kuishi tena.

Mwandishi anapochora picha hizi anatarajia kubainisha matatizo yanayokumba jamii ya sasa ambayo husababisha hofu na shaka miongoni mwa waja. Hali hii huibua migogoro wakati mwingine miongoni mwa wahusika.Anaonyesha pia nafasi ya dini katika maisha ya waja. Dini huumba viumbe upya na kuleta mabadiliko ya wahusika walioathirika pakubwa maishani, aidha kisaikolojia na hata kibinafsi.

### *3.2.2 Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*

Diwani humu pia mna matumizi ya taswira, hasa katika hadithi fupi ya "*Kachukua Hatua Nyingine"*. Kuna taswira ya mavazi ya watoto wa Mavitu. Mwandishi anaeleza kwamba nguo za watoto wa Mavitu zilikuwa zimepasuka na ilikuwa kazi ya mkewe Mavitu kuzirembesha na viraka vya kila aina, kiwango cha hata mwalimu kulalamika kuwa rangi asili ilisalia tu kwenye vipande vichache (uk46). Taswira hii imetumiwa na mtunzi kuwasilisha maudhui ya umaskini.Hali hii ya maisha ilisababisha familia ya Mavitu kufeli kukimu mahitaji yao ya kimsingi hasa: chakula, mavazi na elimu.

Mwandishi anatuchorea picha hii akitarajia kumulika umaskini katika uhalisia wake.Anaangazia suala hili akitarajia kuonyesha madhara yanayotokana na hali hii ya

maisha. Anabainisha jinsi vile hali kama hii inavyoweza kusababisha afya kudorora, watoto kudunishwa, na hata kukatiza masoma yao. Maamuzi mabaya maishani huweza pia kutokana na suala hili hasa kifo.

Mtunzi wa hadithi fupi ya *"Mayai Waziri wa Maradhi"* anatoa maelezo yanayochora picha akilini mwetu.Anatuelezea jinsi vile mamake Mayai alipokuwa akikinyonyesha kitoto kichanga kilichoshika ziwa lililonyauka, kikitazama kidevu cha mamake. Pia, ameelezea picha ya watoto wadogo waliokuwa wakikoga uchi mtoni kwa maji machafu. Padri anapotoa pipi mfukoni na kuwatupia, wanang'ang'ania (uk64). Kuna picha ya watoto tisa waliokondeana walioketi mezani ambapo mmoja amevaa nguo nzuri na wengine wamevaa mararuraru. Wanapopewa chakula, wanakila kwa pupa na kukimaliza chote (uk69).

Picha hizi zinawasilisha maudhui ya umaskini.Mtunzi anaonyesha kwamba idadi kubwa ya wananchi walikuwa maskini.Hawakuweza kukimu mahitaji ya familia zao hali iliyoathiri afya ya watoto.Wazaza pia hawamudu kuvisha wana wao mavazi mazuri kwa vile hawana uwezo wa kifedha.

Kwa kutumia taswira hizi,mwandishi anatarajia kuwazindua viongozi kuwajibikia majukumu yao kwa kutekeleza ahadi wanazowekea wananchi hasa ugavi wa malighafi kwa usawa. Pia, anataraji kuonyesha athari ya matabaka katika jamii, hasa yanavyoweza kuleta mgawanyiko katika jamii na kuhujumu wasio na uwezo.

Kuna taswira ya walimu na madaktari waliogoma na kuandamana.Mwaandishi anaeleza kwamba Mayai aliota akiona msafara mrefu wa watu wengi waliokuwa wakiandamana kuelekea nyumbani kwake. Mara akapata simu kumjuza kuwa

kulikuwa na mgomo wa walimu na madaktari (uk73).Taswira hii inawasilisha maudhui ya matatizo yanayokumba sekta ya elimu na matibabu.Kuna malipo duni kwa walimu na madaktari.Wasimamizi wa sekta hizi akina Mayai wameshindwa kutoa usimamizi unaofaa.Wanasifu madaktari wanaoua na magonjwa yanayofisha.

Mwandishi anatumia picha hii kuwazindua viongozi kubadili mienendo yao mibaya na kuwajibikia majukumu wanayostahili kutekeleza. Anatarajia kuwazindua viongozi kuhakikisha kwamba sekta husika zinatoa huduma bora kwa wananchi.

Vile vile, hadithnii humu mna picha ya Mayai pamoja na wabunge wenzake wakijiburudisha katika baa. Picha hii inaonyesha Mayai na wabunge wakiwa ndani ya baa wakinywa pombe. Chupa zilikuwa zimejaa mezani na kesi nyingine nyingi zilikuwa zimepangwa pembeni zikiwasubiri.Nyama za kuku na mbuzi zilikuwa nyingi.Vile vile, yeye na wenzake wanakojoa mtoni na chini bondeni kuna wakulima waliokuwa wameweka majembe yao pembeni mwa mto wakikoga na kusugua miili yao kwa mawe. Wao wakiwa walevi chakari, walionyeshana wale wakulima kwa vidole na kuwacheka (uk73). Mwandishi anatumia picha hii kusawiri maudhui ya kutowajibika na matatizo yanayokumba sekta ya kilimo.

Viongozi wa sekta mbalimbali hawakuwajibikia wizara zao. Wizara hizi zinakejeliwa kwa vile hazikuwa na maendeleo yoyote. Sekta ya elimu ilikumbwa na migomo, katika vituo vya afya matibabu yalidorora nayo wizara ya makazi na nyumba ilikuwa magofu tu. Katika sekta ya kilimo, maisha ya wakulima hayakubadilika miaka kumi ya uhuru iliyopita.Wizara ya biashara ilijaa ufisadi.Viongozi walitumia rasilimali ya umma kwa manufaa yao wenyewe. Viongozi wenyewe wanashiriki katika kuyaharibu

mazingira.Mayai na wenzake wanakojolea mto na maji haya yanatumiwa na wakulima.

Matarajio ya mtunzi ni kuonyesha matumizi mabaya ya rasilimali ya umma ilhali raia wanaangamia katika lindi la mateso. Vile vile, anatarajia kuangazia matumizi mabaya ya mazingira yanayoweza kuathiri afya.Isitoshe, anabainisha viongozi wapotovu wasio vielelezo bora katika jamii.

Kuna picha ya waafrika wanaoonyesha sura za kushiba na macho majanja (uk66). Taswira hii inawasilisha maudhui ya ufisadi. Mayai anashirikiana na watu ambao ni majangili kuendeleza biashara ya kimagendo. Anapotazama picha hizi anazichana na kuzitupa akiogopa mkono mrefu wa serikali. Hii ni dhihirisho tosha kuwa Mayai alikuwa fisadi na alihofia kutiwa mbaroni na serikali. Akiwa katika wizara ya elimu, alifuja fedha ndipo kulikuwa na migomo ya kila mara.Wizara zote zilikumbwa na ufisad i kwani hazikuwa na maendeleo yoyote.

Mwandishi anatumia picha hii akitarajia kubainisha uongozi mbaya usiofaidi wananchi. Anatarajia kutahadharisha wananchi na viongozi waliokosa maadili, wanaoongozwa na ubinafsi, pupa ya kujitajirisha na ukatili.Kwa hivyo, anatarajia kuangazia kubadili mienendo hii potovu ili kuimarisha uongozi.

Katika hadithi ya *"Msamaria* Mwema" mwandishi anatuchorea picha ya Kizito Kibambo anayetaka kumweka Likono nyuma ya gari baada ya kumgonga. Mtunzi anasema ya kwamba mwenye gari, mwanamume wa makamo aliyevalia suti ya hudhurungi, mwenye nywele nyeusi na tumbo pevu, aliruka kufungua mlango wa nyuma wa gari. Aliyekuwa mtu wa kwanza kuchungulia ndani aliruka na kusema

“Ehh umbagaze nyuma kwa kuwa hiyo ndiyo thamani yake? Kwa kuwa umemweka mbwa pale unadhani ana thamani moja na mbwa ehh? Utamweka mbele! Ni binadamu!” (uk81). Picha hii imechorwa na mwandishi kuwasilisha maudhui ya ukosefu wa utu.

Kizito kutaka kumweka Likono nyuma yake gari ilhali ameliweka jibwa lake mbele, ni tendo linalobainisha Kizito alikosa utu. Anakosa kutambua kuwa Likono alikuwa mwanadamu kama yeye. Anathamini sana jibwa lake kuliko Likono ilhali ndiye aliyemgonga kwa gari lake.Hata hivyo, anashurutishwa na wasamaria wema kumweka mbele ingawa anakubali shingo upande.Anaona kuwa gari lake lingechafuka.

Kutokana na picha hii, mwandishi anatarajia kuonyesha umuhimu wa waja kuthamini utu maishani. Anatarajia wanadamu kuwa na utu kwa wanadamu wenzao na si kuwatendea unyama.Vile vile, anaonyesha umuhimu wa kuwaenzi wenzetu jinsi vile tungependa kuenziwa.

Hadithini humu mna picha ya hospitali ya kibinafsi ya Gipfel alikolazwa Likono. Mwandishi anasema kwamba Likono aliwekwa katika chumba cha huduma ya kwanza .Wale wauuguzi walitaka maelezo kuhusu yaliyotendeka.Mmoja wao alishangaa kuona mguu wa Likono uliovimbiana kama bunju (uk83). Taswira hii inaonyesha huduma za afya zilizotolewa.Wasimamizi wa hospital hii walikuwa watu wa tabaka la juu kama kina Kizito Kibambo.Likono anapolazwa hospitalini anashindwa kumudu matibabu kwa sababua alikuwa wa watabaka la chini.

Huduma za matibabu katika hospitali hii zimekumbwa na ufisadi. Daktari anayemhudumia Likono anapendekeza afanyiwe oparesheni. Lengo kuu likiwa anataka tu fedha.Likono anapobadilishwa na kupelekwa hospitali ya Kenyatta, daktari anayemchunguza anapendekeza afungiwe plasta na bado Likono akapona.

Mwandishi anatuchorea picha hii matarajio yake yakiwa ni kuonyesha manufaa ya kusema ukweli maishani na kuepukana kutawaliwa na misingi ya tamaa. Anasisitiza kutolewa kwa maamuzi yanayofaa.

Katika hadithi fupi ya *"Fumbo la Mwana"* kuna picha ya Mzee Atanasi aliyekuwa ametulia chini ya mpapai uliopo mbele ya nyumba yake.Ameketi katika Kiti chake cha henzirani akisinzia. Upande wake wa kulia kuna kopo lenye mabaki ya uji wa mtama,na koo mmoja ananyatia akilinyemelea(uk90). Picha hii inawasilisha maudhui ya umaskini na uchovu aliokuwa nao mzee Atanasi. Ufukara huu unamfanya kushindwa kumudu mahitaji yake ya kimsingi. Lile kopo la uji linaashiria kuwa, asubuhi anamudu tu kunywa uji kama staftahi.Mahitaji yake anayashughulikia kwa kiwango cha chini.Karo inalipwa kidogo kidogo. Anarauka alfajiri na mapema kusaka fedha ndipo tunamwona mwenye uchovu mwingi kwani anapopumzika anasinzia.Ukata huu unasababisha Mzee Atanasi kumshirikisha mwanawe Nanda katika ajira ya watoto ili kujikumu.

Kwa kutumia taswira hii, matarajio ya mwandishi ni kumulika umaskini katika mazingira yake halisi.Anabainisha changamoto zinazotokana na ufukara.Waja hushindwa kumudu mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi na hata elimu. Hali hii ya maisha hulazimu wahusika kutia bidii ya mchwa ndiposa waweze

kujikimu. Hata hivyo, kwa kiwango fulani huweza kushirikisha familia zao katika mambo yasiyofaa.

Katika hadithi, hii kuna taswira ya shule ya sekondari alikokuwa akisoma Nanda. Mwandishi anatueleza kuwa Mzee atanasi anaitikia wito wa mwalimu mkuu anapoitwa shuleni. Mtunzi anasema Atanasi alibisha ofisini pa mwalimu mkuu. Sauti nzito ilimwitikia, akaingia na bakora yake kaibandika kwapani na kijikofia chake kakibeba mkononi. Mwalimu mkuu anamkaribisha na kumweleza alilokuwa amemwitia hasa kuhusu mabadiliko ya afya ya mwanawe Nanda, yaliyokuwa yamechangiwa pakubwa na matumizi ya dawa za kulevya (uk91,92). Picha hii, inawakilisha matatizo yanayokumba sekta ya elimu.

Katika shule hii, wanafunzi wanajihusisha na matumizi ya dawa za kulevya. Matumizi ya dawa hizi za kulevya zinadhuru afya yao, husababisha viwango vya elimu kudorora na hata kutozingatia usafi wa mwili.Vile vile, kuna changamoto ya wanafunzi kushirikishwa katika ajira ya watoto.Nanda, mwanafunzi wa shule hii anatumiwa na Mzee Makulu kulangua dawa za kulevya shuleni. Pia, anashirikishwa katika biashara ya kuuza bidhaa dukani na kazi ya kilimo. Changamoto hizi zinasababisha viwango vya elimu kudorora.

Mwandishi anapotuchorea picha hii anayo matarajio ya kuwahamasisha wazazi kuwajibika katika malezi ya wana wao na si kuacha jukumu hili tu kwa walimu. Anawaangazia wazazi kudhibiti maisha ya watoto wao. Anasisitiza suala la wazazi kuwa na wakati wa kutosha na watoto wao. Hata hivyo, kwa upande mwingine anayo matarajio ya kuonyesha madhara halisi ya matumizi ya dawa za kulevya na ajira za

watoto. Kwa hivyo, mwandishi anawatahadharisha wazazi kuwa waangalifu katika malezi ya watoto wao. Vile vile, kujitahadhari na marafiki wanafiki.

Katika hadithi fupi ya *“Ngome ya Nafsi”* kuna taswira ya picha inayojichora akilini mwetu jinsi Naseko alivyofukuzwa na kushikwa na wale vijana wanne. Wanambeba mzegamzega kumpeleka kwa mumewe aliyelazimishiwa, Mzee Sakaja. Mwandishi anasema kuwa Naseko alilia akitupatupa miguu na mikono yake hewani ili kujinasua. Ilikuwa ni patashika na nguo kuchanika lakini vijana hawa wenye misuli ya siha hawakushindwa kuvizuia vikumbo vyake (uk100). Taswira hii imetumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui ya ndoa za mapema na lazima katika jamii.

Wasichana katika jamii hii walichaguliwa wachumba wakiwa bado wanaendelea na elimu yao. Hawakupewa fursa ya kujichagulia wachumba kwa hiari yao wenyewe. Mahari yalipoletwa mabinti wengi walikatiza masomo yao ili waozwe kwa waume wanaowazidi umri jinsi vile Naseko alivyofanyiwa. Wengi wa wanawake katika jamii hii waliozwa kwa njia hii. Wazazi nao hasa akina mama hawakuhusishwa katika mazungumzo haya ya kuozwa kwa mabinti wao. Walishuhudia tu mabinti zao wakipelekwa kwa waume waliochaguliwa na wazee, yaani akina baba.

Wanawake hawa waliozwa wakiwa wadogo na masomo yao yalikatizwa. Katika ndoa hizi, wanawake walikumbwa na matatizo chungu nzima.Walipigwa kwa makosa madogo madogo, wengine walitishiwa talaka na hata kufa wanapojifungua kwa sababu ya umri wao mdogo. Naseko nusura ayapitie haya kama asingejinusuru.

Matarajio ya mwandishi anapotuchorea picha hii anataka kukashifu mila na desturi zisizofaa katika jamii. Anaonyesha tendo hili kama unyama wanaofanyiwa jinsia ya

kike. Hii ni kwa sababu, hufifisha ari ya watoto wa jinsia ya kike. Mahari hutumiwa kama kigezo cha kudhibiti wanawake na kuwadhulumu kama watumwa. Jinsia ya kike hudunishwa hasa katika ile harakati ya kubebwa na mavazi huchanika.Kwa hivyo, anawazindua wanawake kwa jumla waweze kujikomboa kutokana na mila na desturi zisizofaa. Vile vile, anapendekeza jinsia ya kike kusikizwa katika jamii kwa vile mchango wao una manufaa na ni haki yao. Kwa hivyo, mtunzi anatarajia kubadili mienendo ya wanaume kuweza kuthamini usawa wa jinsia katika jamii.

Hadithini humu pia mna taswira ya kichumba cha Mzee Sakaja. Mwandishi anaeleza kwamba chumbani humu mlikuwa na viti viwili vidogo, kitanda kimoja cha msonabari na mito minne ya rangi ya hudhurungi. Chumbani humu pia mlikuwa na kijimeza cha mviringo kilichotandikwa kitambaa cheupe.Juu yake kulikuwa na bilauri pamoja na chupa iliyojaa maji (uk105). Picha hii inadhihirisha maudhui ya umaskini. Wanawake walipoozwa kwa lazima walikwenda kuishi maisha ya ufukara. Wanaume waliwatumia wanawake kama vyombo vya kukidhi uchu wa mapenzi na kuwazalia watoto. Hawakujali yale makazi waliyoishi. Kwa sababu hii, wanawake waliishi maisha duni.

Mwandishi anachora picha hii akitarajia kukashifu wanaume wanaoongozwa na misingi ya tamaa maishani na kupuuza hali ya maisha iliyopo. Anatarajia kuonyesha jinsi misingi hii ya tamaa inavyoweza kuwaelekeza wanaume kuwadhulumu wanawake kuishi katika makazi duni.

Kuna picha ya makazi ya Bi. Tesi.Tunaelezwa kwamba makao haya yalikuwa na madarasa ya wanafunzi, bweni la wanafunzi, jikoni na mahali pa kupikia chakula.

Kulikuwa na lango la kuingia ndani lililolindwa na bawabu (uk112). Kuwepo kwa madarasa na bweni la wanafunzi inadhihirisha wazi sekta ya elimu. Lile lango linalolindwa na bawabu ni dhihirisho tosha kuwa mahali hapa palikuwa na ulinzi wa kutosha. Kitivo hiki cha elimu kilichomilikiwa na Bi. Tesi kilikumbwa na changamoto nyingi. Kwa mfano, mbali na kuwapa elimu watoto wa kike, alipigana vita dhidi ya tamaduni ambazo zisingewaruhusu watoto wasichana kupata elimu.

Hata hivyo, aliweza kuwapa wasichana hawa ulinzi wa kutosha ili kukamilisha masomo yao ambayo yangekatizwa na ndoa za mapema au lazima. Naseko anayakimbilia makao haya baada ya kujinusuru katika jela la Mzee Sakaja. Anapewa sare na vitabu kutimiza ari yake maishani.Isitoshe, kuna wasichana wengi ambao hawakutimiza ndoto ya malengo yao.Kwa hivyo, makao ya Bi.Tesi yanakuwa kama makao yaliyowaokoa wasichana na mila mbovu zilizowafunga kama watumwa.

Mwandishi anatupa picha hii akiwa na matarajio ya kutaka kuonyesha umuhimu wa kujikomboa maishani.Anatarajia kukashifu suala la kuwafanya waja wengine kuwa watumwa wa mila na desturi zisizofaa.Anatarajia kuzindua kuthamini elimu ya mtoto msichana ili asitumiwe tu kama chombo cha kujipatia mali.

Katika hadithi fupi ya *"Mkimbizi",*kuna taswira ya miili ya nduguze na mamake Musimulizi waliouawa na wanamgambo wa vita. Mwandishi anaeleza jinsi vile mamake wa kambo Musimulizi alivyokufa kwa uchungu mwingi. Anasema mamake alikufa akiwa ameuma mdomo wa chini kwa meno, macho yake yalimtoka kama ambaye alikuwa anagombana na ulimwengu uliompa mgongo (uk117). Pia kuna picha ya Bonde la Betinga ambapo miili ya wafu ilikuwa imetapakaa kila sehemu

(uk121). Isitoshe, hadithini humu mna picha ya mwili wake Jesse rafikiye Musimulizi uliowachwa tu njiani (uk121). Picha hizi zinazochorwa na maelezo ya mtunzi, zinawasilisha maudhui ya tanzia na athari za vita vya kikabila.

Mwandishi anatuchorea picha hizi kubainisha kwamba panapotokea vita hutokea vifo vingi hasa vya jamaa zetu; wazazi, ndugu na hata marafiki.Mamake na nduguze Musimulizi wanauawa usiku huo wa vita.Jesse rafikiye Musimulizi pia anakufa msafarani wakitoroka kutafuta usalama kutokana na maradhi ya nimonia. Vita vya kikabila pia husababisha kukatiza kwa masomo, kwa  hivyo huathiri viwango vya elimu pakubwa. Musimulizi na Jesse wanapotoroka vita hawaendelei na elimu yao.Vile vile, wakimbizi hukumbwa na ukosefu wa chakula na hata uchovu wa safari ndefu. Akina mama na watoto ndio huumia sana

Mwandishi anapochora picha hizi anatarajia kuonyesha hali halisi ya vita. Anadhihirisha jinsi vita vinavyoweza kudhuru maisha ya waja. Watu hukosa usalama na kuishi kwa hofu. Wengine huwachwa yatima na kuishi maisha ya upweke. Pia, husababisha wengi kuwa  na uchungu kwa ajili ya mapenzi ya dhati waliokuwa nayo kwa wapendwa wao wanaokufa vitani.Isitoshe,maendeleo ya eneo husika huzorota kwa sababu ya watu kupoteza mali yao na hata makazi kuharibiwa ovyo ovyo;hali hii hurudisha uchumi wa nchi chini.

Kuna taswira ya kambi ya wakimbizi iliyokuwa mpakani. Mwandishi anasema kwamba sehemu hii ilikuwa imefurika furifuri.Mahema na mahema yalijengwa hapa na pale kiwango cha kuifanya sehemu nzima kuonekana kama iliyotandazwa mawimbi meupe. (uk123). Picha hii inadhihirisha maudhui ya ukosefu wa usalama

nchini. Vita vya kikabila vinapotokea watu hukimbilia usalama wao.Watutsi na Wahutu wanapopigana wote wanakimbilia nchi jirani yaTanzania kwa usalama wao.

Matarajio ya mwandishi kwa kuchora picha hii ni kutaka kuonyesha hali halisi ya maisha ya wakimbizi kambini. Anadhihirisha masaibu wanayoyapata wakimbizi kambini. Anaonyesha jinsi vile kupata chakula huwa ni vigumu, ukosefu wa maji, makazi, mkurupuko wa magonjwa kwa sababu ya wingi wa watu na hata kutegemea wafadhili kwa misaada.

Katika hadithi fupi ya *"Ndimi za Mauti"* kuna taswira ya bweni linaloteketea kwa moto wanafunzi wakiwa ndani. Mwandishi anaeleza jinsi wanafunzi walivyokuwa waking'ang'ana kujiokoa moto ulipozuka.Mtunzi anasema kwamba kila mmoja alikimbilia mlangoni wengi wao wakibanana mlangoni.Mlango ule wa upembe wa nje ulikuwa umekomelewa nje. Wengine walijinasua kwa kupitia madirishani (uk128). Picha hii inadhihirisha maudhui ya changamoto zinazokumba sekta za elimu hasa shule mbalimbali.Miongoni mwa changamoto hizi ni migomo shuleni.

Wanagenzi wanapoelekezwa na walimu wao kufuata sheria za shule huona kwamba wanadhulumiwa na mara nyingi huchocheana na kuandamana. Hali hii husababisha wanafunzi kuteketeza shule na kudhuru wenzao na hata kuharibu mali mengi ya shule. Mbunda na Kamaliza wanasema kwamba mwalimu mkuu anawakazia ,kwa hivyo wanapanga mipango yao na kuteketeza bweni kwa moto.Wanapotekeleza unyama huu, wanawadhuru wanafunzi wenzao sitini na wanane.

Changamoto nyingine inayokumba shule nyingi na kupelekea migomo, ni ile inayotokana na nidhamu ya wanafunzi pale shuleni. Wazazi wengi hawawajibiki

katika malezi ya wana wao.Jukumu la nidhamu limewachiwa walimu.Vile vile, hapana usawa wa nidhamu shuleni na nyumbani.Wazazi wamewatelekeza watoto wao nyumbani. Mbunda anasema kwamba yeye wazazi wake hawajawahi kumwaadhibu. Kwa hivyo, wanaamua kumfunza mwalimu mkuu funzo kwa kuwaadhibu pale shuleni.

Mwandishi anatumia taswira hii kuashiria suala la wazazi kuwapa watoto wao fedha nyingi za matumizi shuleni. Fedha hizi, wanafunzi huzitumia kununulia hata vifaa hatari vinavyoweza kuleta madhara makubwa pale shuleni. Musesi ndiye aliyehusika na kununua petrol iliyotumiwa kuteketeza bweni. Anapotaka kujitoa katika shughuli hii, Mbunda yuko tayari kumrejeshea fedha zake na yeye kununua petroli nyingine

Mwandishi anatumia taswira hii matarajio yake yakiwa ni kuzindua uongozi wa shule kuhusisha wanafunzi katika vikao vya maoni au kuwasikiliza wanapokuwa na matatizo. Umuhimu wa mawasiliano unasisitizwa. Mawasiliano husaidia kusuluhisha migogoro katika sekta yoyote ile husika.Vile vile, anatarajia kuzindua jamii nzima kushirikiana katika malezi ya watoto ili kusiwe na utofauti katika malezi.

Vile vile, mtunzi ameitumia taswira hii akitaka kutahadharisha uongozi wa shule kuhakikisha kwamba wanafunzi wana usalama wa kutosha wanapokuwa pale shuleni. Kuwepo na milango inayoweza kusaidia wanafunzi kukwepa hatari na madirisha yasiambwe kwa vyuma. Magari ya wazima moto pia yaweze kuwasili kwa wakati pahali pa mkasa. Walimu wakuu wanapaswa pia kuwafunza vijana mbinu za kujiokoa.

Pia, kuna picha ya wazazi na jamii nzima iliyofika pale shuleni kuuzima moto uliokuwa ukiteketeza bweni. Mwandishi anasema kuwa watu walifika katika shule hii ya Angeko (uk129). Taswira hii inasawiri maudhui ya umoja na utangamano. Wanakijiji wote wanashirikiana kuuzima moto ili kuokoa roho za wanafunzi zilizokuwa zinapigania uhai. Umoja na ushirikiano huu unahitajika kila wakati si tu panapotukia balaa au shida.

Picha hii imetumiwa na mtunzi kuhamasisha sekta za elimu au zozote zile kuwa na vifaa mwafaka vinavyoweza kutumiwa kuuzima moto unapozuka.Isitoshe, anahamasisha jamii kwa ujumla kuwa na ujamaa  ili kuweza kutekeleza majukumu bila kuzingatia mipaka.

Kuna picha ya hospitali walikolazwa manusura (uk130). Picha hii inadhihirisha huduma za afya. Kituo hiki cha afya kinatoa matibabu kwa waathiriwa wa majanga kama haya ya moto na mengine mengi. Manusura wa shule ya  Angeko kama kina Musesi walinusurika kifo baada ya kupewa matibabu pale hospitalini. Matarajio  ya mwandishi anapochora picha hii ni kutaka kuonyesha kazi muhimu inayotekelezwa na sekta ya afya.

Aidha, kuna picha inayojichora akilini mwetu ya eneo lililochomeka likachukua sura ya tanuri la kuchomea makaa. Mwandishi anasema kuwa mahali pale palikuwa na majivu na uweusi  uliotandaa pote. Miti  iliyokuwa karibu na pale ilivaa weusi,viunzi vya vitanda vya nyaya na masanduku ya bati vilienea  pote (uk130). Picha hii, inawasilisha maudhui ya uharibifu wa mali na mazingira. Wanafunzi wengi waliangamia ,vitabu, malazi,vitanda,sare za wanafunzi na bweni  lenyewe,vyote

viliharibiwa na kuwa majivu tu. Vitu hivi vilivyoharibiwa na moto vitagharimu shule na hata wazazi fedha nyingi.Miti iliyonawirisha mazingira, kuleta mvua na kutumika hasa katika ujenzi inachomeka na kuwacha mazingira ambayo hayavutii.

Mwandishi ameitumia taswira hii kutaka kuonyesha madhara ya moto. Anatahadharisha  jamii kuepukana na hali ya kulipiza kisasi maishani. Anataka waja kuweza kutambua pengo kubwa ambalo linaweza kusababishwa na tendo hili.

Pia, kuna picha ya ibada ya kikao cha matanga.Waliozungumza katika kikao hiki walikashifu tendo hili la unyama (uk132). Picha hii inawasilisha maudhui ya dini. Kuna kasisi anayeongoza ibada hii kuzika miili ya wanafunzi walioteketezwa kwa moto. Ibada hii imeandaliwa rasmi ili kuombea roho za wafu na pia kuwafariji waliofiwa. Taswira hii imetumiwa na mtunzi akitarajia kuonyesha nafasi muhimu ya dini katika jamii. Dini hutia waja tumaini.

Katika hadithi hii, pia kuna picha ya Musesi anayedondokwa na machozi akijiuma kidomo chake cha chini,majina ya wenzake walioaga yalipokuwa yakisomwa (uk132). Upande ule mwingine kuna picha ya watu wanaofuatilia ile ibada ya mazishi. Mbanda pia alikuwa miongoni mwa watu hawa.  Alianza kujilaumu kwa kutekeleza kitendo hiki.Wandani wake wawili pia waliangamia (uk133). Picha hizi zinawasilisha maudhu ya majuto.

Musesi alijua mpango wa bweni kuteketezwa lakini  anaporudi katika bweni  lakini hawajuzi  wenzake wala  kumweleza   mwalimu mkuu kutahadhari.Hali hii ndiyo inayomfanya kujutia kwamba  laity angewajuza wenzake.Naye Mbanda anajutia

tendo lake la kuwateketeza wenzake. Jambo hili linamhuzunisha sana na kumfanya kuwa mwenye mawazo mengi kichwani.

Mwandishi anatuchorea picha hizi kutaka kutahadharisha watu wanaopenda kufanya mambo kimzaha na mwisho yakasababisha maafa makubwa maishani. Anaonyesha jinsi vile mzaha unavyoweza kupelekea waja kukumbwa na simanzi, hofu na hata upweke.

Kuna picha ya kituo cha polisi. Mbanda baada ya kuteketeza bweni na kujiona mwenye makosa anajisalimisha katika kituo hiki cha polisi ili sheria ichukuliwe. Kituo hiki cha polisi kinachunguza wale wanaovunja sheria na kuwatia mbaroni. Kwa hivyo, kinasaidia kuhakikisha kuwa haki inatendeka.Mtunzi anachora picha hii akitarajia kuonyesha matumizi ya sheria katika jamii.

## 3.3 HITIMISHO

Katika sura hii, tumejadili matumizi ya taswira katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Matumizi haya ya taswira yametazamwa katika hadithi fupi zilizoteuliwa kutoka Diwani mbili za Kiswahili. Diwani hizi ni za: *Pendo la Heba* na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Tumetazama matumizi haya ya taswira yanavyotumiwa kusawiri maudhui ya mwandishi.Vile vile, tumeonyesha matarajio yanayotokana na matumizi haya ya taswira.

## SURA YA NNE

# MATUMIZI YA TASHBIHI,TASHIHISI,MAJAZI NA ATHARI ZINAZOTOKANA NA MATUMIZI HAYO KATIKA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI

## 4.0 UTANGULIZI

Katika hii sura, tumeelezea matumizi ya tashbihi, tashihisi na majazi katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Tumebainisha pia dhima kuu ya matumizi ya mbinu hizi katika utafiti huu.Isitoshe, matarajio ya matumizi ya mbinu hizi yamejadiliwa kwa mapana. Matumizi haya tumeyaangalia katika machapisho ya *Pendo la Heba (1996)* na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004).*Katika sura hii,mihimili yote mitatu ilitumiwa kuonyesha matumizi ya mbinu hizi.

## 4.1 Matumizi ya Tashbihi

### 4.1.1 Pendo la Heba

Tashbihi ni tamathali ya usemi ambayo hulinganisha vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti kwa kutumia maneno kama vile; mithili ya, kama, mfano wa, sawasawa na, miomgoni mwa mengine. (Senkoro 1981:14,1993:4,Khatibu1999:77) Dhima kuu ya matumizi haya ya tashbihi katika utafiti wetu ni kusawiri ujumbe wa mwandishi katika diwani husika za hadithi fupi zilizoteuliwa.

Katika hadithi fupi ya *"Mtembo"* tunaelezewa kuhusu familia ya akina Fadhila kwamba babake na mamake waliishi wakipendana kama chanda na pete (uk27). Tashbihi hii imetumiwa kudhihirisha maudhui ya mapenzi na ndoa.Ndoa baina ya wazazi wake Fadhila ilijengwa kwa misingi ya upendo na uaminifu. Mapenzi yalikuwa ya dhati, walimpenda binti wao Fadhila na kumuenzi kwa vyovyote vile.

Mwandishi anatumia tashbihi hii kujenga tabia au mienendo ya mhusika katika jamii.Kwamba ni wenye mapenzi ya dhati.Kwa hivyo, hii imejenga utangamano katika jamii hii.

Hadithi hii pia inaelezea kumhusu Fadhila ambaye aliteswa na mamake wa kambo ambaye wakati mwingi hakumpa chakula hali iliyosababisha Fadhila kudhoofika kiafya na kuwa kama ufito (uk28). Hapa, tashbihi hii imetumiwa kuelezea maudhui ya wivu na chuki katika ndoa. Kutokana na wivu na chuki aliokuwa nao mamake wa kambo, anamshurutisha Fadhila katika mateso ya kila anuai. Hamlishi vema, hamvishi vizuri jinsi alivyokuwa akifanyiwa hapo awali na wazazi wake halisi,waliompa mahitaji yote ya kimsingi.

Mwandishi anaeleza athari inayotokana na ukosefu wa chakula mwilini.Ameonyesha jinsi vile muhusika anavyoweza kudhoofika kiafya na hatari hata ya kuweza kufa au kuwa na maumbile yanayotisha.

Kuna vile vile, maelezo yanayomhusu mamake Mganga ambaye alikuwa amelazwa hospitalini kwa kufanyiwa upasuaji. Tunaambiwa kwamba baada ya kuugua kwa muda mrefu alipokuwa akilala kitandani alionekana kama gofu la mtu lililotupwa

ovyo (uk49). Mwandishi wa hadithi hii ameitumia tashbihi hii kudhihirisha maudhui ya mkurupuko wa maradhi. Maradhi haya yamesababishwa na uchafu wa kila anuai ulioenea kote katika kijiji cha Mathare walikoishi akina Mganga na mamake pamoja na dadake Siti. Miongoni mwa maradhi haya, ni kipindupindu kilichomwangamiza Siti dadake Mganga.

Matarajio ya mtunzi anapoitumia tashbihi hii ni kwamba anamtaka msomaji kuona madhara yanayoweza kusababishwa na magonjwa kama yale ya kipindupindu.Mtu hukonda na kuwa na maumbile yanayotia hofu.

Katika hadithi fupi ya "Mtembo"tunaelezewa kuhusu mwana wa mfalme ambaye alikuwa amemwoa Fadhila baada ya kufuzu kuutoa mtembo uliokuwa uking'aa kwenye mto na kumletea mwana huyu wa mfalme. Anapotambua kwamba amebadilishiwa mkewe Fadhila, na kupewa Hasidi, anakuwa mkali kama moto kwa hasira (uk 39). Kupitia tashbihi hii, inadhihirisha maudhui ya wongo. MwanaMize anajaribu kumlaghai mwana wa mfalme kwamba, Hasidi ndiye aliyekuwa mkewe wa halali. Haya yanatambuliwa baadaye na ikawa Hasidi auawe na kufanywa kitoweo.

Matarajio ya mtunzi anapoitumia tashbihi hii anataka kubaisha mienendo ya mwana wa mfalme kwamba ni mtu ambaye ni mkali vile vile mwenye hasira.

Aidha, mwandishi wa hadithi fupi ya *"Jehanamu"*ametuelezea masikitiko aliyokuwa nayo Mganga alipomtembelea mamake aliyekuwa mgonjwa pale hospitalini. Anapiga magoti pale kitandani na kulia kama mtoto mdogo (uk.49). Maudhui yanayodhihirishwa na matumizi ya tashbihi hii ni ya ukiwa na upweke. Mganga

anakuwa na hofu pia huzuni mwingi anapotambua kuwa mamake huenda akakata kamba kutokana na ugonjwa aliokuwa akiugua. Hali hii inamfanya kujiona mwenye upweke uliosababishwa na magonjwa yaliyoleta utengano miongoni mwa aila hii iliyotawaliwa na mapenzi ya dhati.

Mwandishi wa hadithi hii ameitumia tashbihi hii akitarajia msomaji kutambua umuhimu wa kuthamini na kuwaenzi wazazi wetu. Anaonyesha kuwa wazazi huwa uti wa mgongo katika familia. Kwa hivyo, wanapoathirika kwa njia moja au nyingine, huweza kusababisha watoto wao kuathirika kisaikolojia. Kwa hivyo, anaonyesha nafasi muhimu inayochukuliwa na wazazi katika aila yoyote ile.

Vile vile, nyumba ya Mheshimiwa Mlaji, mbunge wa eneo la Jangwani imeelezewa kuwa kubwa.Mwandishi anasema jumba hili lilionekana kama kasri la kifalme lilimkodolea Maria macho na hapo moyo wake ulianza kumwenda mbio kwa dukuduku (uk51). Hapa, tashbihi hii imetumiwa kuelezea maudhui ya utajiri. Inathibitisha kwamba, matajiri waliishi mitaa ya kifahari na makazi mazuri ikilinganishwa na maskini. Kwa jumla, waliweza kukithi mahitaji yao ya kimsingi kama vile chakula, mavazi makazi na hata elimu. Mbunge Mlaji alikuwa tajiri wa kutajika ndipo jumba lake limelinganishwa na jumba la kifalme. Naye Maria alikuwa anatoka katika familia maskini ndipo anakuwa na shauku kama angekaribishwa katika jumba hili la kitajiri.

Mwandishi huyu anaitumia tashbihi hii akitarajia msomaji kuona ule utengano ambao huwepo kati ya matajiri na maskini. Anaonyesha jinsi vile utengano huu unavyoweza kuwaweka hofu maskini wasiojiweza. Anamtaka msomaji kuona jinsi maskini

huendelea kuijidunisha na kuangamia katika lindi la shida kwa sababu hawapati ile fursa ya kuweza kutangamana na matajiri ili wawasaidie kutoka katika matatizo yanayowakumba.

Isitoshe, Maria alipofika kwa mbunge, alikaribishwa kwenye kiti kikubwa chenye foronya. Kiti hiki kinasemekana kilikuwa laini kama sufu (uk52). Mwandishi anasisitiza jinsi ambavyo kiti kilikuwa laini. Kinachoendelezwa na tashbihi hii ni maudhui ya utabaka. Watu wa tabaka la juu wanamiliki vitu vya hali ya juu inapolinganishwa na wale wa tabaka la chini. Mbunge Mlaji alimiliki fanicha nzuri na za bei ghali mno.Akina Maria wanaotoka katika tabaka la chini hawakumiliki chochote cha thamani.

Mwandishi anapotumia tashbihi hii, anatarajia kufananisha vitu viwili.Anaonyesha jinsi nyumba za matajiri huwa kubwa na husheheni vitu vya bei ghali inapolinganishwa na zile za maskini ambazo huwa tu ndogo kiasi cha haja yao na zisizo na vitu vyovyote.

Pia, tumeelezewa kuhusu hali ya Njeri baada ya daktari Madevu kumdadisi na kugundua kuwa alikuwa akiugua ugonjwa usiokuwa na tiba. Njeri anapopanda basi kurudi chuoni tunaambiwa kwamba anajibwaga kwenye kiti kama gunia (uk66). Vile tunaambiwa kuwa mkono wake unakuwa mdhaifu kama mwilli mzima (uk67). Hata hivyo, anawatazama wasafiri wenzake kama sanamu (uk67). Mwandishi amezitumia tashbihi hizi kudhihirisha maudhui ya uchovu na masikitiko.

Mtunzi wa hadithi hii fupi, ametumia tashbihi hizi kuonyesha mienendo ya waja kuwa, ni wenye  kupenda anasa na kukosa uaminifu.Hali hii inawatumbukiza katika lindi la mashaka.Wanajipata wenye wasi wasi na mashaka baada ya kujitosa katika mienendo ya uhawara.

### 4.1.2 Mayai Waziri wa Maradhi

Kuna matumizi ya tashbihi pia katika Diwani hii.Katika hadithi fupi ya *"Siku ya Mganga"*tumeelezwa kuhusu hali ya mkewe Mteja wa kwanza baada ya kuugua kwa muda na kuletwa kwa matibabu kwa mganga Mwaibale. Tunaambiwa kuwa alikuwa amekonda kama sindano (uk26).Vile vile nywele kichwani  zilikuwa kama kamba za katani (uk27). Istoshe aliharisha kama bomba la maji (uk27). Matumizi haya ya tashbihi yanadhihirisha wazi maudhui ya maradhi.

Maradhi yanayozungumziwa ni maradhi ya ukimwi. Mke wa Mteja wa kwanza alikuwa akiugua ugonjwa huu wa ukimwi. Analetwa kwa matibabu kwa mganga Mwaibale ambaye pia ni mbumbumbu na hana maarifa kuhusu maradhi haya. Anatumia wembe ule alioutumia kumchanjia chale mgonjwa huyu wa ukimwi kwa wateja wengine waliowasili pale kwake siku hiyo.Bila shaka, anachangia katika suala la kueneza ugonjwa huu wa ukimwi.

Matarajio ya mtunzi ni kutaka msomaji kuelewa madhara ya ugonjwa wa ukimwi kwa mja.Ugonjwa huu husababisha afya ya waja kudhoofika na kuonekana kama watu ambao hawastahili kuishi katika familia.Wanashukiwa na kutengwa kwa sababu ya dalili wanazozionyesha.

Vile vile, tumeelezewa kumhusu Mavitu kuwa wanakijiji wanapozungumzia kuhusu mienendo yake mibovu ya kumdhibiti mkewe Sakina, anachukizwa nayo.Mwandishi anasema kuwa maneno haya yanamng'ata moyoni kama usena wa nyuki (uk42). Tashbihi hii imeetumiwa kusawiri maudhui ya ukweli. Wanakijiji wanaposema ukweli kumhusu Mavitu, kuwa ana mazoea ya kumdhibiti mkewe anayemshuku kuwa na uhusiano na wanaume wengine anakasirishwa. Lakini ukweli ni kwamba hulka hii si nzuri.

Mwandishi ameitumia tashbihi hii akitarajia kubainisha tabia ya Bwana Mavitu.Kuwa ni muhusika mwenye hasira na asiyependa kuambiwa ukweli wa mambo.

Mwandishi pia, anasema kwamba serikali ilipokata msaada kwa wananchi wa Kijiji cha Imanga, ilikuwa kama jabali kubwa lililomwangukia Mavitu (uk43). Matumizi ya tashbihi hii inasawiri maudhui ya umaskini.Familia ya Mavitu ilikuwa na uwezo mdogo wa kumudu mahitaji yao ya kimsingi. Hasa chakula, mavazi na elimu.Mara nyingi walitegemea serikali kuwapa chakula na hata kuwalipia karo shuleni.Msaada huu unapotolewa, unampiga butwaa Mavitu ambaye sasa hakuwa na namna nyingine ya kukidhi mahitaji ya familia yake.

Mwandishi ameitumia tashbihi hii akitarajia kuonyesha jamii umuhimu wa kujitegemea maishani. Anaangazia hatari inayoweza kutokea ikiwa mhusika atakuwa wa kutegemea watu maishani mwake. Hata hivyo, anaizindua jamii kwa mapana kwa kuzaa watoto wanaoweza kuwapa malezi bora na kuepuka kuwa wahitaji wa kupindukia.

Pia, tumeelezwa kwamba shida ziliendelea kuwaning'inia kama mikanda ya masizi (uk45). Tashbihi hii imetumiwa kuendeleza maudhui ya matatizo maishani. Familia ya Mavitu iliweza kukumbwa na matatizo si haba hasa baada ya Mavitu na mkewe Sakina kuwacha kazi. Mwanzo, watoto wao wanakatiza elimu, shamba lao kuchukuliwa na tajiri wao, bintiye Mavitu kuwa mjamzito na mwisho Mavitu kujitia kitanzi.

Matarajio ya mtunzi atumiapo tashbihi hii anataka kuonyesha sifa ya waja kwamba wawe wenye bidii maishani ili wapate mapato ya kutosha kujikimu katika maisha.Wasiwe tu walala hoi wakutegemea wenzao.

Katika hadithi fupi ya *"Ngome ya Nafsi",* tumeelezewa kumhusu Naseko aliyekuwa anawatoroka wale vijana waliotaka kumnasa ili kumwoza kwa mchumba aliyemzidi umri. Naseko anajipenyeza katikati ya vijana hawa kama risasi (uk 100). Wanapofua dafu kumnasa wanambeba kwa urahisi kwa sababu mwandishi anatueleza kwamba alikuwa kama mzigo wa sufi.(uk.100).Matumizi ya tashbihi hizi zinadhihirisha maudhui ya taasubi za kiume.

Wanawake walipewa nafasi duni katika jamii hii. Hawakupewa  nafasi ya kutoa ushauri au maoni kwani walidharauliwa na kutohusishwa  katika maamuzi yoyote. Babake Naseko hakumhusisha katika kuchagua mchumba  anayempenda.Anaamua Naseko ashikwe na aozwe kwa Mzee Sakaja anayemzidi umri.

Mwandishi ameitumia tashbihi hii akitarajia kuonyesha sifa ya wavulana waliotumiwa na jamii kuwanasa wasichana wadogo na kuwaoza kwa lazima kwa

waume waliowazidi umri.Anaonyesh kwamba walikuwa wenye nguvu na uwezo mkubwa ambao ulizidi walionaswa kama kina Naseko.

Vile vile, tunaambiwa kuwa Naseko alipokuwa amefungiwa katika kichumba baada ya kubebwa hobelahobela,anakumbana na mzee mwenye ndevu nyeupe mithili ya theluji (uk101). Mzee huyu alionekana mwenye hasira nyingi Naseko anapojibizana naye.Tashbihi hii imetumiwa kuthibitisha maudhui ya udhalimu wa jinsia ya kike.Mzee Sakaja anatumia umri wake mkubwa kutaka kumdhulumu Naseko. Hamruhusu Naseko kuzungumza na anapomjibu anaona kama msichana huyu mdogo alikosa heshima kwake. Anakuwa mkali na kutaka kumuadhibu.

Mwandishi ameitumia tashbihi hii akitarajia msomaji kuweza kutambua wahusika wenye hulka dhulumati katika jamii zetu. Wahusika hawa mara nyingi hujitakia makuu upande wao pekee. Kila wakati, hutaka walimbikiziwe sifa tele tele.Lakini wao hawawapi wengine heshima hiyo , hasa jinsia ya kike.Huwa wanatawaliwa na misingi ya ubinafsi na kuwadharau wengine.

Aidha, katika hadithI hii tumeelezwa kuhusu hatima ya mtoto wa kike katika jamii.Mwandishi anasema kuwa Naseko anapotoroka kujinusuru, alipita kwenye msitu uliokuwa na miti iliyoonekana kama majitu (uk101). Pia, tunaambiwa kuwa alisikia sauti ya milio kama upepo ikimjia (uk.110). Anaachilia usiyahi unaopenye kwenye msitu kama mwale wa moto (uk110). Mtunzi anasema kuwa Naseko anatetemeka kama unyasi (uk110). Hali hii inatokea hasa Naseko anapokumbana na mwanamume mmoja kwenye msitu. Maneno ya mwanamume huyu yanamchoma

Naseko kama mshale (UK.110). Anatoa kicheko mithili ya sokwe (uk 111). Matumizi haya ya tashbihi hizi yanadhihirisha maudhui ya vizingiti au vizuizi vya ukombozi.

Jamii hii haikuthamini elimu ya mtoto wa kike. Ndipo Naseko anatoroka kujinusuru ili aweze kuendelea na elimu yake.anakumbana na vizingiti hivi:hatari ya wanyama wa mwituni na mwanaume ambaye alimchekelea badala ya kumsaidia.Mtunzi anatarajia kuonyesha sifa ya uoga ambayo wahusika humiliki wanapokumbana na hatari.

Aidha, Naseko anapowasili na kufika kwa Bi.Tesi, mwanamke mmoja aliyestawisha makao yaliyowahifadhi wasichana waliolazimishiwa ndoa za lazima, kuna watoto waliomkodolea macho kana kwamba waliona kizuka (uk111). Pia,Bi. Tesi anapozungumza na Naseko, Naseko anayaona maneno hayo kama ukombozi katika jamii. Naseko anawekwa huru na kupewa chumba, vitabu ili kuendelea na masomo yake ambayo nusura yakatizwe.

Matarajio ya mwandishi anapotumia tashbihi hizi anataka kuonyesha hali halisi ya jinsia ya kike katika jamii.Kuwa, hawakupewa uhuru bali waligandamizwa na kunyimwa haki zao za kimsingi na hawakuruhusiwa kutangamana na wenzao katika jamii kielimu.walifungwa na mila gandamizi.

Vile vile, tunaelezwa kuwa Naseko aliwaona wasichana ambao hawakuweza kujinasua kama viumbe waliofungiwa ndani ya ngome (uk114). Tashbihi hii imetumiwa na mwandishi kusawiri maudhui ya mateso.Jinsia ya kike ilipitia mateso ainati hasa kutumiwa kama vyombo vya kufanya kazi za nyumbani,kuozwa kwa

lazima,kutoelimishwa na hata kutohusishwa katika kutoa ushauri. Mtunzi ametumia tashbihi hii akitaka kuonyesha mienendo ya wanajamii walio na sifa dhulumati katika jamii.

Katika hadithi fupi ya *"Mkimbizi"* tumeelezwa na mwandishi kwamba kilio cha mamake wa kambo wa Msimulizi kilikuwa kama dua ya kuku isiyompata mwewe (uk116). Tashbihi hii imetumiwa kudhihirisha maudhui ya ukatili. Mamake wa kambo Msimulizi anauawa na wanamgambo wa vita bila huruma. Anawaomba msamaha lakini wanamwua kwa bunduki walizokuwa wamejihami nazo. Kuuawa kwake kwa ukatili, kunapelekea Musimulizi kuwa na huzuni nyingi alipoona mamake akiuawa kwa ukatili.

Mwandishi ametumia tashbihi hii akitaka kuonyesha hali halisi ya vita.Kuwa, vita husababisha mauaji, uyatima na athari za kisaikolojia kwa watoto wanaosalia nyuma.

Pia, katika hadithi hii, tunaambiwa na mtunzi ya kwamba baada ya msimulizi kunusurika kifo na wanamgambo walioangamiza familia yake,anasikia bundiki zikipigwa kama ngoma.(uk.118), kisha akatetemeka kama mgonjwa wa homa (uk119).Tashbihi hizi zinadhihirisha maudhui ya uhasama wa kikabila. Uhasama huu husababisha vita, hutia woga na kuhatarisha maisha ya waja.

Mwandishi ametumia tashbihi hizi kuonyesha athari ya vita .Anabainisha kwamba vita hutia jamii uoga na hasa watoto wadogo huathirika kimawazo.

Matumizi ya tashihisi kwa mujibu wa Mohamed (1995) tashihisi ni mbinu inayotumiwa na mwanadamu kuvihusisha vitu visivyo na uhai na vyenye uhai hasa binadamu mwenyewe . Vitu hivi visivyo na uhai hupewa sifa tabia au matendo ya kiuhai na kibinadamu.

Hata hivyo, tashihisi inalenga kuvipa vitu visivyo na uhai sifa za kibinadamu kwa njia ya maelezo. Vile vile husisitiza sifa ya kitu hicho ambacho ni muhimu katika hadithi. Isitoshe, huleta ufundi au mvuto wa kisanaa katika hadithi. Huweka pia uzito wa matukio katika vitushi muhimu. Zaidi ni kwamba tashihisi inaweka wazo zaidi maana.

## 4.2 Matumizi ya Tashihisi

### 4.2.1 Pendo la Heba

Mtunzi katika hadithi fupi ya " jitu la kisasa" anatueleza hali ilivyokuwa baada ya Nanjekho kufa. Anasema bintiye Mzee Lomo alipokata kamba. Vilio na kwikwi zilipasua miti iliyojenga ua la hospitali. (uk. 40) katika kauli hii vilio vinapewa sifa ya mwanadamu ya kupasua miti.

Kwa hivyo matumizi haya ya tashihisi yanadhihirisha hisia za huzuni. Nanjekho alipoaga, jamii nzima inahuzunika na kuomboleza pale hospitalini kama ishara ya upendo kwa kiumbe huyu.

Mwandishi ametumia tashihisi hii akitarajia kuonyesha hali halisi, kifo kinapotokea kwamba kuna pengo kubwa ambalo huachwa. Nafasi hii haiwezi kufidiwa na mhusika mwingine . Maisha ya waja yanathaminiwa kwa kiwango kikubwa.

Vile vile katika hadithi hii mtunzi, pia ametueleza kuhusu hali ya Nanjekho baada ya kufa kuwa Nanjekho alinyongonyea na kuzungukwa na ubaridi pande zote za mwili wake. (uk. 40). Hapa baridi imepewa sifa ya kibinadamu ya kuzunguka. Mtunzi ameitumia tashihisi hii kujenga maudhui ya mauti. Nanjekho baada ya kuwa mgonjwa anapelikwa hospitalini na wazazi wake, huko anaugua kwa muda na baadaye kukata roho. Mazishi yanatayarishwa kule mashambani Iambeka kwa Mzee lomo ili kumzika Nanjekho.

Matarajio ya mtunzi anapotumia tashihisi hii anataka kubainisha hatua katika maisha ya wanadamu. Anaonyesha hatua katika maisha ya wanadamu. Anaonyesha kuwa mwanadamu huzaliwa, hukua na mwisho hufa. Anawachochea watu kukubali kifo maishani mwao. Kwamba kifo kina nguvu na hakiwezi kikaepukwa.

Aidha tunaambiwa kuhusu vibanda vya wakazi wa Mathare vilivyoteketea kwa moto. Mwandishi anasema kuwa vibanda zaidi vilimezwa na zimwi lile la moto (uk 47).

Moto unapewa sifa ya kibinadamu ya kumeza. Matumizi haya ya tashihisi yanadhihirisha maudhui ya ukosefu wa vifaa mwafaka vya kuzima moto. Kijiji hiki cha Mathare alichoishi mganga pamaoja na aila yake kinateketezwa kwa moto isipokuwa tu makazi ya kina mganga. Juhudi za kuuzima moto huu na wanakijiji haukufua dafu. Magari ya wazima moto yanawasili baada ya mali nyingi kuharibiwa

na moto na hata kusababisha vifo. Tumeelezwa kuwa kuna mtoto mchanga aliyekuwa akilala katika kibanda mojawapo, aliyeteketezwa kwa moto.

Matarajio ya mtunzi kutokana na matumizi ya tashihisi hii anataka kuonyesha hasara inayoweza kuletwa, panapozuka moto.Anaonyesh kwamba moto huweza kusababisha kifo na uharibifu wa mali.Vile vile anaonyesha ukosefu wa kuweka mikakati bora ya kuthibiti hatari ya moto.

Pia mwandishi wa hadithi fupi ya``Genge`` anaeleza jinsi vile jumba la Mheshimiwa Mlaji lilivyoonekana Maria alipokuwa akilikaripia. Tunaambiwa kuwa jumba hili la kifalme lilimkodolea macho Maria ambaye alishuku kama angekaribishwa ndani (U.K 51). Jumba linapewa sifa ya kukodoa macho sifa ambayo hupatikana tu kwa wanadamu. Tashihisi hii imetumiwa kuonyesha utabaka katika jamii. Jamii hii iligawika katika matabaka mawili. Tabaka la juu na la chini. Watu kama Mheshimiwa Mlaji walikuwa wa tabaka la juu. Hii inathibitishwa na jumba kubwa alilokuwa nalo, bawabu langoni na fanicha chungu nzima jumbani mwake. Maria anayeenda kuomba asaidiwe kupata ajira, alikuwa wa tabaka la chini. Yeye ni mchochole, anatembea kwa miguu hana ajira na hii hali yake ndiyo inayomfaya kushuku kama angekaribishwa ndani kwa Mheshimiwa Mlaji.

Matarajio ya mtunzi kwa matumizi haya ya tashihisi ni kutaka kuonyesha sifa kuu walionao watu wa tabaka la juu kuwa mara nyingi huwa na dharau, si wakarima na ni waovu. Vile Vile wametawaliwa na ubinafsi wa kiwango cha juu.

Hadithini humu pia mwandishi anatueleza hali ilivyokuwa baada ya Mkaange kumpapasapapasa Maria pale hotelini. Anasema kuwa Maria alipomsukuma akaanguka chini kuta za chumba kizima ziliteteméka. (U.K 59). Matumizi haya ya tashihisi hii yanadhirisha dhuluma walizofanyiwa kina Maria. Maria anaalikwa hotelini Peponi na kina Mlaji na Mkaange kwa lengo la kumpa ajira lakini baadaye Mkaange baada ya kunywa mvinyo na kulewa chakari anataka kumdhulumu kimapenzi.

Mwandishi ametumia tashihisi hii akitarajia kuonyesha jinsi viongozi waliotawala na kuwalinda wananchi walivyokuwa wapotovu na wakosefu wa adhabu kwa wananchi wanaowatumikia. Mtunzi anaonyesha jinsi walivyoongozwa na tamaa mbaya iliyosababisha madhara kwa wananchi. Anadhihirisha jinsi viongozi hawa walivyotumia nafasi na vyeo vyao kuwa dhulumu wachochole

**4.2.2 Mayai Waziri wa Maradhi.**

Mwandishi ameeleza katika hadithi fupi ya "Kachukua Hatua Nyingine" kuhusu hali ilivyokuwa katika familia ya Mavitu. Anasema kwamba Njaa ilikuwa ikiwatanulia mabawa na kuwakondolea macho.

(uk 40). Kutanua na kukodoa ni sifa za uhai ambazo haziwezi kumilikiwa na njaa, matumizi haya ya tashihisi hii yanadhihirisha swala la ukosefu wa chakula. Familia ya Mavitu haikuweza kumudu mahitaji haya ya kimsingi. Ilitegemea serikali kutoa msaada.

Mwandishi ametumia tashihisi hii akitarajia kuonyesha umuhimu wa kuwa na uwezo katika jamii. Anasisitiza swala la waja kuwa na ajira itakayowasaidia kuweza kumudu mahitaji yao ya kimsingi ya kila siku.

Pia hadithini humu ameeleza hali ilivyokuwa kwa Sakina Mkewa Mavitu. Anasema kuwa wakati huo Shemeji alikuona mbele kumevaa vazi kubwa jeusi (uk 39). Dhana ya mahali imepewa sifa ya kibinadamu ya kuvaa. Hii inadhihirisha wazi suala la kukosa matumaini hasa Sakina mkewe Mavitu alipoacha kazi.

Ukulima ulimwendea mrama na kuzalia katika janga la matatizo anakata tamaa maishani. Istoshe mtunzi anasema kwamba pesa zikiwaona maskini zinakimbia (uk40). Hapa pesa zinapewa sifa ya uhai ya kukimbia, matumizi haya ya tashihisi bado yanadhihirisha maudhui ya umaskini. Familia ya Mavitu pamoja na wanakijiji wa Imanga waliishi maisha duni ya uchochole. Hawakuweza kumudu mahitaji yao ya kimsingi kwa sababu ya kukosa fedha. Hii ndio inayosababisha wengine wao kama Sakina mkewe Mavitu kukata tamaa maishani. Na kwa mhusika kama Mavitu mwisho anajitia kitanzi.

Mwandishi amezitumia tashihisi hizi akitarajia kuonyesh athari inayoweza kusababishwa na umaskini.Anaonyesha jinsi umaskini unavyoweza kusababisha waja kuishi maisha ya yaliyojaa mateso.

Vile vile anaeleza jinsi Sakina alivyokuwa mrembo. Anasema kuwa urembo huu ungekinasa chochote kilichotua juu yake (uk40)  urembo unapewa sifa ya uhai ya kunasa matumizi haya ya  tashihisi hii yanajenga maudhui ya anasa. Sakina alikuwa

mrembo na aliweza kuvutia wanaume waliomwona. Hii inasababisha Mavitu mumewe kuacha kazi ili aje amdhibiti Sakina aliyekuwa anawavutia waume wengine waliomtaka awe na uhusiano wa kimapenzi nao.

Katika hadithi fupi ya ``Msamaria Mwema`` mtunzi ametoa maelezo yanayomhusu Likono aliyekuwa akielekea nyumbani baada ya kutoka maabadini kuabudu. Anasema Likono aliiona siku hiyo kama iliyoshiba matumaini (uk78). Kwa hivyo siku inapewa sifa ya uhai wa kibinadamu wa kushiba. Matumizi haya ya tashihisi yanadhihirisha nafasi ya dini.

Likono licha ya kuwa, mchochole alipoenda kanisani aliweza kujifariji na kuwa mwenye matumaini maishani ingawa alikumbwa na taabu chungu nzima. Hasa kuvaa magwanda, bintiye kukosa kazi miongono mwa matatizo mengine. Wakristu maskini walienda kanisani kujifariji Likono akiwa mmoja wao.

Kwa kutumia tashihisi hii matarajio ya mwandishi ni kutaka kuonyesha kuwa watu wa tabaka la chini wana ule uchu wa kumcha Mungu ili shida zao zitatuliwe kisha wale wa tabaka la juu wanaongozwa na mali wanayomiliki na kumcha mola kwa nadra sana.

Hadithi ya "Ngome ya Nafsi" pia mtunzi anasema kuwa Naseko alipoteka maji kisimani ndoa yake ilishiba maji (uk 99). Ndoa chombo kisicho na uhai kinapewa,sifa hii ya kibinadamu ya kushiba. Matumizi ya tashihisi hii yanadhihirisha maudhui ya uwajibikaji. Naseko baada ya kutoka shuleni aliwasaidia wazazi wake kazi za nyumbani kama kuteka maji miongoni mwa kange zingine.

Mtunzi anapoitumia tashihisi hii anataka kuonyesha majukumu ya jamii. Kuwa kila Mhusika alitekeleza jukumu alililohitajika kulifanya.

Pana matumizi ya tashihisi pia katika hadith fupi ya ``Ndimi za Mauti`` ambapo mtunzi anaeleza jinsi vile moto ulivyoteketeza bweni. Anasema kwamba nyumba zilimezwa na hasira za moto. Vile, vile mwangaza uliokuwapo ulitimua giza mbio(uk128). Moto na mwangaza zimepewa sifa ya kibinadamu ya kumeza na kutimua. Matumizi haya ya tashihisi yanadhihirisha maudhui ya uharibifu wa mali.

Kamaliza na mwenzake Mbunda wanateketeza bweni kwa lengo la kutaka kumfunza mwalimu mkuu funzo, ambaye wanasema anawakazia na kuwaadhibu. Uteketezaji huu unaharibu mali mengi hasa bweni, godoro, sare na vitabu vya wanafunzi. Wanafunzi 68 wanaangamia pia, mazingira yaliharibiwa pakubwa. Matarajio ya mtunzi kwa kutumia tashihisi hizi ni kutaka kuonyesha athari zinazosababishwa na moto.Moto huteketeza mali,husababisha kifo na huleta simanzi katika jamii.

Mwisho mtunzi anaeleza jinsi hali ilivyokuwa siku ya mazishi ya wanafunzi wa shule ya Angeko walioaga. Anasema kwamba baada ya maziko, mvua ilicharaza aridhi wakati ambao Mbunda aliwaza kujisalimisha kwa polisi (uk 134). Mvua hapa inapewa sifa ya kibinadamu ya kucharaza. Matumizi haya ya tashihisi yanasawiri maudhui ya majuto na msamaha, Mbunda anajuta kwa maovu aliyotendea wanafunzi wenzake. Hii ndivo sababu ya yeye kutaka kujisalimisha katika kituo cha polisi ili ukweli kupatikana na mwisho aombe msamaha baada ya kuhukumiwa.

Mwandishi ameitumia tashihisi hii akitaka kuonyesha athari ya kutenda maovu. Anaonyesha jinsi uovu hupelekea mja Kutiwa mbaroni au kujirudi mwenyewe kimawazo.

### 4.3. Matumizi ya Majazi

Wamitila (2003) anaeleza majazi kama hali ya kuwapa watu majina aghalabu ambayo huwa na maana.Vile vile, anasema kuwa majina haya yanaweza kuhusiana na tabia zao,maisha yao,matabaka yao, mtazamo wao na hata elimu yao.Isitoshe, anaeleza kwamba inawezekana pia mwandishi akasawiri mahali au mandhari na kuyapa majina yenye maana fulani. Hata hivyo,majazi ni hali ya kuwapa wahusika majina kulingana na mienendo yao. Pia, mahali au mandhari hupewa majina haya kulingana na sifa za mahali pale au mandhari hayo.

#### *4.3.1 Pendo la Heba*

Mwandishi ametumia majina ya kimajazi kusawiri ujumbe katika hadithi yake. Mifano ya majazi ni pamoja na Mheshimiwa Mlaji. Huyu ndiye alikuwa mbunge wa eneo la jangwani. Katika kamusi sanifu ya Kiswahili, neno mlaji lina maana ya kula au kuhujumu kwa siri.Jina hili linaonyesha kuwa Mlaji alikuwa amenyanyasa umma na watu wa eneo lake kwa masilahi yake binafsi. Akawa ni wa kula kila alichoweza kupata kiwe halali au haramu. Eneo alilowakilisha bungeni nalo liliitwa jangwani.Jangwa ni eneo kavu lenye mchanga usio na rutuba. Hii ina maana kuwa, mheshimiwa Mlaji alikuwa ameila mpaka ikaishiwa, na hivyo kuwa jangwa. Kwa

hivyo, uongozi wake ulikithi ufisadi na hapakuwa na maendeleo yoyote katika eneo lake.

Mwandishi amelitumia jina hili kimajazi akiwa na matarajio ya kutaka  kuizindua umma kuepukana na viongozi ambao wanaongozwa na misingi ya ubinafsi badala ya kujali masilahi ya umma kwa ujumla. Anaitahadharisha umma kuwashusha viongozi wa haiba ya sampuli hii na kuteua wale ambao wanashughulikia mahitaji na matatizo yanayokumba umma.

Pia, Diwani Mrija ni jina la kimajazi. Mrija ni kichombo cha kufvyonzea vitu maji maji.Vile vile, ni namna ya kujipatia mapato kwa kuwatumikisha wengine.  Hivyo ndivyo Diwani Mrija alivyowafanya watu wa Eneo Lake. Walimteua wakitarajia awasaidie lakini sivyo hivyo ilivyokuwa, kwani ilikuwa kinyume cha mambo. Pale hotelini Peponi anategemea wenzake kumnunulia chakula, mvinyo na vinywaji vingine. Anamhangaisha Maria pale hotelini badala ya kumsaidia.Badala ya kuwa kiongozi wa kutegemewa akawa wa kuwanyonya wengine.Diwani Mrija aliwatumia watu kwa manufaa yake mwenyewe.Hivyo jina lake linaakisi mienendo na tabia yake na kudhihirisha dhuluma katika jamii.

Mtunzi alitumia jina hili kimajazi akiwa na matarajio ya kutaka kuonyesha uozo wa viongozi wanaochaguliwa na wananchi kuwatumikia. Anawamulika  viongozi wa sampuli hii wanaojihusisha katika anasa na starehe kwa kutumia mali ya umma au ya wenzao isiyo yao. Anaitahadharisha umma kuepukana na kuwachagua viongozi wa namna hii ambao wanaongozwa na mikabala ya tamaa na ubinafsi.

Jina lingine la kimajazi ni Bwana Mkaange. Huyu ni mkuu wa shirika la biashara liitwalo Natija.Mkaange ni jina linalotokana na neno kaanga.Fasili yake ikiwa ni kudhulumu. Bwana Mkaange alikuwa anawadhulumu watu  hasa maskini, kutokana na uwezo wake wa kiuchumi. Shirika la kibiashara alilolisimamia liliitwa Natija kumaanisha faida kubwa. Lengo lake la biashara hii ni kujinufaisha mwenyewe pasipo kujali wateja na watu wengine.Ni katika harakati hizi ambapo   Mkaange aliwadhulumu watu ili apate faida kubwa.

Matumizi haya  ya majazi yametumiwa ili kuonyesha hulka za baadhi ya viongozi wenye uwezo mkubwa kiuchumi.Viongozi hawa ni dhulumati,wenye tamaa na ubinafsi mwingi. Hawana utu na huruma. Ingawa wana uwezo wa kuwasaidia maskini, si  karimu lengo lao lilikiwa kuwatumia maskini kwa manufaa yao wenyewe na si ya wahitaji hawa.

Bwana Mkaange pia alikuwa na hoteli yake ya kifahari ya Peponi. Peponi kulingana na wakristu ni mahali pazuri ambapo panaaminika kuwa roho za wafu huenda kupumuzika. Jina hili limetumiwa kudokeza kuwa mahali hapa palikuwa ni mahali pa starehe ambapo matajiri walikuwa wakienda kujistarehesha. Miongoni mwa matajiri waliopatikana mahali hapa ni pamoja na Mheshimiwa Mlaji, Diwani Mrija na Bwana Mkaange.Viongozi hawa ambao walistarehe katika hoteli hii ya Peponi walishiriki ulevi anasa na maovu ya kila namna. Ni mahali hapa wanapomwita Maria aje kuonana na Bwana Mkaange amsaidie kupata ajira. Lakini lengo lao kuu lilikuwa ni kumhusisha katika mapenzi.

Mwandishi wa hadithi hii amelitumia jina hili kimajazi kutaka kubainisha athari ya maovu yanayoendelezwa katika sehemu za burudani.Kwa hivyo, anawatahadharisha wananchi wa kiwango cha chini kuwa macho wanapoingia sehemu kama hizi wasije wakadhurika na matajiri wanaoendesha uozo huu.

Aidha,jina Maria ni la kimajazi. Hili ni jina ambalo limenukuliwa kutoka katika Bibilia takatifu. Katika Bibilia, lilitumiwa kurejelea mamake Yesu Kristo, mwasisi wa dini ya Kikristo.Maria huyu alilimbikiziwa sifa kemkem. Hizi ni pamoja na kuwa mtakatifu asiyekuwa na dhambi hasa ya uasherati. Hivi ndivyo Maria, msichana anayekwenda kutafuta usaidizi kwa Mheshimiwa Mlaji alivyokuwa.Hata mwandishi anasema," Maria,msichana mbichi ambaye alikuwa kahitimu chumba cha kumi mnamo mwaka uliotangulia,alikuwa na uzuri wa umbo si haba." (uk51).

Jina hili linaashiria utakatifu wake. Hata hivyo, kutokana na uhitaji akawa ni sharti aende kwa wenye uwezo wamsaidie.Badala yake nao wakawa wamejitolea kumdhulumu. Maria alipambana na Bwana Mkaange kwa ujasiri aliyenuia kufanya mapenzi naye katika mazingira ya Peponi.Hapa utakatifu ukapata ushindi.Maria hakuwa tayari kudhuru ubikira wake kwa mahasidi hawa.

Matumizi haya ya majazi yametumiwa na mwandishi kutaka kuonyesha kwamba sifa ya utakatifu ambayo haiwezi ikaenda sambamba na maovu. Mara nyingi hushinda maovu na kuweka waja huru. Wanaotaka kuhujumu utakatifu hubaki wameaibika na huwa hawafui dafu kutekeleza mipango yao ya uovu.

Isitoshe, Musa pia ni jina la kimajazi. Ni jina lililotumiwa katika Bibilia kurejelea kiongozi aliyekuwa na imani na Mungu. Kuwa na imani hii, aliweza kuwaongoza Waisraeli kutoka nchi ya utumwa ya Misri hadi Kanani nchi ya ukombozi.Jina hili linaashiria ukombozi. Hivi ndivyo ilivyokuwa na Musa mumewe Lea. Aliweza kuwakomboa wenzake kwa kuwashauri na kuwaelekeza.Kwanza, anamshauri mkewe Lea kuepukana na hali ya kuwa na macho ya nje.Pia, amemshauri Nyenzo jinsi ya kulea ndoa yake vizuri.Hata hivyo, alikuwa daktari aliyewatibu na kuwaponya wagonjwa. Kupitia mikononi mwake waja wengi walipata ukombozi.

Kupitia matumizi haya ya majazi, mwandishi anatarajia kuonyesha sifa za wahusika ambao wanastahili kuigwa na wanajamii  wengine. Anaonyesha kuwa wanajamii wanafaa kuwa watiifu na watakatifu maishani ili waweze kufaulu maishani mwao. Hasa viongozi wanaoteuliwa kuwaongoza  wengine wanastahili kuwa mfano bora.La sivyo, watawapotosha wanajamii  ambao mwisho watapotoka kimaadili na kukosa mwelekeo unaofaa katika maisha yao.

Mwisho ,majina Fadhila na Hasidi yametumiwa kimajazi. Fadhila ni jina ambalo linatokana na neno fadhila. Fadhila ni hali ya kuwa  karimu na mwenye shukrani. Jina hili linaashiria wema maishani. Fadhila aliishi vyema na wazazi wake hadi alipopotoshwa na MwanaMize Matongo kumwua mamake.Hasidi ni adui na mtu mwenye chuki.Hasidi akiongozwa na mamake MwanaMize Matongo alikuwa mwenye wivu, chuki na adui mkubwa wa fadhila. Hii imedhihirishwa pale anapomnyakua mume wa fadhila mwana wa Mfalme.Matumizi ya majina haya ya majazi yanatujengea maudhui ya wema na uovu maishani.

Matarajio ya mwandishi kutumia majina haya ya kimajazi ni kutaka kudhihirisha kwamba chochote mtu anachokitenda kwa uzuri matokeo huwa ya kuridhisha na ya kujivunia.Vile vile, mabaya yanayotendwa matokeo yake huwa huzuni na kilio.

### 4.3.2 Mayai Waziri wa Maradhi

Katika Diwani hii kuna pia matumizi ya majazi. Jina Mavitu ni la kimajazi. Mavitu ni jina ambalo limetokana na neno vitu. Linaloashiria kuwa na mali mengi. Hivi ndivyo alivyokuwa Mavitu hapo awali alipokuwa akifanya kazi katika Toray Mills. Kazi ya cherehani.Aliporudi kwake alinunuwa toroli nzima ya unga wa ngano na vitu vingine vya kula. Jina hili limetumiwa kimajazi kudokeza suala la ajira inayoleta mapato maishani.Mavitu alipofanya kazi hii ya kuajiriwa ofisini, llimpa mapato akaweza kuikimu familia yake. Anapoibadilisha na kufanya kazi ya ukulima, inaathiriwa na hali ya anga na kusababisha maisha duni ya Mavitu na aila yake.

Mwandishi amelitumia jina hili kimajazi akitarajia kubainisha umuhimu wa waja kuthamini kazi zao za mwanzo wanazozifanya. Anaonyesha athari inayoweza kuletwa na mapuuza ya kazi.

Vile vile, jina Mayai Waziri wa Maradhi ni majazi.Maradhi ni ugonjwa ambao hufisha ikiwa matibabu hayatatolewa.Hii inaambatana na hulka za mhusika Maradhi.Yeye kama waziri alisifu magonjwa na madaktari waliofisha wagonjwa.Matumizi haya ya majazi yanadokeza suala la uongozi potovu.Uongozi wa namna hii haukuwasaidia wananchi waliomchagua kuwaongoza.Mayai, baada ya kuchaguliwa miaka kumi iliyopita amekuwa akiwadhulumu tu wagonjwa hasa kwa

kusifu magonjwa kama kifua kikuu yanayoua  badala ya kutafuta tiba ya magonjwa haya.uongozi wa namna hii haukuwafaidi wananchi kwa vyovyote vile.

Matumizi haya ya  majazi yametumiwa na mtunzi  akitarajia kuonyesha athari inayoweza kuwepo hasa, nchi inapoongozwa na viongozi ambao si wawajibikaji. Hii husababisha kudhorora kwa maendeleo , vifo na hata umaskini.

Ukombozi, jina ambalo Mayai alimpa mwanawe ni jina la kimajazi.Ukombozi ni ile hali ya kuwa huru na kujiondoa katika utumwa au dhuluma. Jinsi vile ilivyo, Ukombozi aliweza kuwakomboa wale watoto tisa maskini ambao afya yao ilikuwa imedsorora. Aliwakaribisha nyumbani kwao na kuwapa chakula chote kilichopatikana nyumbani mwa Mayai. Watoto hawa walikula kilafi na wakawa huru kabisa nyumbani humu hata kiwango cha kutandikiwa  malazi na wakalala vizuri.

Katika matumizi haya ya majazi, mtunzi ameyatumia akitarajia kuonyesha athari inayoweza  kuwepo kama waja hawatajikomboa. Kwamba watasalia kuwa maskini na kutojimudu . vilevile watadhoofia kiafya.

Tukitamatisha, jina Kizito, Yule tajiri aliyemgonga Likono limetumiwa pia kimajazi. Mhusika huyu alipewa jina hili kwa sababu alikuwa na fedha,hivyo mfuko wake ulikuwa mzito. Aidha, ni mgumu au mzito wa kutenda wema wowote ule. Anapomgonga Likono kwa gari lake analazimishwa kumpeleka hospitalini. Mwisho, anatoweka bila kugharamia malipo hospitalini. Likono ambaye ni maskini anaachwa akihangaika, hana mbele wala nyuma hadi alipopelekwa hospital ya Kenyatta na

Dakitari msamaria mwema ndipo akatibiwa. Matumizi haya ya majazi yanadhihirisha maudhui ya ubinafsi na uchoyo.

Mwaandishi ametumia mbinu hii akitarajia kuonyesha sifa kuu ya ukarimu. Anaonyesha kwamba kutoa ni moyo na wala si utajiri. Hii ni kwa sababu licha ya matajiri kuwa na uwezo haimanishi kuwa wana moyo wa kutoa hata wanaposababisha tatizo wenyewe.

**4.4 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeshughulikia matumizi ya tashbihi, tashihisi na majazi katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili teule. Matumizi haya yameangaliwa katika Diwani ya *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine(1996) na Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine(2004).*Vile vile, matarajio ya athari zinazotokana na matumizi hayo yamejadiliwa kwa mapana.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii  ni hitimisho la utafiti.Katika sura hii muhtasari wa utafiti umetolewa.Pia,lengo kuu la utafiti limeelezwa pamoja na;upeo wa utafiti na yaliyomo katika kila sura.Matokeo ya utafiti yamejadiliwa kwa kina hasa kwa kueleza jinsi vile utafiti huu ulivyofanikiwa katika kuyaafikia malengo yake.Maeneo ambayo yanafaa kufanyiwa utafiti zaidi yamependekezwa.

### 5.1 Muhtasari

Tasnifu hii imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi,suala la utafiti,maswali ya utafiti,malengo ya utafiti,sababu ya kuchagua mada,upeo na mipaka,misingi ya nadharia ya kimtindo, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilishughulikia fasili, historia na maendeleo ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili hadi sasa.Sifa na vijenzi vya hadthi fupi vilishughulikiwa kwa kuonyesha uhusiano wake na mtindo katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.Katika sura hii, tuliweza kuonyesha ufafanuzi ambao umetolewa na wataalamu mbalimbali kuhusu fasili, historia na maendeleo ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili hadi sasa. Miongoni mwa wataalamu hawa ni: Mohamed  S.M, Mbatiah, Wamitila, MCOnyango, Msokile, Banzi,

Iribe Mwangi miongoni mwa wataalamu wengine.Maelezo yaliyotolewa katika sura hii yaliwekea utafiti wetu msingi imara.

Sura ya tatu, ilishughulikia matumizi ya taswira katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Pia,imeonyesha matarajio ya athari zinazotokana na matumizi hayo ya taswira katika hadithi fupi teule.Hapa,tumeeleza jinsi mtunzi hutumia taswira kuibua ujumbe wake.Vile vile,tulionyesha namna mwandishi hutumia taswira akitarajia wasomaji kupata funzo husika kutokana na matumizi hayo.

Nayo sura ya nne imeshughulikia matumizi ya tashbihi, tashihisi na majazi katika hadithi fupi teule za Kiswahili.Pia,matarajio ya athari zinazotakana na matumizi ya mitindo hii ya matumizi ya lugha yameelezwa kwa kina.Mitindo hii imetumiwa na mwandishi katika hadithi fupi zilizoteuliwa kuibua ujumbe wake.

Sura ya tano ni hitimisho la utafiti.Imeelezea muhtasari wa kila sura kwa kina.Vile vile imefafanua matokeo ya utafiti.Istoshe, sura hii pia imependekeza maeneo ambayo yanaweza kufanyiwa utafiti baadaye.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulipambanua malengo matatu makuu.Kuhusu lengo la kwanza, utafiti ulipata ya kwamba hadithi fupi za kisasa za Kiswahili hutumia mitindo kama vile: taswira,tashbihi,tashihisi na majazi kuibua dhana husika. Taswira, ilitumiwa kuonyesha jumla ya mkusanyiko wa picha ambazo ziliundwa na maelezo ya waandishi wa hadithi fupi teule za kisasa za Kiswahili. Tashbihi ilitumiwa hasa katika kulinganisha vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti kwa kutumia vifananishi kama vile: mithili ya, kama, mfano

wa, miongoni mwa vifananishi vingine.Nayo tashihisi ilitumiwa kuvipa vitu visivyo na uhai sifa ya uhai ya kibinadamu.Vitu hivi vilipewa sifa ya kuweza kutenda kama mwanadamu.Mwisho, majazi ilitumiwa kuwapa watu au mandhari majina aghalabu ambayo huwa na maana katika hadithi fupi teule za kisasa za Kiswahili.

Lengo la pili la utafiti lilihusu matumizi ya mitindo hii katika hadithi fupi teule za kisasa za Kiswahili.Matumizi ya mitindo hii,yaliweza kuibua ujumbe wa mwandishi.Kwa kutazama matumizi ya taswira,tashbihi,tashihisi na majazi katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili;utafiti ulipata kwamba matumizi ya mitindo hii yaliibua ujumbe wa waandishi.Miongoni mwa maudhui yaliyoibuliwa na matumizi ya mitindo hii ni:umaskini,utabaka ,ukosefu wa utu,changamoto zinazoathiri sekta ya elimu na matibabu,dhuluma za kijinsia,ukombozi,ukosefu wa usalama,ubabedume na ubinafsi.

Lengo la tatu lilihusu matarajio ya athari zinazotokana na matumizi ya mitindo hiyo.Matumizi haya ya taswira, tashbihi, tashihisi na majazi yaliweza kuibua matarajio ya mwandishi.Utafiti ulipata kuwa, kwa kutumia mitindo hii mtunzi alitarajia wasomaji kutambua mambo kadha wa kadha.Hasa suala la kuthamini elimu,hali halisi ya umaskini,kuthamini utu maishani,usawa wa jinsia,uaminifu katika masuala ya ndoa miongoni mwa matarajio mengine.

### 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu ulijikita katika mada ambayo ni mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.Matumizi ya mitindo kama vile: taswira, tashbihi, tashihisi na majazi yalishughulikiwa. Katika kuendesha utafiti huu, ilidhihirika kwamba kuna maeneo

mengine yanayofaa kufanyiwa utafiti zaidi.Kwa ajili hii, ni mapendekezo yetu kwamba,utafiti ufanywe kuhusu matumizi ya mitindo kama vile:kuchanganya ndimi,chuku, na balagha katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.Pia,utafiti ufanywe kuhusu muundo wa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.Vile vile,utafiti zaidi ufanywe kuhusu aina mbalimbali ya wahusika wanaotumiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

## MAREJELEO

Banzi, A. (1980). Tamaa Mbele na Hadithi Nyingine. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Crystal,D.&Davy,D.(1969) World and Investigating English Style.London:Longmans.

Diyanni, R. (2000), Reading, Finction, Poetry and Drama U.S.A: The Mac Graw Hill Companies, Inc.

Elizabeth, F.P. (1998), Study Guide: Literary Visions. New Jersey: Prentice- hall Inc Publishers.

Grand Saigne, J. (1985) (Mha.) African Short Stories: Nairobi: Macmillan Press.

Halliday, M. A. K. (1971). Linguistic Function and Literary Style: An Inquiry into the Language of William Golding's The Inheritors. in S. Chatman (Ed.), Literary Style: A Symposium (Pp. 330-368). London: Oxford University Press.

Iribemwangi, P.I. (2007). (Mha.). Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine. Nairobi. E.A.E.P.

Kinge'i G.K. na Wafula R.M. (1996), (Wah). Pendo la Heba na Hadithi Nyingine. Nairobi: Chama cha Waandishi; Kenya.

Leech N.G. and Short M.H. (1981), Style in Fiction. A linguistic Introduction to English Fictional Prose. London:Longman.

Lodge D. (1972), (Mha) 20th Century Literary Critism: London:Longman.

Lodge, O. (1972), 20TH Century Criticism, Longman: London.

McOnyango, O. (2006). Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine. Nairobi: Focus Publishers.

Mohochi E.S. (1997), 'Hadithi Fupi Utanzu Uliopuuzwa' katika Mulika Nambari 24. Tuki: Dar es Salaam.

Mohochi, E.S. (2000), Fasihi ya Kiswahili katika Karne ya 21 Nafasi ya Hadithi Fupi. Dar es Salaam, Tuki.

Mphahelele, E. (1996). A Guide to Creative Writing. Nairobi: Dar es Salaam; Educational Publishers.

Msokile M. (1992), Misingi ya Hadithi Fupi. Dar es Salaam: Dar es Salaam University.

Mukopi, M.H. (2005). "Hadithi Fupi kama Utanzu Mahuluti". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Muusya J.K (2012). "Mandhari katika Hadithi Fupi: Ulinganishaji wa Diwani za Pendo la Heba na Hadithi Nyingine na Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mbatiah( 2000), Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine Jomo Kenyatta Foundation :Nairobi

Ngara, E. (1982). Stylistic Critism of the African Novel. London: Nairobi: Heinemann.

Njogu, K. (2007), (Mha). Kiswahili na Elimu Nchini Kenya. Koibe Press: Nairobi.

Ntiba, O.G (2011). Dhamira na Mtindo katika Hadithi Fupi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Osore, K.M. (1974). "Uhakiki wa Kiisimu wa Riwaya za Suleiman Mohamed". (Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Poe, E.A. (1938). The Complete Tales and Poems: New York: Random Housen Inc.

Saussure, F. DE (1995). A course in General Lingusitic,  New York: MGraw-Hill.

Senkoro, E.F.M.K. (1988). Ushairi: Nadharia na Tahakiki. Dar es Salaam: University Press.

Senkoro, F.E.M.K. (1982). Fasihi: Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K.W. (20002a). Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi. Nairobi: Focus.

Wamitila, K.W. (2002b). Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia: Focus Books.

Wamitilia, K.W. (2002c). Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila , KW.(2003), Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi . Nairobi; Focus.

Wamitila .KW. (2004),(Toleo Jipya), Kichocheo cha Fasihi Simulizi Na Andishi. Nairobi